**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 1 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007

**MHE. FATMA OTHMAN ALI (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 317

**Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji yanayotumika Mpanda Mjini ni pamoja na maji ya mtaro wa Manga; na kwa kuwa, vyanzo vya mto Manga ni kutokana na chemchem zaidi ya tano katika vilima vya Kabenga katika makazi ya Wakimbizi Katumba, vilima hivyo vimeharibika kutokana na hali ya ukataji miti, mashamba na makazi ya Wakimbizi:-

(a) Je, Serikali na Jumuiya za Kimataifa zina mpango gani wa kurekebisha dosari za uharibifu wa mazingira uliofanywa na Wakimbizi?

(b) Je, Jumuiya za Kimataifa zitasaidia kukarabati maeneo hayo yaliyoharibiwa; pia vyanzo vya maji ndani ya makazi vimeharibiwa kutokana na kupanuka kwa makazi na kufuata maeneo mapya ya rutuba?

(c) Je, Jumuiya za Kimataifa zimesaidia vipi maeneo mengine yenye Wakimbizi nchini katika kurekebisha athari za uharibifu wa mazingira na makazi yaliyo katika Wilaya ya Mpanda na yalinufaika vipi na mpango huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:_

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Wakimbizi ya Katumba yenye wakazi 106,300 yanayohudumiwa na Serikali tangu mwaka 1978. Mwezi Agosti 2004, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira ilitembelea makazi hayo na vijiji vya Kambuzi, Nsanda, Urwira pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Serikali ilizingatia ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Arfi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurekebisha dosari za uharibifu wa mazingira, pamoja na mambo mengine Serikali imetekeleza yafuatayo:-

- Kuwaondoa Wakimbizi katika maeneo waliyovamia na kurejeshwa kwenye eneo walilotengewa awali;

- Kupima, kuweka bayana mipaka na kutayarisha ramani ya eneo la makazi ya Wakimbizi ya Katumba; na

- Shirika lisiko la Kiserikali la *Africare*, kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Mpanda, wanafanya doria katika eneo la misitu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID)* kwa kupitia *Africare,* limeingia mkataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya

kufanya tathmini ya uanzishaji wa maeneo tengefu ya hifadhi za jamii (*Community-Based Natural Resources Management Areas)* katika Wilaya ya Mpanda, yakiwemo maeneo yanayozunguka Makazi ya Wakimbizi ya Katumba. Shirika hilo pia limeanzisha mradi wa hifadhi ya Ugalla (*Ugalla Community Conservation Project (UCCP).* Lengo ni kuhamasisha jamii zinazozunguka mfumo wa ikolojia ya Ugalla, ikiwemo hifadhi ya msitu wa Mpanda Kaskazini Mashariki, katika kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali yake. Ni matumaini yangu kwamba kwa kupitia mradi huu, maeneo yaliyoharibiwa, vikiwemo vyanzo vya maji na miti iliyokatwa, yatarudi katika hali yake ya awali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya za Kimataifa zimekuwa zikisaidia hifadhi ya mazingira katika maeneo ya Wakimbizi hapa nchini. Kuanzia mwaka 1996 hadi mwaka 2000, mradi wa "*Special Project for the Rehabilitation of Refugee Affected Areas (SPRAA)* uliokuwa unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ulisaidia, pamoja na mambo mengine, hifadhi ya mazingira katika Mkoa wa Kagera. Hivi sasa, mradi wa miaka mitatu (3) unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark kwa gharama ya shilingi bilioni kumi unasaidia hifadhi ya mazingira, ujenzi wa miundombinu, na kampeni dhidi ya UKIMWI, katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Mradi huu unaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa upande wa Mikoa ya Tabora na Rukwa, Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* kupitia programu ya hifadhi ya mazingira na maliasili (*Environment and Natural Resources Management*), linasaidia, pamoja na maeneo mengine hapa nchini, hifadhi ya maeneo ya Wakimbizi, likiwemo eneo la Makazi ya Wakimbizi la Katumba katika Wilaya Mpanda.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yenye kutia faraja ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa napenda kumwuliza swali moja la nyongeza.

Wakimbizi wanalazimika kutoka katika eneo la makazi na kutafuta maeneo mapya yenye rutuba kwa sababu ya ardhi kuchoka. Na si ardhi katika makazi tu ambayo yamechoka na maeneo mengine katika Wilaya ya Mpanda ambayo yametumika kwa kilimo kwa muda mrefu. Je, Serikali inawashauri vipi wananchi ili waweze kurutubisha ardhi zao zilizochoka ziweze kutoa tija tena?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wananchi wanashauriwa kufuata maelekezo ya wataalamu kuhusu matumizi bora ya ardhi.

Pili, Halmashauri inabidi zitenge maeneo mbalimbali kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi. Kwa mfano, kutenganisha maeneo ya wakulima na maeneo ya wafugaji.

Mwisho, ni kutumia ardhi vizuri tu pamoja na kuiacha pale ambapo imechakaa ili uoto wa asili uweze kurudi tena.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wakimbizi walioko katika Makazi ya Katumba walikuja zamani za miaka ya 1970. Lakini sasa hivi tunawaona Wakimbizi waliokuja miaka ya 1990 tuseme machafuko ya miaka ya 1994 sasa wanarejea kwao. Je, ni lini hawa Wakimbizi wa Katumba watarejea kwao ili kuleta suluhishi la kudumu la hifadhi ya mazingira?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa hivi Wakimbizi wanaorudi ni wale waliokuja mwaka 1994 na ndiyo ambao wako kwenye Makambi hasa katika Mkoa wa Kigoma na Kagera. Ndiyo makubaliano yetu ya Shirika la Wakimbi *UNCHR* kwamba awamu ya kwanza tuwarudishe wote wale ambao wako kwenye Makambi na mpaka sasa karibu 208,000 wamesharejea na zoezi linaendelea. Tukishamaliza walioko kwenye makambi kwa mujibu wa makubaliano yetu awamu ya pili itahusu wale ambao wako katika makazi waliokuja miaka ya 1972 wako katika makazi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu.

Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wananchi wa Tanzania kwamba wale Wakimbizi wa mwaka 1972 kwanza bado ni Wakimbizi na zamu yao ikifika wote itabidi warudi kwao. *(Makofi)*

Na. 318

**Miti Inayoathiri Vyanzo vya Maji**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inahimiza upandaji wa miti kila mahali ili kutunza vyanzo vya Maji; na kwa kuwa, wananchi wa Mkoa wa Singida waliitikia wito huo na kupanda miti mingi hasa kwenye mashamba yao; na kwa kuwa, baadhi ya maeneo yalianza kuwa makame zaidi na kukausha kabisa vyanzo vya maji na baadhi ya mashamba kutokuwa na rutuba:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti wowote wa kupata uhakika wa maeneo yanayoathiriwa na miti hiyo?

(b) Je, ni aina gani ya miti inayoathiri vyanzo vya Maji na kumaliza rutuba ya mashamba kwa mazao?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya lalamiko hilo toka kwa wananchi hasa wa Mkoa wa Singida?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata (Viti Maalum), lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Baada ya uzoefu wa muda mrefu katika kampeni ya upandaji miti, Serikali na jamii kwa ujumla imebaini kuwepo kwa aina ya miti ambayo husababisha ukame na kukausha vyanzo vya maji. Kwa mfano Singida na maeneo mengi nchini yameathirika na miti aina ya mikaratusi (*Eacalyptus spp*). Utafiti wa kitaalam umefanywa katika sehemu mbalimbali nchini ukihusisha aina ya miti, aina na hali ya udongo, hali ya hewa, upatikanaji wa maji na athari au faida ya miti hiyo kwa mazao. Utafiti huo umefanywa na unaendelea kufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu *(TAFORI),* Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Kilimo na Misitu *(International Centre for Research on Agriculture and Forestry (ICRAF).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ya kigeni ambayo huathiri vyanzo vya maji na kuharibu rutuba ya mashamba mara nyingi ina mizizi inayoambaa juu juu na majani yake hayaozi haraka. Aina ya miti hiyo ni pamoja na Mikasia ya Australia (*Australian acacias*), Mikaratusi (*Eucalyptus spp*), Misindano (*Pines* na *Cypress*). Miti inayofaa kwa kilimo misitu, ni ile yenye mizizi mirefu kwenda chini na yenye majani yanayooza haraka yakichanganyika na udongo. Huachia virutubisho vingi ardhini na haiharibu mimea mashambani. Hii ni mimea ya jamii ya mikunde; mfano Milusina (*Leucaena spp*). Mingine ni Migrivea (*Grevillea robusta*), Milonge (*Moringa olifera*), na Minyasa (*Newtonia buchananii).* Aina ya miti ya asili inayofaa kupandwa katika vyanzo vya maji ni pamoja na Mikuyu (*Ficus sycomorus*), Mirumba pori (*Ficus thonningii*), Michenje na Mikenge (*Alibixia spp),* Mihale (*Acacia Nilotica)* na Mikungu *(Ficus katapa).*

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 1 Aprili, 2006, Serikali ilitoa tamko kuhusu hatua za kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji. Halmashauri za Wilaya na Miji zimetakiwa kutambua maeneo ya vyanzo vya maji; kutambua maeneo yenye miti isiyofaa na kuiondoa na kupiga marufuku upandaji wa aina hiyo ya miti; kuandaa vitalu vya miche inayofaa na kuhamasisha upandaji wa miti hiyo kwenye vyanzo vya maji na kuandaa na kutangaza orodha ya aina ya miti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia mojawapo ya kuhifadhi ardhi na mazingira ni kuacha ardhi isitumike ili uoto wa asili ujitokeze. Kwa njia hii miti yenye asili ya maeneo husika huota tena na kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni, 2006 tulisherehekea, Kitaifa, Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho hayo yalifanyika Singida kwa madhumuni yanayofanana na maudhui ya swali la Mheshimiwa Mlata yaani Majangwa na Kuenea kwa Halii ya Jangwa: Tusisababishe Maeneo Kame kuwa Majangwa. Nachukua nafasi hii; kwa niaba ya Serikali kuwashukuru viongozi wa Mkoa wa Singida, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa huo, na wananchi wa Singida kwa kufanikisha maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanamazingira namba 1, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, ameniagiza jana nami nafurahi na natoa taarifa kwamba sasa hajambo na ni mzima wa afya. Anatarajia kurudi wakati wowote kuanzia sasa wiki hii. Anawashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge na wananchi

wote kwa salaam zao za kumtakia kheri na afya njema na dua zao kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nitakuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa amesema kwamba ni kweli kabisa kuna miti ambayo inaathiri vyanzo vya maji. Wananchi wa Mkoa Singida waliitikia wakapanda miti hiyo ambayo ameitaja na tayari kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekwisha kuathirika. Je, Serikali ina mpango gani kuweka miti mbadala na kuwawezesha wananchi wa Mkoa wa Singida ambao tayari wamekwisha kuathiri maeneo hayo kwa kuwawezesha.

Pili, je, Serikali kwa nini huachia mambo kama haya kuendelea hadi kuleta madhara ndipo kuchukua hatua ya kutibu madhara haya badala ya kuzuia? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo ameathirika nini cha kufanya katika jibu langu la swali la msingi tumeelekeza kwamba Halmashauri ziyatambue maeneo hayo na kuondoa miti hiyo ambayo inaharibu vyanzo vya maji na inaleta ukame. Vile vile nimejaribu kutaja aina ya miti ambayo inaweza kukua vizuri tu katika maeneo ya sehemu za Kati ya Tanzania, Singida ikiwa mojawapo.

Kuhusu kuwawezesha wananchi tunahitaji Halmashauri zihuishe katika mipango yake yote suala zima la hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na upandaji miti. Lakini vile vile Taasisi Zisizo za Kiserikali hasa hasa vikundi vya kijamii tunaweza tutavisaidia kwa kuvielekeza wapi vinaweza kupata fedha za kushughulikia suala zima la upandaji miti na hifadhi ya mazingira.

Kuhusu Serikali kuachia masuala haya mpaka yalete madhara. Ningependa kusema tu kwamba pamoja na kutaja miti ambayo haina faida kwa maana ya kuleta ukame na kuharibu vyanzo vya maji vina faida mbadala. Faida nyingine ni kwanza kuni lakini vile vile mbao kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, ni kiasi cha kutambua tu wapi upande miti na ya aina gani.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kule Njombe tunastawisha miti ya misindano ambayo ikiota chini yake hakuna mmea mwingine wowote utakaoweza kuota tena.

Miti ya Miwati, Mikaratusi hii miti yote ni ya kigeni lakini kutokana na miti hii ambayo inaota kwa haraka na kutatua tatizo la mbao nchini, tuna Wasukuma na makabila mengine mengi ya Tanzania yanakuja kuchukua mbao kule Njombe. Na kule ndio chanzo cha mito mingi pamoja na Mto wa Ruaha na Kilombero.

Je, Waziri anashauri nini akilinganisha faida ya miti hii kiuchumi na kwa maana hiyo na kwa upande wa mazingira. Njombe angeshauri tupande miti gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ya biashara hasa ambayo inaharibu vyanzo vya maji ushauri ni kwamba ipandwe katika maeneo ambayo tunahitaji kuokoa ardhi kwa sababu ardhi imeharibika.

Lakini pale ambapo kuna mvua nyingi, hakuna tatizo la maji basi unaweza hata ukapanda hii miti kibiashara kama inavyofanyika Njombe na Mufindi.

Na. 319

**Zana za Kisasa Kwa Wavuvi**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi wana uwezo, maarifa na dhamira ya kujitegemea kiuchumi; na kwa kuwa, wananchi wanaoishi kandokando ya Ziwa Nyasa uchumi wao unategemea sana uvuvi katika Ziwa hilo, ingawa uvuvi huo bado unafanyika kwa njia za kizamani zinazoharibu sana mazingira na kusababisha hali ya uchumi wa wananchi hao kuwa duni ikilinganishwa na wenzetu wa upande wa pili wa nchi ya Malawi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kupata zana bora na za kisasa za uvuvi ili kuwaletea wananchi ongezeko la uchumi wenye tija na kupunguza kwa kiasi kikubwa athari za uharibifu wa mazingira wa kukata miti?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, uchumi wa wananchi wanaoishi kando kando ya Ziwa Nyasa unategemea sana uvuvi katika Ziwa Nyasa na pia zana za uvuvi wanazotumia ni duni ambazo ni pamoja na makokoro na nyavu zenye macho madogo na zinachangia katika uharibifu wa mazingira ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kupata zana bora za uvuvi, Serikali imeendelea kuhamasisha wavuvi hao kuunda vyama vya kuweka na kukopa kutokana na mapato yao ili waweze kununua zana bora za uvuvi.

Aidha, Serikali imeendelea kuwahamasisha wavuvi nchini kwa kuwapa mafunzo kuhusu ulinzi wa rasilimali ya uvuvi pamoja na kuunda vikundi vya uzalishaji na vyama vya ushirika kwa lengo la kuwawezesha kuwa na uwezo wa kukopa katika Taasisi za fedha nchini. Wavuvi 50 katika Mkoa wa Ruvuma walipata mafunzo juu ya ulinzi wa rasilimali, jinsi ya kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa pamoja na mbinu za kupambana na umaskini katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Ludewa na Kyela inao mkakati wa kuwafundisha wavuvi wa Ziwa Nyasa kutumia zana bora zaidi za kuvulia samaki ili waongeze kipato chao.

Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara imepanga kuwafundisha kwa vitendo wavuvi kutoka Wilaya ya Mbinga kuwa uvuvi wa kutumia ndoana unaweza kuwapatia samaki wakubwa na wenye bei nzuri zaidi. Mafunzo hayo yatahusisha kikundi kimoja cha wavuvi wapatao 30 kwa kuwashirikisha maafisa uvuvi na wavuvi wazoefu. Zoezi hili limetengewa kiasi cha shilingi 14,840,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira Ziwa Nyasa, katika mwaka wa fedha 2006/2007 itaendesha mafunzo ya kuhamasisha jamii ya wavuvi juu ya ushirikishwaji jamii ya wavuvi kwenye kulinda, kuendeleza na kuvuna kwa busara rasilimali ya uvuvi na kutunza mazingira kwa ujumla katika eneo la Mto Ruhuhu ambao upo mpakani mwa Wilaya za Ludewa na Mbinga.

Mto Ruhuhu ni maarufu kwa mazalia ya samaki aina ya Mbelele na unamwaga maji yake kwenye Ziwa Nyasa. Mafunzo haya yametengewa kiasi cha shillingi 3,800,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kutoa elimu ya ushirikishwaji wa jamii ya wavuvi kwenye menejimenti ya uvuvi na hifadhi ya mazingira, jamii ya wavuvi watahamasishwa katika kutambua umuhimu wa kuwa na sheria ndogo ndogo zitakazosaidia kudhibiti uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira ya samaki pamoja na ukataji miti hovyo kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wenzetu wa Malawi wanatumia ziwa hilo hilo lakini wanatumia kulisha samaki kwenye mazalia ya samaki na hivyo kusababisha kupata samaki wengi zaidi.

Je, Serikali haioni kwamba mpango huo ni mzuri kwetu pia tukalisha samaki ili wavuvi wetu waweze kupata samaki wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Capt. Komba, Mheshimiwa Naibu Waziri anaomba urudie swali lako hajalisikia sawa sawa.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Pole sana Mheshimiwa Waziri. Swali langu ni hivi.

Kwa kuwa wenzetu wa Malawi wana utaratibu wa kulisha samaki kwenye mazalio yao ya samaki na hivyo kusababisha kupata samaki wengi na kuongeza uchumi wao. Je, mpango huo si vizuri na sisi tukauridhia ili tulishe mazalia ya samaki ili wavuvi wetu waweze kupata samaki wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea kwa upande wa Ziwa Nyasa kuna mambo mawili. Kwanza upande wa Ziwa Nyasa kuna kina kifupi cha maji kinachotokea ni kwamba wakati upepo wa kusi unapovuma kwa kuwa kina cha maji ni kifupi huwa kinachanganya yale maji matokeo yake ni kwamba inachanganya inatoa lile tope la chini ambalo lina chakula cha samaki na ambacho kinasaidia sana katika kuzaana kwa samaki.

Kwa hivyo unakuta samaki wanazaana sana upande wa Malawi kuliko kwetu ambako kina ni kirefu. Wakati upepo wa kusi ukipita kwetu kwa kuwa kina ni kirefu maji yale hayawezi kuchanganyika sana kama yanavyochanganyika upande wa Malawi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, upande wa Malawi wanachofanya kuna ufugaji wa samaki katika uzio. Wakifugwa katika uzio maana yake ni kwamba wale samaki hawawezi kuwa na uwezo wa kutoka katika uzio na kwenda kutafuta chakula katika sehemu nyingine. Hivyo basi inabidi wapewe chakula katika uzio ule. Lakini chakula hicho huwa ni chakula ambacho kinatengenezwa viwandani kuhakikisha kwamba hakileti madhara katika Ziwa, hicho ndicho ambacho kinafanyika.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa uvuvi unaofanyika Ziwa Nyasa unafanana sana na uvuvi unaofanyika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na maziwa mengine yanayopatikana ndani ya nchi hii na kwa kuwa zana zinazotumiwa na wavuvi hawa zinafanana sana na hizo zinazotumika katika Ziwa Nyasa; na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanatoa matumaini makubwa sana kwa mkakati ambao Serikali inao kuwasaidia wavuvi wanaofanya shughuli za uvuvi, ninaomba kujua kauli ya Serikali kuhusu uvuvi unaopatikana nje ya maeneo ya Ziwa Nyasa kwa mfano waliko katika Ziwa Tanganyika, Victoria na hasa maeneo ya Jimbo la Sengerema ni nini kauli yao kuwasaidia wavuvi hawa kwa vile shughuli wanayoifanya inasiadia sana kuongeza uchumi wa Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngeleja nafikiri swali hilo ulitengeneze vizuri ni swali la msingi sana kwa Jimbo la Sengerema nafikiri uliweke vizuri na ulilete kwa utaratibu ule wa maswali ili lipate majibu yote yanayohitajika.

Na. 320

**Ukarabati wa Magofu ya Kilwa Kivinje**

**MHE. HASNAIN G. DEWIJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kilwa ni Mji wa Kitalii na kwa kuwa katika mji huu mkongwe yapo magofu licha ya kwamba yanavutia sana watalii, lakini pia yanaweka kumbukumbu za historia na kwa kuwa, magofu hayo yameanza kuharibika na kuwa hatari ya kutoweka kama juhudi za kuyakarabati hazikuchukuliwa haraka.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuyakarabati magofu hayo kabla hayajatoweka kabisa ili kuimarisha utalii na kutunza kumbukumbu za mambo ya kale katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewiji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua ukweli kwamba magofu ya Kilwa Kivinje ni kivutio vya utalii Wilayani Kilwa na pia ni Kumbukumbu muhimu ya kihistoria na akiolojia. Aidha kuna umuhimu wa kuyaendeleza magofu hayo ili yasiwe tu kumbukumbu bali pia yaweze kuwa kichocheo cha shughuli za kimaendeleo katia mji wa Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Kilwa Kivinje lina majengo mengi yenye umuhimu kihistoria na kisanifu. Majengo ambayo mengi ya hayo yanamilikiwa na watu binafsi. Aidha hali ya majengo hayo ni mbaya na mengi yapo katika hatari ya kubomoka baada ya wamiliki wake kuyatelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Serikali inaandaa utaratibu wa kuongeza eneo la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ambako liko kwenye orodha ya Urithi wa Dunia ili lihusishe pia Kilwa Kivinje. Makabrasha yote hayo yamewasilishwa *UNESCO*, Makao Makuu Paris, Ufaransa ili kuanza mchakato huo.

Endapo eneo hili litafanikiwa kuwa sehemu ya Urithi wa Dunia litakuwa kwenye nafasi kubwa ya kupata misaada ya kimataifa.

(ii) Serikali inafanya uchambuzi yakinifu kuhusu idadi ya majengo pamoja na gharama halisi ya ukarabati kupitia Mradi wa *MACEMP* ambao unagharamiwa na Benki ya Dunia.

(iii) Serikali imeanza kazi ya kufanya ukarabati wa boma huko Kilwa Kivinje na kwa kuzingatia umuhimu huo idara imehamisha mafundi wawili kutoka Bagamoyo kwenda huko ili kukidhi mahitaji ya kazi hii muhimu.

(iv) Kuhamasisha wananchi kuyatumia kuyalinda na kuyakarabati majengo hayo ili yawe na matumizi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma hiyo Wizara yangu itategemea sana ushirikiano wa wananchi wa Kilwa Kivinje hasa wamiliki wa majengo hayo na uongozi wa Halmashauri ya Kilwa. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWIJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana mimi nina maswali mawili ya kuongeza hapo. La kwanza Serikali haioni umuhimu wa kutenga pesa za ndani ili magofu hayo yakarabatiwe kwa haraka ili tusipoteze historia ya Kilwa?

La pili, kuna Boma la Kilwa Kivinje. Je, Serikali kama anapatikana mfadhili aweze kuweka *museum* pale anaweza kukubaliwa kuweka *museum* ya historia ya Kilwa ili ihifadhiwe pale kwenye Boma?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi Serikali inatambua umuhimu wa magofu haya na nimeeleza kwamba Serikali inafanya kila jitihada pamoja na kutumia fedha zake za ndani na pia kuomba wafadhili waweze kusaidia ili kuyakarabati baadhi ya haya majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Boma, tayari Serikali imekwishaanza kazi katika boma hili lililokuwa la Wajerumani. Tayari imeanza kufanya ukarabati mdogo mdogo, imeweka nguzo, kuzuia paa lisiweze kuanguka na kama nilivyoeleza kuna mafundi wawili ambao wametoka Bagamoyo wamepelekwa Kilwa kwa ajili ya kazi hiyo na iwapo atapatikana mfadhili atakayetaka kutengeneza *museum* anaweza kufanya hivyo lakini kwa kupata ushauri kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali mja la nyongeza. Kwa kuwa pale Kilwa Kivunje kuna soko lenye historia kubwa ya taifa hili. Mahala ambapo biashara ya utumwa ilifanyika kipindi hicho watumwa wakiwa wananadiwa. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kupanua soko hilo ili likidhi mahitaji ya sasa kwa wakazi wa Kilwa sambamba na kuhifadhi historia ya taifa hili kwa sehemu ya Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kujibu naomba nimpongeze kwa kuonyesha *interest* kwa kuhusiana na magofu ya Kilwa Kivinje pamoja na kwamba yeye anatoka sehemu nyingine. Soko la

Kilwa Kivinje ambalo mwanzo lilikuwa ni soko la watumwa lina umuhimu wake. *(Makofi)*

Kwa sasa soko hilo linatumiwa kama soko la kuuza bidhaa kwa ajili wananchi wanaoishi pale jirani. Serikali inachofanya ni kwamba, iwapo wananchi wa Kilwa Kivinje wataonyesha *interest* ya kutaka soko lile liweze kukarabatiwa na kuongezwa wakionyesha hiyo, Wizara iko tayari hakuna kuwasaidia kuandika *write u*p nakutafuta wafadhili waweze kuja kusaidia kulikarabati soko hilo na kuliongeza kwa sababu soko lile kwanza ni dogo. Wafanyabiasha mle ndani wamesongamana sana na wako wengine wanauza bidhaa zao nje. Hilo ni wazo zuri na litafanyiwa kazi lakini wannchi wa Kilwa Kivinje waonyeshe wana nia hiyo. *(Makofi)*

Na. 321

**Tanzania *Housing Bank (THB)***

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya nyuma kabla ya mwaka 1995 Serikali ilianzisha Benki ya Nyumba *(THB)* kwa lengo la kutoa mikopo ya kujenga nyumba bora: na kwa kuwa, nchi kama Kenya, Uganda na India zinatoa huduma kama hiyo kwa wananchi wake; na kwa kuwa *THB* iliifungwa mwaka 1995:-

(a) Je, kwanini *THB* ilifungwa?

(b) Je, Serikali inampango gani wa kufufua Benki hiyo ili iendelee kuwa kichocheo cha kuboresha miji kwa kujenga nyumba bora?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Nyumba Tanzania (*THB*) ilifungwa mwaka 1995 kutokana na matatizo ya kifedha na kiutendaji. Matatizo hayo yalipelekea Benki hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kukusanya amana na kuzielekeza kwenye miradi ya majengo ya kuishi na biashara, ilishindwa kutoa mikopo, ushauri na misaada ya kiufundi kwa watu binafsi au vikundi vilivyokuwa vinajishughulisha na ujenzi wa nyumba. Pia ilishindwa kusimamia mifuko maalum ya Serikali iliyokuwa imewekwa chini yake kwa uangalizi (*Management of Special Government Funds)* kwa lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuifufua iliyokuwa Benki ya Nyumba Tanzania, bali itaandaa utaratibu utakaowezesha kuwepo kwa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba kwa Watanzania wote. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa

linaloshughulikia Makazi Duniani, (*UN-HABITAT*) tumeandaa Taarifa yenye Mapendekezo ya Utaratibu utakaowezesha kuwepo na mikopo nchini kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Uchambuzi wa mahitaji muhimu ya kuwa na mikopo nchini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba umekamilika. Matokeo ya awali ya uchambuzi huo yanaonyesha kuwa kuna haja ya kutunga sheria mpya au kurekebisha sheria zilizopo. Aidha mfumo unaopendekezwa kuanzishwa unalenga kushirikisha sekta binafsi ili iweze kutoa mchango mkubwa katika ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini bado nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza ni kwamba katika majibu yake ya msingi ameeleza kuwa kwanini Benki ilifungwa ikiwa ni pamoja na matatizo ya kifedha, matatizo ya kiutendaji na kushindwa pia kupeleka mikopo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo. Swali langu ni kwamba, kwa kuwa Serikali ya awamu ya nne imeonyeshwa kuwa makini sana katika utendaji wake na tukifuata msemo wa Rais wetu ambao ndiyo unapalekea kufanya kazi katika awamu ya nne, Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuifufua rasmi Benki hii kwa sababu ilikuwa ni muhimu sana kwa wananchi na hawa wananchi wenye uwezo wa chini na ukizingatia asilimia 70 ya makazi ya Dar es Salaam yamejengwa kiholela na hii ni kwa sababu ya uwezo mdogo waliokuwa nao wananchi?

Swali la pili, kwa kuwa hali ya sasa inaambatana na ushindani wa soko huria. Je, Wizara inaweza ikatueleza mbali ya *THB* kufungwa ni taasisi gani nyingine binafsi za kifedha ambazo zinatoa mikopo ya riba nafuu, kwa wananchi ili waweze kwenda kukopoa na kujenga nyumba za waishi katika makazi mazuri na bora hasa watumishi wa Umma? Naomba majibu tafadhali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba hakuna mpango wa kufufua au kianzisha Benki ya Nyumba Tanzania kwa sababu haipo, ilifutwa tangu mwaka 1995. Lakini katika mikakati ya Serikali ya awamu wa nne katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mikopo ya nyumba kuna taratibu nyingi ambazo zimekuwa zikifanywa. Hadi sasa hivi tumeshaandaa waraka ambao utawezesha kuzihusisha sekta binafsi kwa sababu ujenzi wa nyumba hata mahali pengine duniani haujengwi na Serikali. Marekani karibu asilimia 70 ya nyumba zake zimejengwa kwa kuhusisha sekta binafsi, Public Private partinership. Kwa hiyo hicho ndicho tunachokifanya kwa kurekebisha baadhi ya sheria zetu ili kuhakikisha kwamba watu binafsi wanahusika katika suala zima la kujenga nyumba.

Lakini kwa upande wa Serikali, kwa mfano Wizara ya Ardhi hadi sasa hivi imeshatumia zaidi ya bilioni 2.8 katika kuwakopesha wafanyakazi wa Serikali katika kujenga nyumba zao. Hadi sasa hivi zaidi ya watu 779 wameshakopeshwa na interest ni asilimia 3 kwa kila mtu anakapokuwa anapata. Kwa hiyo suala zima ni kuwahusisha sekta binafsi katika kuhakikisha kwamba suala la makazi linaendelezwa na Serikali inalifanyia kazi kwa nguvu na ari mpya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa Wizara hii bado haijawasilisha Bajeti yake na kwa kuzingatia muda na bado tuna maswali sita, ninaomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 322

**Mpango wa MKURABITA**

**MHE. JUMA H. KILIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005- 2006 inaeleza kuwa katika kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya Benki na mifuko mingine inayokopesha. Aidha, Mabenki nayo yataandaliwa ipasavyo katika kubadili tabia ili yaonekane na mawazo ya ugumu wa kutoa mikopo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia hatimiliki ya ardhi wananchi wa miji midogo ya Shelui, Kinampanda, Misigiri, Ndago na sehemu zingine ambako wamepokea kwa furaha mpango wa MKURABITA?

(b) Je, ni lini Taasisi za Fedha yakiwemo mabenki, Serikali zitajitayarisha ili kutembelea Jimbo la Iramba Magharibi tayari kwa kutoa mikopo iliyo na riba nafuu kwa wananchi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kifungu cha 42 (a) Serikali inaelekezwa kutekeleza Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Mpango huu ni mkubwa na unahitaji ushirikishwaji wa wadau wengi. Serikali ilianza na imekamilisha utafiti wa kutambua matatizo dhidi ya urasimishaji wa rasilimali zisizokuwa kwenye mfumo uliorasmi wa uchumi.

Kwa sasa Serikali inafanya tathimini ya matatizo na kutayarisha mapendekezo juu ya mfumo unaofaa kwa ajili ya urasimishaji. Mara kazi hii itakapokamilika Serikali itatekeleza mapendekezo yatakayokuwa yameainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti miji midogo ya Shelui, Kinampanda, Misigiri, Ndago na mingine nchini itapatiwa hatimiliki mara baada ya upimaji, utambuzi wa maeneo yaliyojengwa bila kupimwa na ujenzi wa miundomsingi utakapokamalika. Wizara kwa kushirikiana na Halmashahuri ya Wilaya ilikwishapima baadhi ya vijiji katika Kata ya Shelui vikiwemo vijiji vya Kizonzo, Mgongo, Mseko, Kibigiri na Wembere.

Vijiji vingine vitapimwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Iramba inalo jukumu la kutenga fedha kwenye bajeti yao kwa ajili ya upimaji wa miji midogo na vijiji katika maeneo yao. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Fedha mara zote ziko tayari kutoa mikopo kwa wananchi wenye kukidhi masharti yaliyowekwa. Nawashauri wananchi wa Iramba na sehemu zingine nchini wenye hatimiliki na leseni za makazi wawasiliane na taasisi za fedha na watume maombi ya mikopo. Aidha kwa mujibu wa sera ya mikopo midogo midogo *(Micro-Finance Policy)* ya mwaka 2000 inahimiza wananchi kujiunga katika vikundi vidogo vidogo vya *SACCOS* na *SACCAS* ili waweze kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo mikopo ilivyo nafuu, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba inashauriwa kuwahamasisha wananchi wake.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri na amezungumzia suala la Mkurabita kwa upana wake na hali ya Mkurabita kama ilivyoelezewa ni kweli njia pekee inayoweza kumwezesha mwananchi hasa wa hali ya chini walioko vijijini na ikamkomboa katika lindi la umaskini. Sasa kwa kuwa wananchi wanayo ardhi na Mkurabita ndiyo unasema kwamba upo tayari kuralimisha vitu vya namna hiyo. Je, Wizara iko tayari kutoa vibali kwa wananchi walipo vijijini. Hivi vibali vikatumika kama dhamana ya mikopo wakati utaratibu mzima ukisubiri hati miliki?

Pili, kwa kuwa ameongelea vijiji alivyovijta katika miji hasa kwenye Kata ya Shelui kule tayaru vile vijiji vilivyopimwa wananchi wanalazimishwa watoe shilingi 32,000/- kwa ajili ya upimaji wa viwanja. Lakini hali ya wananchi hao ni ya chini sana. Je, kwa kuwa wananchi wamekuwepo pale kwa muda mrefu Serikali inatoa tamko gani juu ya kuwapa msamaha wa ulipaji wa fedha kwa kuwa wamekuwa wakilinda ardhi katika kipindi chote ili waweze kuendelea kwa sababu hiyo ardhi walikuwa nayo tangu awali?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkubarata unatokana na ushauri na taalam, mwekezaji wa masuala duniani Henardo Desanto kutoka Peru ambaye anashiriki kikamili kwa kushirikiana na Serikali hii kuhakikisha kwamba raslimali za wanyonge zinazingatiwa katika kujenga uchumi. Mheshimiwa Mbunge amesema kutoa vibali kwa dhamana ya mikopo, kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 1999 na sheria namba 5 ya mwaka 1999, Wizara ya ardhi inawajibu wa kutoa hati kwa vijiji au eneo lolote lililopimwa kwa mujibu wa sheria hizo na si kutoa vibali kwa dhamana ya mikopo. Kwa hiyo, ninapenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji vile na maeneo yote yanayohusika kupimwa ni vizuri kwanza yakapimwa ili sheria ya nchi namba 4 na 5 ya mwaka 1999 ikazingatiwa katika kutoa hati ambazo zitawawezesha wananchi wananchi hawa kupata mkopo uliohalali.

Katika sehemu yake ya (b) anasema wananchi wanalazimishwa kutoa shilingi 32,000/- kwa ajili ya upimaji wa ardhi. Ardhi kwa sasa hivi ina thamani na kwa vile ardhi

inathamani inawajibu thamani hiyo ikazingatiwa kikamilifu. Hata hivyo napenda kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Ardhi katika fedha ambazo huwa zinakusanywa kutokana na *land rent* katika Halmashauri za Wilaya, asilimia 20 huwa zinabakizwa katika Halmashauri hizo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri husika watumie hizo asilimia 20 zinazobaki kwa ajili ya mapato yanayobaki huko kwao kwa ajili ya matumizi yao ikiwemo na kupunguza gharama kwa wananchi katika upimaji wa ardhi zao. *(Makofi)*

Na. 323

**Usugu wa Dawa za Kutibu Malaria**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa usugu wa dawa za Malaria umekuwa kero kwa wananchi hata kupelekea dawa za Malaria kubadilishwa mara kwa mara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kutatua tatizo la usugu wa dawa za kutibu Malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliweka utaratibu wa kufuatilia uwezo wa dawa za kutibu ugonjwa wa Malaria hapa nchini tokea mwaka 1999. ufuataliaji huu umekuwa ukifanyika kila mwaka katika vituo vinane vilivyopo Mlandizi–Kibaha, Ujiji–Kigoma, Chamwino – Dodoma, Butimba –Mwanza, Nagaga –Masasi, Mlimba – Kilombero, Ipinda –Kyela na Mkuzi –Muheza. Vituo hivi vinawakilisha maeneo tofauti ya uambukizaji wa Malaria hapa nchini. Nia ya utafiti huu ni kuhakikisha kuwa dawa zinazotumika kutibu Malaria zina uwezo wa kutibu au hapana.
Hii hutuwezesha kujua mapema ni kiasi gani dawa husika imeshindwa kutibu na inapobidi maamuzi ya kubadili sera za matibabu hufanyika. Utaratibu huu ndio umekuwa ukifuatwa na Wizara yangu katika kutoa maamuzi ya kubadili dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kuhusu dawa za tiba ya malaria ni kwamba endapo dawa itashindwa kuponya kwa asilimia 24 ya wagonjwa waliothibitika kuwa na malaria au iwapo asilimia 15 ya vimelea vya Malaria ni sugu dhidi ya dawa husika basi ni lazima ibadlishwe. Kwa mantiki hiyo, mwaka 2001 dawa ya *chlroquine* ambayo kwa miaka mingi ilikuwa dawa ya safu ya kwanza ya kutibu Malaria, usugu wake ulithibitika kufikia asilimia 60. Kufuatia hali hii Serikali iliamua dawa ya *Chlroquine* isitumike na badala yake dawa ya *Sulfadoxine/Pyrimethamine* (*SP*) ilichukua nafasi yake kwa vile wastani wa kushindwa kuponya wagonjwa kwa dawa hii

wakati huo ilikuwa asilimia 10 tu. Aidha ilikubalika kuwa dawa ya *SP* iliyopendekezwa itakuwa ni ya mpito wakati nchi ikijiandaa kupata dawa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na kuongezeka kwa usugu wa vimelea vya ugonjwa wa malaria, Tanzania pamoja na nchi zingine duniani zimo katika harakati za kubadilisha Sera za matibabu ya malaria. Makubaliano yaliyopo kuhusu dawa za safu ya kwanza kutibu Malaria ni kutumia dawa mseto zenye *Artemisin* zilizochanganywa na dawa nyingine ambazo pia zina nguvu ya kutibu Malaria.

Matumizi ya dawa mseto yameonyesha kupunguza ugonjwa kujirudia rudia pia kupunguza uwezekano wa vimelea kujijengea usugu. Kufuatia tafiti zilizofanyika hapa na nchi kuhusu dawa mbadala ya *SP*, dawa ya *Artemether/Lumefantrine (ALu)* ndiyo dawa mseto iliyopitshwa kutumika kama dawa ya safu ya kwanza ya kutibu Malaria isiyo kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu hivi sasa iko katika maandalizi ya kuanza kutumia dawa hiyo mpya kuanzia mwezi Novemba 2006. Kwa kuchagua dawa hiyo kutibu malaria isiyo kali na malaria kali, Wizara yangu ina matumaini kwamba tatizo la usugu wa vimelea vya Malaria dhidi ya dawa hii halitakuwa kero tena kwa kipindi kirefu kijacho.

Napenda kutoa rai kwa Watanzania wenzangu kuwawahisha watoto na wao wenyewe kupita matibabu ya malaria kila wakihisi dalili za malaria na kutumia dawa kwa kiasi chote walichoandikiwa kwa muda ulioainisha. Matumizi ya dawa kwa muda mfupi au kiasi cha dawa ni njia mojawapo ya kukaribisha usugu wa vimelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba dawa zimekuwa zikibadilishwa mara kwa mara na sasa hivi wanatumia hii dawa ya *Artemisin,* katika utafiti hii dawa imefanyiwa utafiti kama akinamama wenye ujauzito wa chini ya miezi mitatu na watoto wa chini ya miaka mitano wanaweza kutumia dawa hizi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakinamama wenye ujauzito wa chini ya miezi mitatu kwenda chini dawa hii wanaweza kuitumia lakini ningependa kushauri kwamba mtu yoyote yule anapokuwa na tatizo la malaria anapaswa kabla hajatumia dawa awe mjamzito au asiwe mjamzito ni lazima afuate ushauri wa Daktari. *(Makofi)*

Na. 324

**Wanafunzi wa Fani ya Uhasibu - Chuo Kikuu Mzumbe**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa fani ya uhasibu katika Chuo Kikuu, Mzumbe wamefunga chuo kwa muda mrefu. Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanasoma katika muda wa kawaida kama ilivyo kwa wanafunzi wengine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa kawaida kalenda ya masomo ya Chuo Kikuu Mzumbe ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Oktoba | - | Januari (Semista ya kwanza) |
| Februari | - | Likizo fupi |
| Machi | - | Juni (Semista ya pili) |
| Julai | - | Septemba (likizo ndefu) |

Wakati huo huo Semista ya kwanza (Oktoba – Januari) wanafunzi wa mwaka wa tatu huenda kwenye mafunzo ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kabwe Zitto kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa fani ya Uhasibu katika Chuo Kikuu cha Mzumbe walikaa nyumbani kutokana na utaratibu unaoitwa kusepetua semista au *(semister staggering)* kwa kingereza.Naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu mfumo wa kusepetua. Mfumo wa kusepetua semista huwawazesha wanafunzi kupishana chuoni yaani wakati kundi moja linasoma kundi jingine linakuwa nje ya chuo ama kwa likizo za mafunzo ya vitendo. Chuo Kikuu Mzumbe kilianzisha mfumo wa kusepetua mwaka 2004/2005. Mfumo huu unahusu semista ya pili ya mwaka wa kwanza kwa baadhi ya programu za Shahada ya Kwanza. Katika mwaka wa masomo 2004/2005 wanachuo wa mwaka wa Kwanza wa Shahada ya Sheria ndio waliohusika na mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2005/2006 wanachuo wa mwaka wa kwanza waliohusika ni wa Shahada ya Uhasibu na Fedha na Shahada ya Utawala zenye jumla ya wanafunzi 740. Wananchuo hao walisoma Semista ya Kwanza kama kawaida pamoja na wananchuo wenzao wa Shahada nyingine yaani Octoba 2005 hadi Januari 2006 kisha wakaenda likizo wakati wanzao wanaendelea na semista ya pili ya kawaida iliyoanza mwezi Machi na kumalizika mwezi Juni, 2006. *(Makofi)*

Wanafunzi hawa walio Sepetua Semista wa Shahada ya Uhasibu na Fedha na Shahada ya Utawala, wamerudi Chuoni tayari mwezi Juni na wanaendelea na masomo hadi mwisho wa Mwezi Septemba 2006, wakati wengine ndio wanaenda likizo ya muda mrefu na wanafunzi wote wanatarajiwa kuendelea na masomo ya mwaka wa pili kama kawaida ifikapo Oktoba 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, wanachuo hao wa fani ya Uhasibu pamoja na fani nyingine ambao wapo kwenye Mfumo wa Kusepetua Semista, wanasoma kwa kiwango kile kile kama wanachuo wengine na Uongozi wa Chuo unazingatia viwango vya Ubora wa Elimu vinavyowekwa na kusimamiwa na *Commission* ya Vyuo Vikuu Tanzania. Kilichobadilika ni likizo yao na pia ni lini wanafunzi wanasoma Semista ya pili ya mwaka wa kwanza wa masomo. *(Makofi)*

Na. 325

**Kuanzisha Chuo Kikuu Mtwara**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa mikoa ya Kusini mwa Tanzania yaani Mtwara na Lindi inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wenye sifa na uwezo hasa wa Elimu ya Chuo Kikuu:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha Chuo Kikuu katika Mkoa wa Mtwara?

(b) Kama Serikali haina mpango kama huo. Je, haioni kuwa inafanya upendeleo wa wazi kwa baadhi ya mikoa kuwa na zaidi ya Chuo Kikuu kimoja wakati mikoa ya Kusini ikiacha bila chuo hata kimoja?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu vimeanzisha matawi katika mikoa mbali mbali ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu Mzumbe ambacho kina matawi Mbeya, Dar es salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina vituo mikoa yote ya Tanzania, pamoja na Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuongeza Vyuo Vikuu nchini kwa kujenga Chuo Kikuu kipya katika Mkoa wa Dodoma ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi kati ya 20,000 na 40,000 wakiwemo wa Mikoa hiyo ya Kusini. Hata hivyo, Kutokana na kwamba Vyuo vya Elimu ya Juu ni vya kitaifa na kwa hiyo hudahili wanafunzi kutoka sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa wa Tanzania na kutoka nje ya nchi.

Aidha, endapo Chuo Kikuu kitajengwa Mtwara vile vile kitadahili wanafunzi kutoka mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina upendeleo katika suala la Elimu kwa wananchi wake. Lakini, ikumbukwe kwamba uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo na ujenzi wa Chuo Kikuu ni gharama kubwa sana, hivyo ni vigumu kujenga Chuo Kikuu katika kila Mkoa wakati mmoja. Hata hivyo, kwa kadri uwezo wa kifedha utakavyokuwa ukiongezeka, Serikali itaendelea kujenga Vyuo Vikuu katika Mikoa mingine ambayo haijapata fursa hii. Aidha wawekezaji wengine katika Elimu ya Juu watashauriwa kuwekeza katika Mikoa mingine na hususan Mikoa ya pembezoni na isiyokuwa na Vyuo Vikuu vya kutosha.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri ka majibu yake mazuri na niipongeze Serikali kwa kuanzisha Chuo Kikuu hapa Dodoma. Swali langu ni kwamba; Je, mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki katika Mkoa wa Mtwara, umefikia hatua gani na kitakuwa tayari lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nimpongeze Mheshimiwa Mariam R. Kasembe kwa kufuatilia masuala ya elimu katika Mkoa wake na hususan elimu kwa watoto wa kike.

Pili, naomba nimweleze kuhusiana na hicho Chuo cha Mtwara. Chuo cha Mtwara, nilijibu swali hili wakati nahitimisha hotuba yetu ya bajeti taerehe 21. Nilieleza kwamba hiki Chuo kwanza sio Chuo Kishiriki. Naomba niweke hili sawa. Vyuo Vishiriki ambavyo vilikuwa Vyuo vya Ualimu ni Chuo Cha Ualimu Dar es salaam kilichojulikana kama Chang'ombe pamoja na Sekondari ya Mkwawa.

Hivi viliwekwa Vyuo Vishiriki kwa maana kwamba Uongozi pamoja na Umiliki, umeenda katika Elimu ya Juu chini ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam ili kusaidia Idara ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam kuongeza idadi ya Walimu wa Shahada wanaohitajika sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ualimu Mtwara, chenyewe kilianzishwa kama Chuo Kiambata, *Affiliated College*. Maana yake ni kwamba, kile Chuo kitaendelea kuwa chini ya Uongozi na Utawala. *Governance* yote itabaki chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wizara ya Elimu ya Juu itashughulikia masuala ya programu, *quality assurance* na kuhakikisha kwamba wanataaluma au walimu wanaoteuliwa kwenda pale, wana sifa za kutosha, lakini kitaendelea kuwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema, upembuzi yakinifu ulishafanyika kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Maafisa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Bado tunachosubiri, kwa kuwa bado kiko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 ambayo ilirekebishwa 1995.

Lakini, bado haijaruhusu Chuo cha Ualimu Mtwara kuingiliwa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa ajili ya kukipandisha hadhi na kukifanya *Affiliated College*. Mchakato huo unaendelea na Wizara yangu inaendelea kufuatilia kwa karibu kwa sababu tunashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na mchakato utakapokuwa umefika mwisho, Chuo kile kitakuwa *Affiliated College* na kitatoa Kozi ya *Diploma* ya Ualimu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba ndugu zangu wa Mtwara, tuwe na subira hadi hiyo hatua itakapofikiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Swali Namba 326 kulingana na muda wetu, naomba Mheshimiwa Siraju Kaboyonga aniridhie swali hilo liingizwe kwenye ratiba ya kesho ili tuendane na ratiba yetu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatoa matangazo ya vikao na mambo mengine mbali mbali, ninaomba Waheshimiwa Wabunge katika *Order Paper* yetu ya leo, zile hoja za Serikali katika ule ukurasa wa mwisho wa tisa, pale Mtoa Hoja, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, imekosewa na ilitakiwa iwe Mtoa hoja wa leo ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninaamini kila mtu amepata karatasi ya marekebisho. Kwa hiyo, ninaomba mchukue hiyo kama marekebisho ya *Order Paper* yetu ya Leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile naomba niwakumbushe, niendelee kuwakumbusha katika utaratibu wa kupitisha Bajeti zetu kwa vifungu. Naomba tuendelee kuzingatia mwongozo wa Kanuni zetu wa kuhakikisha kwamba kila Mbunge anafuata Kifungu kinachohusika na sio wote kukamata ule Mshahara wa Waziri tu peke yake. Vile vifungu vitawanywe kulingana na utaratibu wa *vote* mbali mbali. Lakini tangazo hilo linaendana labda mimi niwape tangazo jingine moja.

Leo asubuhi nimepokea *message* nyingi sana kutoka kwa watu na watoto mbali mbali, wananiuliza, kwa kuwa tumekuwa na changamoto kubwa sana ya kukamata mishahara ya Mawaziri ili tuweze kupata mahitaji mbali mbali katika maeneo yetu, lakini watoto wanatuuliza, hivi kuna utaratibu gani wa kukamata mishahara ya wazazi ili wapate mahitaji yao ya kwenda shuleni? *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo ni changamoto ya leo na kwa kuwa tuna Wizara hiyo ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nafikiri itabidi tuwe na utaratibu wa kujua watoto nao wakikosa mahitaji yao, wanakamataje mishahara ya wazazi ili waweze kuipata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya vikao niliyonayo ni kama ifuatavyo:- Kutakuwa na kikao cha Kamati ya Miundombinu na Mheshimiwa Mwenyekiti Mohamed H. Missanga wa Kamati hiyo, ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa leo tarehe 1 Agosti, 2006 kutakuwa na kikao kitakachofanyika kuanzia saa 7.00 mchana, Ukumbi wa Zamani wa Bunge.

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, ananiomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo ya Uwekezaji na Biashara leo tarehe moja kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Zamani. Nafikiri kamati hizi zitafanya kikao kwa pamoja.

Nina tangazo la kikao kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Anaomba kuwatangazia wajumbe Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe moja saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Zamani. Nafikiri kamati hizi zote zitakuwa huko pamoja.

Ninaomba niwatangazie kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, anao wageni wake na wamekaa pale mbele kwenye *Speaker's Galery*. Anao watoto wake wawili, Mmoja anaitwa Linford Cliff amekuja kutoaka California. Anaye mtoto wake mwingine, Mwijuma Abdulaziz na ana mdogo wake anaitwa Hawa Idd. Kwa hiyo, hawa wote wamekuja kwa niaba ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Godfrey W. Zambi ameomba nitangaze kwamba, anaye Katibu wake wa Jimbo anaitwa Mr. Msukwa, yuko hapa ndani pamoja nasi leo. *(Makofi)*

Ninaomba nitangaze kwamba katika Ukumbi wa *Public Galery*, leo tuna wageni pia wa Mheshimiwa Spika wetu. Naomba niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa Spika, kuna Diwani Mheshimiwa Stephen Chambala na Mheshimiwa Diwani Charles Msyolo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje anasema ana viongozi 17 wa CCM na Serikali kutoka Kata za Jimboni kwake Chilonwa. Naomba hawa wageni wake pia tuwatambulishe. *(Makofi)*

Tuna wageni pia wa Mheshimiwa Kaika S. Telele, Daniel Ole Mbilika, Olidibelo Mwana, Sandiha Makiro, Nakerai Limbai na Alalami Ngarai. Ahsanteni sana. Tunawashukuru kwa ujio wenu na haya majina kwa kweli hata Mwenyekiti yamenipa shida kidogo kuyatamka. *(Makofi)*

Naomba nitangaze kwamba, kuna kikundi cha akina mama kutoka Kyela wakiongozwa na Mama Neema, wamekuja kusikiliza Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hao ni wageni wa Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe. Karibuni sana akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Devota Likokola, anasema ana viongozi 30 wa Vikoba wakiongozwa na Ndugu Filbert Lwambano akiwa na Florah Mwaisaka wa Dodoma, Neema Mwakalinga na Goerge Mhilu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni wengine leo, wanafunzi 100 kutoka shule ya Sekondari ya Msalato. Naomba wasimame wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Kwa umuhimu wa hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nimepewa taarifa tena hapa sasa hivi kwamba, tunao Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka Dodoma Vijijini na Dodoma Mjini, nao wako pamoja nasi hapa leo. Karibuni sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007**
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata wa kuweza kupata dhamana ya kuliongoza Taifa hili kama Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne.

Aidha napenda pia kumpongeza kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu Maalum wa CCM kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, pia natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa John S. Malecela Mbunge, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Mheshimiwa Abeid Amani Karume, Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Mheshimiwa Luteni Mstaafu Yusuf R. Makamba Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na pia kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu mpya wa CCM.

Aidha napenda kuchukuwa fursa hii kuwapongeza wajumbe wa Sekretariati ya Hamashauri Kuu ambao ni Mheshimiwa Jaka Mwambi, Naibu Katibu Mkuu (Bara), Mheshimiwa Rostam A. Azizi, Mbunge, Mweka Hazina, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mbunge, Katibu wa Itikati na Uenezi, Mheshimiwa Dokta Asha-Rose M. Migiro, Mbunge, ambaye ni Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge, ambaye ni Katibu wa Oganaizesheni.

Napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwake tena kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na hatimaye kupitishwa na Bunge lako tukufu kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na uhodari na uchapakazi wake ambao sisi sote tunaufahamu, ni wazi kwamba watanzania wote tunayo matumaini makubwa na uongozi wake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Spika, wa Bunge Mheshimiwa Samwel John Sitta, Mbunge wa Urambo Mashariki kwa kuchaguliwa kushika nafasi hii yenye wajibu mkubwa wa kuliongoza Bunge letu tukufu. Hii ni nafasi inayohitaji hekima, umakini, busara na utulivu mkubwa.

Aidha, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Anna Semamba Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika. Ni matumaini yangu kwamba uzoefu wake wa muda mrefu utalinufaisha Bunge hili na kwamba atakuwa msaada mkubwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Pia nakupongeza Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Paramiho na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii, kuipongeza Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge, kwa kuchaguliwa kwao kuiongoza Kamati hii na pia kwa kuweza kuichambua na kuijadili Bajeti ya Wizara yangu kwa kina. Maelekezo na ushauri uliotolewa na Kamati hiyo umeweza kuboresha bajeti ninayoiwasilisha hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Mbunge na hatimaye kuniteua kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninaahidi kupitia Bunge lako tukufu na kwa watanzania wote kuwa nitayatekeleza majukumu yangu kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Naomba Mwenyezi Mungu, anipe uwezo na ujasiri ili niweze kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji, Mbunge, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao ambazo zimetupa mwelekeo mzuri wa hali ya uchumi na bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2006/2007. Mwelekeo huo umezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Majukumu ya Wizara Kwa Mwaka 2005/2006: Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2005) imeweka bayana kuwa rasilimali watu ndiyo nyenzo kuu katika jitihada za taifa za kujenga uchumi wa kisasa na kupata maisha bora kwa kila Mtanzania. Aidha, Ilani inatambua kuwa watu waliojikita katika mitazamo ya kijadi hawawezi kutegemewa katika kukabiliana na changamoto za kujenga uchumi wa kisasa. Kwa kutambua hilo, Ilani inaelekeza Serikali ya CCM ya awamu hii kutekeleza kama jukumu la msingi ushirikishwaji wa wananchi wote katika ujenzi wa uchumi wa kisasa na kutokomeza umaskini kwa njia ya uwezeshaji. Sehemu kubwa ya uwezeshaji huo ikiwa ni ya mabadiliko ya fikra na kupata elimu, maarifa, ujuzi na stadi ambazo zitawawezesha wananchi kujiamini, kujiajiri na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina historia ya kujivunia ya ushirikishwaji wa nguvu za Serikali na za watu katika kuleta maisha bora kwa wananchi wake. Historia hiyo imechangiwa sana na wataalam wa fani ya Maendeleo ya Jamii wanaojulikana kama

Mabibi na Mabwana Maendeleo. Kazi kubwa ya wataalamu hao imekuwa kuwawezesha watu kubadilisha fikra na mitazamo yao, ili waendane na matakwa ya maendeleo na uchumi wa kisasa. Baadhi ya programu na miradi iliyotekelezwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi na za Serikali kwa mafanikio makubwa ni; Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto *(CSPD)*; Afya kupitia Maji na Usafi wa Mzingira *(HESAWA)*; Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*; Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Programu Shirikishi ya Kilimo *(PADEP)*.

Serikali imeendelea kuiimarisha sekta ya maendeleo ya jamii ili iweze kutoa mchango wake muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Sera mbali mbali za kukuza uchumi na kuondoa umaskini na hivyo kuongeza kasi ya upatikanaji wa maisha bora kwa kila Mtanzania. Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu imetekeleza kazi zifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa Maendeleo ya Jamii ndiyo waraghbishi wakuu na chachu ya kuwezesha watu kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli zao za kujiletea maendeleo. Kazi za wataalam hawa ni mtambuka na zinahitajika sana hasa katika ngazi za Wilaya, Kata na Kijiji. Wataalamu hawa kwa kutumia mbinu shirikishi wanafanya kazi nzuri ya kuhamasisha wananchi kushiriki katika miradi mbali mbali ya maendeleo. Hata hivyo wataalamu hawa ni wachache ukilinganisha na mahitaji halisi.

Hivi sasa ni asilimia 40 tu ya kata zote nchini ndizo zenye wataalam hawa. Kwa kuzingatia umuhimu wao, na uchache wa wataalam hao Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2005/2006 imeendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru na mafunzo ya Cheti katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Missungwi na Rungemba. Jumla ya wanafunzi 692 wakiwemo wanawake 362 na wanaume 330 walisajiliwa katika kozi za ngazi za Stashahada ya Juu. Wanafunzi 248 wakiwemo wanaume 97 na wanawake 151 walisajiliwa kwenye kozi za ngazi ya cheti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira mazuri ya kusomea yana nafasi kubwa katika kumwezesha mwanafunzi kusoma na kuyaelewa vizuri masomo yake. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kuunda Bodi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo cha Tengeru, Bodi hii ilizinduliwa rasmi kuanza kazi tarehe 8 Disemba, 2005;

- Kuandaa mitaala ya Shahada ya Kwanza kwa kozi zinazofundishwa Chuoni Tengeru badala ya Stashahada ya Juu; na

- Kukipatia Chuo gari aina ya *Toyota Landcruiser Hard Top*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Missungwi, Buhare na Rungemba, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kufanya maboresho kwa mzunguko. Katika mwaka 2005/2006, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Missungwi kimefanyiwa ukarabati mkubwa wa majengo yote, kimepatiwa gari jipya aina

ya *Toyota Landcruiser* na vifaa mbalimbali vya ufundi. Aidha, Chuo cha Rungemba kimechimbiwa kisima kirefu cha maji na kimewekewa umeme unaotokana na nguvu za jua na Chuo cha Buhare kimefanyiwa ukarabati mdogo. Vyuo vyote vitatu vimenunuliwa Kompyuta na Luninga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2005/2006, ilitoa mafunzo kwa wataalamu wa Maendeleo ya jamii wa Halmashauri ili waweze kuandaa mipango shirikishi Jamii kwa ufanisi zaidi katika ngazi ya Kata. Jumla ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii (Ufundi) 37 kutoka Halmashauri 18 za Bariadi, Bukombe, Dodoma Manispaa, Igunga, Iramba, Kahama, Kishapu, Maswa, Manyoni, Meatu, Nzega, Shinyanga Manispaa, Shinyanga Vijijini, Sikonge, Singida Manispaa, Singida Vijijini, Tabora Manispaa na Uyui walipatiwa mafunzo hayo. Aidha wataalam hao walipewa mafunzo ya kiufundi na pia namna ya kupambana na janga la UKIMWI katika jamii na sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa wataalam wengi wa maendeleo ya jamii wanaofanya kazi chini ya Halmashauri hawana vyombo vya usafiri vya kuwawezesha kuwafikia watu ili kuwahamasisha na kuwaelimisha jinsi ya kubuni, kuandaa na kutekeleza mipango yao ya maendeleo, Wizara imenunua na kusambaza pikipiki kumi (10) katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na halmashauri za wilaya za Rombo, Handeni, Muheza na Rufiji. Nyingine ni Halmashauri za Wilaya za Iringa, Songea, Singida, Shinyanga na Tabora. Ni matumaini ya Wizara kuwa Halmashauri hizo zitasaidia katika uendeshaji na matengenezo ya pikipiki hizo pamoja na kuwawezesha wataalamu hawa kwa kuwapatia nyenzo muhimu za utendaji wa shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuendeleza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira, katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu ilishirikiana na mikoa ya Mbeya na Iringa katika kuongeza uwezo wa wananchi wa kuhifadhi mto Ruaha ambao ni muhimu kwa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa umeme. Wizara yangu kupitia Vyuo vyake vilivyoko katika bonde la mto Ruaha, ilifanya kazi ya kuhifadhi mazingira kwa kupanda jumla ya miche 7,876 kama ifuatavyo:- Chuo cha Maendeleo Wananchi Uyole 120, Ruaha 2,500, Ilula 4,500, Ulembwe 56, na Rungemba 700. Aidha, Chuo cha Njombe kimeandaa miche 2,000 na Ulembwe miche 7,500 kwa ajili ya msimu ujao wa mvua. Kazi hiyo iliwapa nafasi pia wananchi wanaosoma katika Vyuo hivyo kupata elimu ya mazingira watakayoieneza katika vijiji vyao. Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na mkoa wa Iringa, imeweza kutoa mafunzo juu ya mazingira na kuandaa mipango ya mazingira na uhifadhi wa maji kwa Kamati za Maji na Mazingira katika maeneo yanayozunguka Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendesha warsha kwa wazee kutoka Wilaya za Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani kwa madhumuni ya kupata uzoefu, hekima na busara zao kuhusu matumizi ya teknolojia asilia, athari za UKIMWI katika jamii na wajibu wao katika jamii kuhusu kulinda na kuendeleza mila, desturi na

maadili ya taifa letu. Aidha, wazee hao walielimishwa kuhusu umuhimu wa kutumia teknolojia sahihi ambazo zitawawezesha kutumia nguvu kazi yao kadri umri wao unavyoongezeka katika shughuli zao mbali mbali za maendeleo,

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005/2006, Wizara yangu pia iliahidi kufuatilia hali ya Majumba ya Maendeleo *(Community Centres)*, kwa madhumuni ya kuyafufua na kuyapatia vifaa na nyenzo muhimu zitakazowezesha wananchi kupata na kupashana habari za maendeleo. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa ufuatiliaji huo umefanyika katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Rukwa, Singida, Shinyanga, Tanga na Tabora. Ufuatiliaji huo umeonyesha kwamba:-

(i) Halmashauri nyingi ziliwapangisha wafanya biashara majengo hayo, hivyo kubadilisha kabisa matumizi yake yaliyokusudiwa;

(ii) Mwamko wa wananchi wa kupashana habari zinazohusu maendeleo umezorota kwa kukosa sehemu ya kukutana;

(iii) Baadhi ya majumba hayo yanatumika kama ofisi za Idara za Halmashauri;

(iv) Majumba mengi hayana nyenzo na ni machakavu, na yanahitaji ukarabati mkubwa ili kutoa huduma zilizo kusudiwa katika hali ya usalama; na

(v) Majumba yote yako sehemu za mijini.

Kutokana na matokeo ya ufuatiliaji huo, Wizara yangu kwa kuanzia imenunua seti *(TV, Dish & VCR)* kumi na moja (11) ambazo zimewekwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuhakikisha wananchi wanaoishi jirani na vyuo hivi wanapata habari mbalimbali.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2005) inatoa kipaumbele katika elimu ya ufundi na elimu ya watu wazima kama nyenzo muhimu ya kuimarisha jitihada za taifa za kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Wizara yangu inasimamia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58 ambavyo vimeanzishwa kwa madhumuni ya kuendeleza elimu ya watu wazima kwa kutoa maarifa, ujuzi na stadi mbali mbali za kazi ambazo zitawawezesha wananchi wanaovitumia kujiamini na kutekeleza majukumu yao ya kukuza uchumi na kujiletea maisha bora kwa kasi na ufanisi zadi. Vyuo hivi hutoa mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi na kulinganana na mahitaji ya wananchi wanaovitumia. Elimu itolewayo kwenye Vyuo hivi inatoa fursa mbali mbali za kuboresha uzalishaji, kujiajiri na hivyo kujiongezea vipato, kupunguza ukosefu wa ajira na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo ya maarifa na stadi kwa makundi mbali mbali ya jamii kwa kutumia Vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya wananchi 25,486 wamepatiwa mafunzo hayo wakiwemo wanawake 11,637 na wanaume 13,849. Mafunzo hayo yanalenga katika

kuwawezesha wananchi kuelimika na kushiriki katika harakati za kukuza uchumi na kutokomeza umaskini na hivyo kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanavutiwa kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara imeendeleza azma yake ya kuvikarabati vyuo hivyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Vyuo vya Ifakara, Handeni, Kilwa Masoko na Nzovwe vimepatiwa fedha za ukarabati mkubwa wa majengo ambapo Vyuo vya Musoma, Njombe, Ruaha na Tango vimepatiwa fedha za ukarabati mdogo. Wizara yangu pia imevipatia fedha Vyuo vya Arnautoglu, Bariadi, Chisalu, Kibondo, Malya, Muhukuru, Musoma, Mtawanya, Nzega, Urambo na Uyole kwa ajili ya kupima maeneo yake ili vipatiwe hati ya kumiliki ardhi. Aidha, maandalizi ya awali ya kukipatia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi umeme unaotokana na nguvu za jua *(solar energy)* yanaendelea. Vile vile ili kuimarisha usafiri katika Vyuo vyote 58 vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara imetoa fedha za kununulia baiskeli mbili (2) hadi tatu (3) kwa kila chuo kutegemea bei ya mahali Chuo kilipo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya kutoa elimu kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwa lengo la kuwawezesha kujitegemea, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu imetoa mafunzo ya stadi za kazi mbali mbali na ujasiriamali kwa wasichana waliozaa katika umri mdogo wapatao 237 katika Vyuo vya Ilula, Kiwanda, Mamtukuna, Nzovwe, Tarime, Ulembwe na Uyole. Aidha, Wizara pia imeweza kuwahudumia watoto yatima 40 kwa kuwalipia michango katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na karo katika shule za Msingi na za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo Ya Jinsia: Wizara yangu inao wajibu wa kuratibu, kufuatilia na kusimamia Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, inaelekeza uingizaji wa masuala ya jinsia katika Mipango, Mikakati na Sera mbalimbali za kisekta. Ili kufanikisha utekelezaji wa hili, Wizara yangu imeandaa na kusambaza Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia ambao ni Mwongozo wa utekelezaji wa Sera hiyo kwa wadau mbalimbali nchini. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Dawati la Jinsia kwa kutoa mafunzo ya jinsia kwa Watendaji wake katika ngazi mbalimbali. Jumla ya Watendaji 210 wa Dawati la Jinsia kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri na Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata walipewa mafunzo ya elimu ya jinsia. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao na katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango na mikakati ya sekta zao. Pia Wizara na Taasisi zimeendelea kuunda Kamati za Dawati la Jinsia ndani ya sekta zao. Kutokana na hili, sekta mbalimbali zimeweza kuandaa taarifa na takwimu zilizoainishwa kijinsia ambazo imewezesha upangaji mipango kwa kuzingatia usawa wa jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuratibu shughuli za kuwawezesha wanawake kiuchumi ili, waweze kuondokana na umaskini. Mwaka 2005/2006, Wizara ilishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zisizo za Kiserikali kuwawezesha wanawake wafanyabiashara kushiriki katika maonesho ya 30 ya Biashara

ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Jumla ya wanawake 195 walishiriki katika maonesho hayo kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kabla ya maonesho ambayo yalilenga katika kuwapatia mbinu za kuboresha bidhaa na kushiriki katika masoko yenye ushindani. Kutokana na ushiriki wao katika maonesho hayo, waliweza kuuza na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa zao. Aidha walipatiwa mafunzo ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ambao unatoa mikopo kwa wanawake kwa masharti nafuu. Utafiti wa kina umefanyika ili kubainisha mafanikio, matatizo, changamoto na mapendekezo ya kuboresha uendeshaji wa Mfuko huu. Kutokana na utafiti huo imeonekana kuna umuhimu wa kudurusu Mwongozo ambao unabainisha majukumu ya Wizara, Sekretariati za Mikoa na Halmashauri katika uendeshaji wa Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imejiwekea utaratibu wa kutoa mafunzo ya mbinu za kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Maafisa Maendeleo ya Jamii 265 kutoka ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata walipatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yalihusu Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003, uendeshaji wa *SACCOS* na mbinu za kuwahamasisha wanawake na wananchi kwa ujumla kujiunga na kuimarisha *SACCOS/SACAS* zilizopo kwenye maeneo yao.

Kutokana na mafunzo hayo ambayo yalianza kutolewa tangu mwaka 2003/2004, wanawake wamehamasika na wanajiunga na *SACCOS* hizo. Aidha, ili kuongeza kasi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu imekuwa ikiratibu mchakato wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake. Hadi sasa nyaraka muhimu zitakazowezesha Benki Kuu kuisajili Benki hii zimeishaandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa linaloikabili jamii. Tatizo hili limekuwa likidumishwa na mfumo dume uliojengeka katika baadhi ya mila na desturi za jamii zetu. Mwaka 2005/2006, Wizara ilidurusu, kuchapisha na kusambaza Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kutokomeza Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2001 – 2003. Mpango huo sasa utatekelezwa hadi 2015. Mpango huu unalenga katika kubadilisha sheria zinazowakandamiza wanawake na watoto; kutoa elimu, mafunzo na uhamasishaji kwa wananchi kuhusu kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake; kutoa huduma zinazofaa kwa wanaotendewa ukatili na kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mila na desturi zinazoendeleza ukatili.

Aidha, Washauri wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretariati za Mikoa, Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii 202, walipatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yalihusu utekelezaji wa Mpango wa Uzuiaji na Utokomezaji wa Ukatili dhidi ya Wanawake na utoaji wa ushauri nasaha kwa walioathirika na vitendo vya ukatili. Kutokana na mafunzo hayo wanawake walioathirika na ukatili wataweza kupewa msaada wa kisheria na ushauri nasaha pale wanapojitokeza katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo mojawapo ya kuleta usawa wa jinsia ni kwa wananchi kuzijua sheria, kanuni na taratibu zilizopo na kuzizingatia. Hivyo, Wizara yangu iliendesha mafunzo kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kutoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Morogoro, na Pwani kuhusu Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (1998), Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi Vijiji za 1999, elimu ya jinsia na namna ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. Vile vile Wizara ilitayarisha na kusambaza majarida na mabango katika lugha nyepesi ili kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria hizi na athari za vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika ngazi za maamuzi, Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Kutokana na marekebisho ya Katiba ya mwaka 2004, awamu ya nne imeongeza uwakilishi wa wanawake Bungeni kufikia asilimia 30.3 ikilinganishwa na asilimia 22.5 ya mwaka 2000; Mawaziri Wanawake wamefikia asilimia 20 kutoka asilimia 15, Naibu Mawaziri asilimia 32.3 kutoka asilimia 29 hadi kufikia mwezi Juni 2006. Lengo ni kufikia kiwango cha asilimia 50 katika ngazi zote za maamuzi kulingana na malengo ya Umoja wa Afrika *(AU)*, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeshiriki katika Kikao cha 50 cha Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake na vile vile katika mikutano ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Nchi za Maziwa Makuu na Jumuiya ya Madola. Matokeo ya mikutano hiyo ni makubaliano ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Azimio na Ulingo wa Beijing na Malengo ya Milenia, kuhusu maendeleo ya wanawake na jinsia. Aidha, taarifa ya Nne na Tano ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake *(CEDAW)* iliwasilishwa kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa. Taarifa hii ilieleza kwa undani utekelezaji wa nchi kuhusu maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia katika kipindi cha 1998 hadi 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliratibu Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi. Mwaka 2005, Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliagiza kuwa Maadhimisho haya yawe yanafanyika kila baada ya miaka mitano ili kutoa muda wa kutosha wa utekelezaji.

Kwa kuzingatia agizo hilo, mwaka 2006, Maadhimisho haya yalifanyika katika ngazi ya mikoa na yalitoa fursa ya kuitumia siku hii kutathmini utekelezaji wa maendeleo ya wanawake na jinsia na kuongeza ufahamu wa wananchi kuhusu usawa wa jinsia. Kaulimbiu ya mwaka 2006 ni *''Wanawake katika Maamuzi: Dumisha Usawa, Ondoa Umaskini."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuwasaidia wanawake wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojitokeza, Wizara ilifanya zoezi la kubainisha mahitaji yao katika Halmashauri tano za majaribio ambazo ni Manispaa ya Morogoro, Handeni,

Muheza, Rombo na Rufiji. Mahitaji yaliyobainishwa ni pamoja na misaada kwa ajili ya chakula, malazi na matunzo kwa watoto wao na mafunzo ya ujasiriamali.

Aidha, ilibainika kuwa endapo baadhi ya waathirika watawezeshwa kwa kupatiwa mikopo wanao uwezo wa kuendelea kufanya kazi ambayo zitawawezesha kujitegemea katika kujikimu. Baada ya zoezi hili Wizara itaanza kutoa mafunzo ya ujasiriamali, lishe na ushauri nasaha kwa wanawake wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo Ya Mtoto: Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inakusudia kuboresha hali ya maisha ya watoto wote. Wizara yangu kwa kuzingatia azma hiyo, inalo jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto. Lengo la Sera hii ni kuhakikisha watoto wanapatiwa haki ya kuishi, kulindwa, kutobaguliwa na kushiriki katika masuala yanayohusu maendeleo na ustawi wao na taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kuelimisha jamii kuhusu elimu ya idadi ya watu na maisha ya familia, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imeandaa kitini cha mafunzo ya elimu ya idadi ya watu na maisha ya familia ngazi ya Jamii. Kitini hicho kitatumika kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wananchi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kueneza elimu hiyo kwa jamii. Mafunzo yatakayotolewa yatawezesha jamii na hasa familia kuelewa mambo muhimu yanayohusu idadi ya watu na maisha ya familia hasa umuhimu wa uzazi wa mpango; uzazi salama; kupeleka watoto kliniki; kuwapa watoto lishe bora; uhifadhi wa chakula; umuhimu wa kufanya kazi kwa maendeleo ya familia; umiliki wa rasilimali na mgawanyo wa kazi kati ya wanawake na wanaume na watoto wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuratibu uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu haki na ustawi wa watoto. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa taarifa ya Awali ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, kama inavyoelekezwa na Umoja wa Afrika. Aidha Wizara yangu imeandaa taarifa ya Nyongeza ya Ripoti ya Pili ya Nchi ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa ya kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Mtoto. Vile vile, Wizara imetafsiri katika lugha ya Kiswahili Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto na Itifaki zake za nyongeza, ili kuhakikisha kuwa Mikataba hiyo inaeleweka katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto, imetayarisha mwongozo *(framework)* wa namna ya kuandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Malezi na Maendeleo ya Awali ya Watoto Wadogo kwa kubainisha maeneo muhimu yatakayoingizwa katika mkakati huo. Madhumuni ya mkakati huu ni kuwezesha na kuimarisha uratibu wa malezi na makuzi ya awali kwa watoto wachanga na watoto wadogo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhusu elimu ya malezi na maendeleo ya awali ya mtoto ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuwapatia watoto wachanga na watoto wadogo vyakula vya kulikiza kwa lengo la kueneza elimu hiyo kwa wazazi na walezi. Elimu hiyo imetolewa katika wilaya za mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Singida, Tanga, Mara na Mwanza. Aidha, mafunzo hayo yametolewa pia kwa Wakuu wa Vyuo vya Mendeleo ya Wananchi vya Buhangija, Handeni, Ilula, Karumo, Mabughai, Malya, Mamtukuna, Monduli, Musoma, Msinga, Nzovwe, Rubondo, Sengerema, Ulembwe na Kisangwa. Jumla ya Maafisa wa Maendeleo ya Jamii 86, na Wakuu wa Vyuo 15 wamepata mafunzo hayo.Wizara yangu kama Mwenyekiti wa Mtandao wa kudhibiti Ukeketaji Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji hapa nchini kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali Zisizo za Serikali. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara yangu iliandaa mkutano wa wadau wa Kutokomeza Ukeketaji kwa Wanawake na Watoto wa Kike hapa Dodoma uliofanyika Desemba, 2005. Lengo la Mkutano huu lilikuwa ni kubadilishana uzoefu na kujadili njia na mikakati ya kutokomeza ukeketaji hapa nchini. Hata hivyo utafiti unaonyesha kwamba, ukeketaji bado unaendelea na hufanyika kwa siri hasa kwa watoto na hata kwa wanawake.*(Makofi)*

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kuanzia ilifanya utafiti mdogo wa kutambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu katika maeneo yanayozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)*. katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Pwani na Tanga kwa lengo la kujua ukubwa wa tatizo, mahitaji yao na kubaini mbinu na mikakati ya kuwasaidia watoto hao. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitasaidia kutoa mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi kwa watoto walio katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha 2005/2006, mafunzo kuhusu haki za mtoto na madhara yanayotokana na utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari yalitolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya 40 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Pwani, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza, Singida, na Tanga. Mafunzo hayo yatasaidia maafisa hao kuisambaza elimu ya haki za watoto kwa jamii na hatimaye kupunguza tatizo la utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inalo jukumu la kusimamia na kuratibu maadhimisho ya kimataifa yanayohusu Siku ya Mtoto wa Afrika yanayofanyika tarehe 16 Juni ya kila mwaka na Siku ya Familia Duniani inayofanyika tarehe 15 Mei ya kila mwaka. Mwaka huu nchi yetu iliungana na wanachama wengine wa Umoja wa Afrika kuadhimisha miaka 16 ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa shughuli mbali mbali zilizoshirikisha watoto na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa siku hii. *(Makofi)*

Kaulimbiu ya mwaka huu ni; “Piga Vita Unyanyasaji na Udhalilishwaji wa Watoto”. Lengo la kaulimbiu hii ni kuhamasisha jamii ili iweze kuelewa umuhimu wa kuwajali watoto na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji. Aidha, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani yaliyofanyika tarehe 15 Mei, 2006. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa; “Dhibiti

UKIMWI, Familia iwajibike" Kauli mbiu hiyo ililenga kuhamasisha familia na jamii kwa ujumla katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI kuanzia ngazi ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yasiyo ya Kiserikali: Kufuatia mabadiliko ya muundo wa Wizara, Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali umewekwa chini ya Wizara yangu. Serikali inatambua mchango wa Mashirika haya katika kuharakisha Maendeleo ya Jamii ya Tanzania. Katika mchakato wa kuratibu Mashirika haya mambo yafuatayo yametekelezwa katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs.24/2002.* Aidha katika utendaji kazi wa Mashirika haya, Wizara imeshirikiana na Wasajili Wasaidizi wa ngazi za Wilaya (Makatibu Tawala Wilaya) na ngazi ya Mkoa (Maafisa Mipango Mkoa) ili kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli zao. Hatua hii imesaidia kutoa huduma za usajili karibu na wananchi na kurahisisha zoezi hili katika maeneo husika. Pia, Wizara yangu imedurusu nakala za fomu zinazotumika katika usajili, Sheria ya *NGOs* Na. 24/2002, na kanuni za utekelezaji ambazo zimesambazwa kwa wadau nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Sheria. Na. 24/2002 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeunda vyombo viwili muhimu vya kitaifa ambavyo ni Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(National NGOs Coordination Board)* na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(National Council of NGOs)*. Wizara yangu imeviwezesha vyombo hivi kukutana mara kwa mara na kuweka mikakati ya kuendeleza sekta hii. Bodi hii imekutana mara nne kati ya mwezi Juni, 2005 na April, 2006 ambapo pamoja na mambo mengine, maombi 704 ya usajili wa Mashirika haya na cheti cha ukubalifu yamehakikiwa na kupitishwa. Kati ya Mashirika haya, Mashirika 100 ni ya kiwilaya, 78 ya kimkoa, 477 ya Kitaifa na 49 ya Kimataifa. Idadi hii ni kutokana na usajili na cheti cha ukubalifu chini ya Sheria Na. 24/2002, kati ya mwezi Februari, 2005 na Machi, 2006. Aidha napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(National Council of NGOs)* liko katika hatua za mwisho za mchakato wa kukamilisha kanuni za maadili zitakazokuwa mwongozo kwa Mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inaweka bayana tatizo la uwazi, uwajibikaji na ukosefu wa takwimu sahihi za kisekta za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Wizara yangu imeanza kuandaa benki ya takwimu za Mashirika haya itakayowezesha ubadilishanaji wa habari na kuongeza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa wadau. Zoezi la kuchambua taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwetu kupitia maombi ya usajili na cheti cha ukubalifu linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na changomoto katika kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kiasi cha kuwafanya wadau kushindwa kuelewa kuwa wanatakiwa kuwajibika chini ya Sheria gani. *(Makofi)*

Hii ni kutokana na Sheria nyingine kama vile Sheria ya Makampuni Sura ya 212, kama ilivyorekebishwa hivi karibuni, Sheria ya Vyama Sura ya 337 na Sheria ya

Wadhamini Sura ya 375 kuendelea kusajili Mashirika haya. Suala hili litafuatiliwa kwa karibu sana na Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili ufumbuzi wa haraka upatatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Mipango: Kati ya majukumu ya Wizara ni kudurusu Sera za Wizara; kuoanisha Sera nyingine na Sera za Wizara, kuandaa, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara. Ili kufanikisha majukumu haya, Wizara imetekeleza yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilianza mchakato wa kudurusu Sera ya Maendeleo ya Jamii ili iweze kukidhi mahitaji ya jamii kwa wakati huu. Sera iliyopo ina upungufu uliosababishwa zaidi na mabadiliko yaliyotokea nchini na ulimwenguni kwa ujumla katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na sayansi na teknolojia. Mabadiliko mengine ni kuwepo kwa utandawazi na ongezeko la kutegemea sekta binafsi kama muhimili mkuu wa kukuza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili, tabia na kukuza maendeleo ya kiuchumi, kijamii na utawala bora hujengwa na familia. Ili kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa kuimarisha familia kama kitovu cha maendeleo, Wizara yangu imeandaa Sera ya Maendeleo ya Familia na imewasilishwa Serikalini kufanyiwa maamuzi. Sera hii itatoa mwelekeo thabiti utakaowezesha familia kutambulika kama kiini cha uzalishaji mali na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara yangu imekamilisha kudurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996, na imewasilishwa Serikalini kufanyiwa maamuzi. Wizara imelazimika kudurusu Sera hii kutokana na masuala ya watoto yaliyojitokeza kati ya mwaka 1996 na 2005 na ambayo hayakupewa kipaumbele katika Sera ya mwaka 1996. *(Makofi)*

Masuala hayo ni pamoja na kuwepo kwa ongezeko la idadi ya watoto nchini kutoka asilimia 46 ya wananchi wote mwaka 1996 hadi asilimia 50.6 kwa mujibu wa Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2002. Ongezeko hilo la idadi ya watoto limesababisha ongezeko la mahitaji ya watoto nchini. Masuala mengine ni pamoja na kutoingizwa kwa dhana ya ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali ya maendeleo; suala la kutotambua makundi ya watoto wenye mahitaji maalum kama vile watoto wenye ulemavu, yatima, watoto wasio na makazi maalum, watoto wanaotumikishwa kazi za hatari, janga la UKIMWI na watoto kutotengewa maeneo ya kucheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, niliahidi Bunge lako tukufu kwamba, wizara yangu itafanya ukaguzi wa kina wa vyuo vya Maendeleo ya Jamii, na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kutambua matatizo yanayovikabili Vyuo hivi. Ukaguzi huu ulifanyika na kubaini matatizo mengi ambayo yanahitaji ufumbuzi. Baadhi ya matatizo hayo ni uchakavu wa majengo, miundo mbinu na uhaba wa Wakufunzi.

Jitihada zitahitajika kutatua matatizo ya Vyuo hivi ikiwa ni pamoja na Wizara kuwa na bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nililieleza Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu inakamilisha Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* ambao ni muhimu katika kufikiwa kwa malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Wahisani, Mpango Mkakati huo sasa umekamilika na uko tayari kutekelezwa. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana na wadau wote hao katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu wakati ikiwasilisha katika Bunge lako tukufu Bajeti yake ya mwaka 2005/2006, ilitoa taarifa kwamba, imeanza maandalizi ya kuanzisha uwekaji wa kumbukumbu zinazohusu wanawake katika kompyuta *(Women's Database).*

Madhumuni ya kumbukumbu hizo ni kuisaidia Serikali pamoja na wadau wengine kufahamu wasifu wa wanawake kwa matumizi mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba vitabu vya kumbukumbu hizo vimekwisha chapishwa na vitasambazwa kwa utaratibu ambao utakidhi madhumuni ya vitabu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala na Utumishi: Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilisimamia mahitaji, maendeleo na ustawi wa watumishi wake kwa kuzingatia sheria, kanuni, nyaraka na miongozo mbalimbali inayohusu watumishi wa umma. Masuala ya watumishi yaliyoshughulikiwa ni pamoja na mafunzo, upandishwaji vyeo, uimarishaji wa nidhamu, usalama kazini na kuimarisha ikama za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuboresha utendaji kazi linahitaji mipango mizuri ya kuendeleza rasilimali watu hususan watumishi wa Wizara. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imekamilisha Mpango wa kuendeleza rasilimaliwatu ya Wizara. Utekelezaji wa mpango huu unatarajia kuanza katika mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Aidha, Wizara yangu imewapeleka mafunzoni watumishi wapatao 200 ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi na kuwa na upeo mpana zaidi wa kumudu majukumu yao. Napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Mfuko wa Kuboresha Ufanisi *(Performance Improvement Fund)* uliotuwezesha kushiriki katika mafunzo hayo na kuweza kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imefanikisha zoezi la kupandishwa vyeo jumla ya Watumishi 36 ambao walikuwa hawajapandishwa madaraja kwa miaka mingi na hivyo kuathiriwa na utekelezaji wa Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi sahihi ya watumishi ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kila mtumishi anawajibika kikamilifu na hivyo kukamilisha majukumu aliyopangiwa kwa wakati na kwa kiwango kinachokubalika. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imepata kibali cha kuajiri watumishi 24 ambao tayari wameajiriwa ingawaje idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na ajira mpya 50 zilizoidhinishwa katika Ikama ya watumishi. Aidha, uchambuzi wa mahitaji halisi ya watumishi umeonyesha kuwa Wizara bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Watumishi hasa katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa watumishi unategemea kwa kiwango kikubwa ubora wa vitendea kazi pamoja na mazingira mazuri ya kazi. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imekamilisha awamu ya kwanza ya ukarabati wa ofisi ya Makao Makuu ya Wizara na kuwezesha upatikanaji wa vyumba vya ofisi zaidi ikiwa ni pamoja na Ukumbi wa Mikutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwelekeo na Malengo ya Mwaka 2006/2007 wa Maendeleo Ya Jamii: Wizara yangu itaendelea kuwaandaa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na kuwapa mafunzo ya rejea na ya juu zaidi waliopo ili wanapoajiriwa na kuwezeshwa vizuri na Halmashauri waweze kutoa huduma zilizo bora kwa jamii wakishiriana na sekta na wadau wengine wa Maendeleo ya Jamii. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kutoa mafunzo ya stadi za kazi kwa wananchi, wakiwemo vijana waliomaliza shule za msingi na hata sekondari ili waweze kutumia ujuzi huo katika kujiajiri wenyewe. Hivyo, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitaendelea kuimarishwa kusudi vichangie azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kutoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii walioko kwenye Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya ndio wawezeshaji wakuu wa utekelezaji wa Sera na Programu za Wizara na zile za sekta nyingine, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007, itanunua pikipiki 15 ambazo zitagawiwa katika Halmashauri walao 15 kwenye mikoa ambayo haikupatiwa pikipiki katika mwaka wa fedha 2005//2006.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kutenga asilimia 60 ya nafasi za masomo ya Stashahada za Juu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa watumishi waliopo kwenye Halmshauri ambao wana sifa ya cheti cha Maendeleo ya Jamii. Halikadhalika, Wizara itatoa mafunzo ya rejea kuhusu uandishi wa miradi *(project write ups)* kwa watumishi 60 wa Maendeleo ya Jamii kutoka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii, katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Rungemba, Misungwi na Buhare. Aidha, Wizara itakamilisha uandaaji wa mitaala ambayo itakiwezesha Chuo cha Tengeru kutoa mafunzo ya Shahada katika mwaka wa 2006/2007.

Halikadhalika, Wizara itaandaa mitaala ya Maendeleo ya Jamii, katika ngazi ya Stashahada ili kuanzisha mafunzo katika ngazi hiyo kwenye Vyuo vya Rungemba, Misungwi na Buhare kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya Chuo cha Tengeru kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la mihadhara, maktaba na kufanya matengenezo ya Ofisi. Aidha, Wizara yangu itaweka vifaa vya kisasa vya kuwezesha mawasilano na kukuza matumizi ya teknolojia ya kisasa ya habari na mawasiliano kati ya Chuo na wadau wengine. Ili kuwawezesha watumishi wa Chuo cha Tengeru kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia yatatolewa mafunzo ya kompyuta kwa watumishi 20 katika kipindi cha mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa wanachuo 810 wanawake kwa wanaume, katika Chuo cha Tengeru katika ngazi ya Stashahada ya Juu na wanachuo 600 katika ngazi ya cheti kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Missungwi, Buhare na Rungemba.

Mheshimiswa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu itafanya ukarabati mkubwa katika Chuo cha Buhare ambapo Chuo cha Rungemba kitafanyiwa ukarabati mdogo. Aidha, ujenzi wa maktaba na ukumbi wa mihadhara utafanyika katika chuo cha Tengeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kupunguza tatizo la ajira na umaskini unaolikabili taifa letu, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya stadi za kazi mbali mbali yenye uhitaji kupitia vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Makundi yanayolengwa ni ya wanawake, vijana, wazee, wajane na watu wenye ulemavu. Mafunzo hayo yatawawezesha kujiajiri na hivyo kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, jumla ya wananchi 30,000 watanufaika na mafunzo hayo. Ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika vyuo katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha majengo na miundombinu katika vyuo vingine vinne (4) vya Chala, Chilala, Kiwanda na Malya. Wizara itaweka mitambo ya umeme unaotokana na nguvu za jua *(Solar Power)* katika vyuo vitatu (3) vya Chilala, Muhukuru na Ulembwe na kuwezesha upimaji wa maeneo kwenye vyuo thelathini (30). *(Makofi)*

Aidha, katika kupunguza tatizo la usafiri kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ambavyo viko mbali na makao makuu ya wilaya kunakopatikana huduma muhimu, Wizara yangu kwa kuanzia, katika mwaka huu wa fedha, imepanga kununua pikipiki kumi (10) kwa ajili ya Vyuo vya Chala, Chilala, Chisalu, Kiwanda, Nzega, Malampaka, Mlale, Msaginya, Msingi, Muhukuru na Sofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu na mbinu za kupambana na UKIMWI litaendelea kupewa kipaumbele kwanza kwa kudurusu Mkakati wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya UKIMWI na magojwa ya zinaa na kisha kuusambaza Mkakati huo kwenye Halmashauri. Aidha, kwa kuanzia, Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Singida na Tabora watapatiwa mafunzo ya

mbinu shirikishi yatakayowawezesha kuandaa mipango ya kukabiliana na janga hilo pamoja na wananchi wa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jinsia: Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kuhusu jinsia na namna ya kuingiza masuala ya jinsia katika Mipango, Sera na Mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa Watendaji wa Dawati la Jinsia katika ngazi zote. Vile vile, Wizara itaendelea kushiriki na kuiwakilisha nchi katika mikutano ya Kimataifa na Kikanda inayohusu maendeleo ya wanawake na jinsia na kutekeleza maamuzi mbalimbali yanayotolewa katika mikutano hiyo kwa kushirikiana na wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara itaendelea kuelekeza mikakati na Programu mbalimbali ili kufanikisha azma hiyo. Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake katika Halmashauri zote. Katika kuuboresha Mfuko huo, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinachangia kwenye Mfuko huu ipasavyo. Katika kuufanya Mfuko uwe endelevu, wanawake watahamasishwa na kuendelea kupewa mafunzo ya ujasiriamali kabla ya kupatiwa mikopo ili kuboresha uendeshaji wa biashara zao na marejesho ya mikopo.

Vile vile, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake waanzishe vyama vya wanawake vya ushirika vya kuweka na kukopa *(SACCOS)*. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kuwezesha wanawake kushiriki katika maonesho ya biashara ya ndani na nje ya nchi. Aidha ili kuboresha mchango wa wanawake katika kuondoa umaskini katika soko la ushindani, mchakato wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake utakamilishwa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinatokomezwa, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa wa Serikali wanaosimamia utekelezaji wa sheria na upatikanaji wa haki katika jamii. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata wataelimishwa kuhusu utunzaji wa taarifa na takwimu za wanawake na wanaume waliodhurika na vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kupitia sheria mbalimbali ili kuziboresha zile zinazowanyima haki wanawake. Aidha, Wizara kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii, itawahamasisha Viongozi wa ngazi mbalimbali katika jamii kuhusu Sheria za Makosa ya Kujamiiana (1998), Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi Vijijini (1999). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanyika kwa zoezi la kubainisha mahitaji ya wanawake wajane na wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI katika Halmashauri tano za majaribio, ambazo ni Manispaa ya Morogoro, Handeni, Rombo, Muheza na Rufiji, Wizara itaendesha mafunzo ya ujasiriamali na kutoa ushauri nasaha kwa wanawake 200 waliobainishwa na mitandao yao ambao watatoa mafunzo kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2006/2007 Wizara yangu itaweka mkazo katika kuimarisha hali ya maisha ya watoto walio katika mazingira magumu na

kutayarisha mipango shirikishi itakayobaini maeneo ya kufanyiwa kazi. Makundi ya watoto yatakayozingatiwa ni watoto yatima, watoto wanaoishi mitaani, watoto wanaotumikishwa katika kazi za hatari wakiwemo watoto wanaosafirishwa kutoka vijijini kwenda mijini kwa kupewa ahadi za uongo kama vile kupatiwa elimu na badala yake wanatumikishwa. Katika kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa na maisha bora, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na Mashirika yasiyo ya Kiserikali itaandaa mpango utakaohakikisha watoto wanaondolewa mitaani na wanapatiwa elimu kama haki yao ya msingi na kuwaunganisha (*reintegrate*) na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ni mwanzo muhimu kwa binadamu. Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Sekta na Taasisi mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya watoto, itaendelea kuandaa Mkakati wa Taifa wa elimu ya malezi ya watoto wachanga chini ya umri wa miaka nane. Lengo la Mkakati ni kuhakikisha kuwa watoto wanapatiwa mwanzo mzuri wa uhai, ulinzi, makuzi na ustawi wao. Aidha, Wizara yangu inakusudia kuelimisha familia na jamii kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, kwa kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri na Vyombo vya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuendesha mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhusu madhara ya utumikishwaji watoto katika kazi za hatari katika Halmashauri, ili waweze kuelimisha na kuhamasisha familia, jamii na watoto wanaotumikishwa katika kazi hizo za hatari. Lengo ni kuhakikisha kuwa Halmashauri na wadau wa maendeleo ya watoto wanawaondoa na kuzuia watoto kujiingiza katika kazi hizo na kuwapatia kazi mbadala za kuongeza kipato cha familia pamoja na kuwapatia elimu kama haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2006/2007, Wizara yangu itaelimisha jamii kwa njia ya matangazo na habari kupitia Vyombo vya Habari ili kuongeza uelewa wao kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia *(Population and Family Life Education).* Hali kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Sekta na Taasisi zinazoshughulikia masuala ya familia na watoto vikiwemo Vyombo vya Habari, itaandaa zana za habari, elimu na ushawishi kwa lengo la kutoa mafunzo kwa Maafisa Mendeleo ya Jamii 260 katika ngazi ya Kata. Maofisa hao wataisambaza elimu hiyo kwa familia na jamii ili kuhakikisha maisha bora ya familia na kuziwezesha kulea watoto kulingana na uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuelimisha jamii na familia kuhusu haki za msingi za watoto kulingana na Mikataba ya Kimataifa ya Haki na Ustawi wa Mtoto. Elimu hiyo itaendelea kutolewa kwa kushirikiana na Vyombo vya Habari kupitia madhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika na Siku ya Familia Duniani. Vile vile, Wizara yangu itaendelea kusambaza na kuelimisha jamii kuhusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto na Sera ya Maendeleo ya Familia ambazo zinazingatia haki na maendeleo ya watoto na familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji na mila zingine zenye madhara kwa wanawake na watoto wa kike hapa nchini,

Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutoa elimu ya ushawishi dhidi ya vitendo hivyo kwa watekelezaji wa sheria *(law enforcers)* ili waweze kutetea, kulinda na kutoa maamuzi ya haki kwa mujibu wa sheria kwa wanaofanya vitendo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa haki za kikatiba za watoto zinafahamika na kutekelezwa kikamilifu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) itaendelea kuuwezesha Mtandao wa Harakati za Watoto *(Tanzania Movement for and with Children)* kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara yangu itahamasisha watoto washiriki katika kutoa mawazo yao na kusikika katika masuala yanayohusu maslahi na ustawi wao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Vile vile, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa watoto itaendelea kusaidia Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhamasishwa uanzishwaji wa mabaraza haya katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inasisitiza kuimarisha utaratibu wa Mashirika ya hiari. Katika Mwaka 2006/2007, tutaendelea na Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kuyawezesha kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi hususan katika utekelezaji wa MKUKUTA na Malengo ya Milenia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuwezesha uboreshaji wa mazingira ya utendaji kazi kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa huduma bora kwa walengwa na jamii kwa ujumla. Ili kufikia lengo hilo, Wizara yangu itaratibu na kufuatilia kwa karibu shughuli na taarifa za Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Wilaya na Mikoa, kwa lengo la kupima utendaji kazi wao na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mashirika hayo ili yaweze kutoa huduma bora na endelevu kwa jamii hususan katika maeneo ya vijijini. Aidha, Wizara itatafsiri Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 24/2002 katika lugha ya Kiswahili kuwawezesha wadau wengi kuielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za usajili wa Mashirika haya katika ngazi za Wilaya na Mikoa, pia itafanya mapitio na kubaini matatizo yaliyojitokeza, kuwaongezea ujuzi kwa kuwapatia mafunzo Wasajili Wasaidizi ili kuwawezesha kutoa huduma bora na kwa ufanisi zaidi. Aidha, taratibu zinafanyika ili kuweza kuwashirikisha Maafisa Maendeleo ya Jamii katika uratibu wa shughuli za Mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaimarisha mifumo ya mawasiliano miongoni mwa wadau wa Sekta ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na kuendelea kuimarisha Benki ya Takwimu za Mashirika haya *(NGOs Data Base),* kwa madhumuni ya kuchochea matumizi sahihi ya raslimali zilizopo, kuongeza ushiriki, uwazi na uwajibikaji katika Sekta ya Mashirika haya. *(Makofi)*

Aidha, kupitia mifumo hii, wadau wataweza kufahamu ni maeneo gani ya nchi yetu Mashirika haya yameshamiri kwa wingi, malengo yake na walengwa wake ili kuwawezesha kuchukua maamuzi sahihi ya kuenea na kutoa huduma kwenye maeneo

ambayo hayajafikiwa na yenye uhitaji mkubwa wa Mashirika haya. Katika kutekeleza hilo, Wizara yangu itawezesha kuwepo kwa mkakati wa mawasiliano, kitabu cha orodha *(NGOs Directory),* kitabu cha taarifa ya mwaka ya Sekta ya Mashirika haya na kuboresha taarifa za sekta hii katika Tovuti ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu iliandaa mfumo wa ufuatiliaji wa tathmini unaozingatia jinsia *(Computerized Gender Sensitive Monitoring and Evaluation System).* Mfumo huo wa kompyuta umetengenezwa na Wizara pamoja na Kituo cha Kompyuta cha Chuo Kikuu *(University Computing Centre).* Wizara imeshauweka katika mtandao wa kompyuta wa Wizara kwa majaribio na tunategemea kuanza kuutumia rasmi mwezi Septemba mwaka 2006. Mfumo huo utaiwezesha Wizara kutathmini masuala ya jinsia na watoto katika sekta mbalimbali. Mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu itakusanya takwimu muhimu ili mfumo uliowekwa uweze kutumika. Pia, Wizara itaendelea kuweka kumbukumbu muhimu kwenye tovuti ya Wizara ili taarifa zinazohusu Wanawake, Watoto, Maendeleo ya Jamii na Jinsia ziweze kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kukinga jamii haswa wanawake na watoto waishio katika mazingira magumu, Wizara yangu, kwa kushirikiana na sekta na wadau mbalimbali, itaratibu uandaaji wa Mpango wa Kinga ya Jamii. Mpango huu utahakikisha wanawake na watoto wanapata haki zao za kuishi, kuendelezwa, kushiriki, kulindwa na kutobaguliwa. Pia, utabainisha maeneo mbalimbali ya uwajibikaji kwa kila mhusika na kuweka utaratibu wa mgawanyo wa majukumu kwa msingi wa ubia kati ya Halmashauri na wachangiaji wengine kama vile Asasi za Kiraia na wanajamii kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaanza mchakato wa kudurusu Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000. Madhumuni ya kudurusu Sera hii ni kuingiza maamuzi mbalimbali yanayohusu maendeleo ya wanawake na jinsia yaliyofanyika katika mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Pia Wizara itaandaa Programu ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii ambayo itatekeleza Sera hii na Sera nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne imeweka mkazo katika kutoa huduma bora kwa wananchi, kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora kwa wateja ili kujenga uendeshaji unaozingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza mara kwa mara juu ya uwajibikaji sehemu za kazi na kuwa wazi kwa wale tunaowahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake ili waweze kupata, elimu na maarifa ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kutoa mapendekezo ya mafunzo ili kutekeleza programu ya mafunzo kupitia Mfuko wa kuongeza ufanisi *(Performance Improvement Fund).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuendeleza vita dhidi ya rushwa kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hivyo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itatilia mkazo zaidi katika kutekeleza Mkakati wa Wizara wa kupambana na rushwa kwa kutoa elimu kwa watumishi wake kuhusu namna ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara ili kupunguza tatizo la uhaba wa ofisi na vitendea kazi kama nilivyoeleza awali, tatizo hili bado lipo na linaathiri ufanisi katika utendaji kazi. Hivyo, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea na ukarabati wa ofisi zilizopo Makao Makuu ya Wizara na kununua vitendea kazi, samani na mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwashirikisha wadau wetu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea na utaratibu wake wa kuitisha Mkutano Mkuu wa Mwaka unaoshirikisha Uongozi, Maafisa wa Wizara, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Washauri wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa, Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na wawakilishi wa Wizara tunazoshirikiana nazo kwa karibu katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itakamilisha mpango wa kupambana na maambukizi ya UKIMWI sehemu za kazi. Mpango huu utatanguliwa na tafiti ya kiwango cha maambukizi pamoja na utoaji wa mafunzo katika Makao Makuu ya Wizara na kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mtambuka *(cross cutting)*. Kwa mantiki hii, tutaendelea kuhitaji ushirikiano wa karibu sana na wadau wetu mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Lengo kubwa ni kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii na hivyo kuondoa umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wote. Aidha, ushirikiano baina ya Wizara pamoja na Halmashauri ni muhimu sana katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, naomba kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr Batilda Salha Burian (Mbunge), kwa ushirikiano wake. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mariam J. Mwaffisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu katika ngazi zote kwa ushirikiano na moyo waliouonyesha, hususan katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote ambao tumekuwa tukishirikiana nao kwa njia moja au nyingine katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Naomba kutumia fursa hii na kwa kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wafuatao: Shirika la Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP),* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Shirikisho la Vyama

vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA), Chama cha Wanawake Viongozi katika Kilimo na Mazingira - Tanzania (TAWLAE), Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), *Plan Tanzania,* Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF)* na Mashirika mbalimbali pamoja na wale wote tunaoshirikiana nao katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa manufaa ya jamii na Taifa zima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wahisani mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kugharamia miradi mbalimbali nchini inayotekelezwa na Wizara yangu. Wahisani hao ni Serikali za Canada, Ireland, Italia, Netherlands, Norway na Sweden ambao wanaendelea kutusaidia kwa kupitia Mashirika yao ya Kimataifa: Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto *(UNICEF),* Benki ya Dunia *(WB),* Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu *(UNFPA),* Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake *(UNIFEM),* pamoja na Mashirika mengine ya nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2006/2007, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Sh.10,418,355,000/=. Kati ya hizo Sh.8,297,354,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Sh.3,254,754,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.5,042,600,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges).* Aidha, Wizara inaomba kiasi cha Sh.2,121,001,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Sh.1,997,001,000/= ni fedha za hapa nchini na Sh.124,000,000/= zikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha Hotuba ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kaka zangu, wadogo zangu na Ndugu zangu, pamoja na watoto wangu Fredy, Cliff, Adnan na Leeford ambao wako hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau pia kumshukuru sana Ndugu yangu wa hiari Mzee Kitwana Kondo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nafikiri kabla sijamruhusu Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati, niwataje waombaji waliiomba kuchangia ili kama wako mbali waweze kurudi ukumbini.

Tunao wachangiaji tisa mpaka sasa hivi na msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Devotha Likokola, atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Charles Keenja. Kwa hiyo, ninaomba tafadhali sana kama wako nje ya ukumbi wa Bunge wajiandae kwa kuwa mara baada ya hotuba hizi tutaanza kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati, tafadhali.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 81(1) ya Mwaka 2004, naomba sasa nitumie fursa hii kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka uliopita 2005/2006 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku hii ya leo, pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii katika awamu hii, kwa niaba ya Kamati napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Tawala. Aidha, naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa na kuchaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Luteni Mstaafu Yusuph Makamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote, naomba kwa niaba ya Kamati nitoe pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwateua wanawake wengi katika nafasi mbalimbali za uongozi. Ukweli tumeanza kuona wanawake wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Spika, (Bwana Viwango) kwa kuchaguliwa kwake na kuanza kuendesha Bunge hili kwa kasi na viwango vya hali ya juu. Aidha, nampongeza sana Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa umakini wao katika kuliongoza Bunge letu hili kupitia Kamati zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (Mbunge), kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya, nawapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa

kazi zao nzuri. Pia, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi wao na jinsi walivyoanza kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa namna ya pekee namshukuru sana mume wangu mpenzi Bwana Farouk Selemani, pamoja na familia yangu yote kwa jinsi wanavyonipa moyo katika kazi zangu. Nakushukuru wewe Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa jinsi tunavyoshirikiana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu, wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka mitano na kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi hii ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Kamati ilizingatia mambo yafuatayo: -

(i) Dira ya Wizara.
(ii) Dhima ya Wizara.
(iii) Majukumu ya Wizara.
(iv) Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Kipindi cha Mwaka 2005/2006.
(v) Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2005/2006.
(vi) Mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2005/2006.
(vii) Malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2006/2007.
(viii) Makadirio ya mapato na maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanywa kwa Mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya Wizara ni kuleta mabadiliko katika fikra za jamii, kuleta usawa wa kijinsia, haki za watoto na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kushirikisha Asasi zisizo za Kiserikali kama wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Wizara inalenga kuiwezesha jamii kupata maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kupitia njia ya ushirika na mawasiliano, kuandaa sera, mikakati, miongozo na kuratibu na kusimamia shughuli za Asasi zisizo za Kiserikali kwa ajili ya kuendeleza uwezo wa jamii, usawa wa kijinsia na haki za watoto.Ili Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ieleweke vizuri zaidi, naomba nilikumbushe Bunge lako tukufu majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa Sera za Wizara, kuzisimamia, kuziratibu na kutathmini utekelezaji wake;

(ii) Kueneza na kuendeleza dhana ya Maendeleo ya Jamii kwa kuwashirikisha wananchi wote;

(iii) Kutayarisha programu, mikakati na mifumo ya utekelezaji ili kuchochea maendeleo ya jamii;

(iv) Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo ya kufaidika sawa katika maendeleo hayo;

(v) Kuendeleza kuhamasisha na kuiwezesha jamii kuwapatia watoto haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kutobaguliwa na kushiriki katika maendeleo ya Taifa;

(vi) Kuratibu shughuli za Mashirika yasiyokuwa ya Kkiserikali *(NGO)* na kuyawezesha kufanya kazi kwa uwazi na ufanisi zaidi; na

(vii) Kusimamia utendaji kazi Wizarani kwa misingi ya uadilifu, haki na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza takriban maagizo yote ya Kamati kwa kipindi cha 2005/2006. Aidha, Kamati inaendelea kushauri yafuatayo katika maagizo yake:-

Katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, wanawake wanaokopa wajengewe uwezo mpana kwa kupatiwa elimu ya jamii na jinsia, stadi za kazi, ujasiriamali, akiba na mikopo ili waweze kupata mbinu bora za biashara.

Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwajengea uwezo mpana wanawake wanaokopa. Kwa kushirikiana na wadau wengine, Wizara hutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake hao ili kuwawezesha kubuni, kupanga na kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi zaidi kupitia wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavikundi wahamasishwe kuweka akiba mara kwa mara ili kuongeza uwezo wao wa kukopa. Pia wahamasishwe kujisajili katika Vyama vya Akiba na Mikopo, pamoja na utekelezaji wa kuwawezesha watendaji Mikoa/Wilaya katika azma ya uundaji *SACCOS*. *(Makofi)*

Maafisa Maendeleo Jamii wapatiwe usafiri ili waweze kuwafikia wanawake wengi zaidi hasa wa vijijini kwa ajili ya kutoa elimu juu ya mikopo na akiba, hii itasaidia wanawake wengi kutambua umuhimu wa kuchukua mikopo, kurejesha na kujiwekea akiba. Katika mwaka wa fedha uliopita, Wizara imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati kuhusu suala la kuwapatia usafiri Maafisa Maendeleo ya Jamii, ili kutekeleza majukumu yao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwafikia wanawake wengi zaidi hasa wa vijijini kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu mikopo na akiba. Wizara ilizipatia pikipiki Halmashauri kumi kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Kuhusu kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko huu kwani kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo na hivyo kuwanufaisha wanawake wachache tu wa mijini.

Aidha, mikopo hii haichangii kukua kwa biashara na ajira kwa wale wanaokopa kwani viwango vya mikopo vilivyotolewa ni vidogo sana na haviongezeki. Mfano, kwa zaidi ya miaka kumi viwango vya mikopo vimekuwa vikitolewa kati ya Sh.50,000/= hadi Sh.100,000/=. Hizi ni fedha kidogo sana kwa mikopo wanayopata wanawake. *(Makofi)*

Katika kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake unaongezeka na pia kuwanufaisha wanawake wengi zaidi hasa walio vijijini, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kuhimiza Halmashauri kuchangia asilimia 5 ya mapato yao kwenye Mfuko. Kutokana na Mfuko kuwa wa mzunguko, Wizara imejitahidi kufuatilia marejesho ili Mfuko uweze kukua na wanawake wengi zaidi kupatiwa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Fedha zimewasiliana kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuwezesha uanzishaji wa Benki ya Wanawake.

Aidha, kiasi kidogo cha fedha kimetengwa katika mwaka wa 2006/2007 kwa ajili hiyo. Mtalaam ameanza kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uanzishwaji wa Benki hiyo na matokeo ya uchunguzi huo yatawasilishwa Benki Kuu kwa ajili ya uanzishwaji.

Kwa kuzingatia majukumu mengi ya Wizara, Kamati ilishauri Serikali kuona umuhimu wa kuiongezea bajeti. Serikali imeona umuhimu wa kuiongezea Wizara fedha na ndiyo sababu kila mwaka bajeti ya Wizara imekuwa ikiongezeka kulingana na hali ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia Bajeti ya Wizara, Kamati iliombwa kuyakubali mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto – Fungu Na. 53 kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida Sh. 8,297,354,000/=

(b) Matumizi ya Maendeleo Sh. 2,121,001,000/=

**Jumla .......................... Sh. 10,418,355,000/=**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kupitia na kupata maelezo kuhusu Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kuongeza ajira, Kamati inaona umuhimu wa kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kama vituo vya kuwajengea wananchi uwezo na ujuzi na hasa katika fani za ufundi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha Sh.253,571,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. *(Makofi)*

Hata hivyo Kamati inaona kuwa kiasi hiki cha fedha kilichotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya uchakavu wa vyuo vyenyewe na hivyo kufanya visiwe na mvuto kwa wanafunzi kujiunga na vyuo hivi. Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za maendeleo zaidi katika mwaka ujao wa fedha ili vyuo hivi vifanyiwe ukarabati.

Kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni mafundi katika fani mbalimbali, Kamati inashauri, wananchi na wanafunzi hao wapewe kipaumbele cha kazi za kukarabati majengo chakavu katika vyuo husika, sheria ya tenda isiwabane, Serikali iwape kibali cha kufanya ukarabati, bila kuwashindanisha kwa tenda.

Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, Kamati inashauri uongozi wa vyuo hivyo kuwa wabunifu, kubuni mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuzalisha na kujiingizia fedha zao wenyewe badala ya kusubiri ruzuku ambayo hutolewa kiasi kidogo tu na haikidhi mahitaji ya vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo ya uchakavu wa mejengo, mazingira magumu ya kazi na walimu wengi wamekuwa wakishindwa kumudu maisha katika maeneo vilivyopo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na hivyo kuwepo kwa uhaba wa wakufunzi kwa 40.8%, Kamati inashauri kuweka mkakati wa kuboresha maisha ya walimu wa vyuo hivyo, ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba nzuri na kuwalipa malipo maalum ya mazingira magumu ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Maendeleo ya Jamii ni watu muhimu sana katika Jamii, lakini Maafisa hawa wamekuwa hawatumiwi vizuri na Halmashauri wanakofanyia kazi na inaonekana bado Wakurugenzi wa Halmashauri hawajatambua umuhimu wa Maafisa hawa. Kamati inashauri elimu itolewe kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu umuhimu wa kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii. Ingawa katika mwaka wa Fedha wa 2006/2007 Wizara haijazingatia umuhimu wa suala la usafiri kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Kamati inashauri mradi huo uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii kutokuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Maafisa Maendeleo ya Jamii. Utekelezaji wa majukumu kwa Maafisa hawa umekuwa mgumu. Kamati inashauri Maafisa Maendeleo ya Jamii wawe na mawasiliano ya moja kwa moja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii washirikiane kwa karibu sana ili kuboresha utendaji kazi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SELF* ni shirika ambalo limekuwa likitoa msaada mkubwa kwa Jamiii ya Watanzania likiwa chini ya Ofisi ya Rais. Wasimamizi wakubwa wa maendeleo hayo wako chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto.

Kamati inashauri Shirika hili liwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana katika kuleta maendeleo. Kumekuwepo na upungufu wa asilimia 57.3% katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii hasa katika fani za menejimenti, uandaaji wa miradi na takwimu, mawasiliano, utunzaji wa watoto na usanifu majengo, hali hii inachangiwa zaidi na mazingira magumu ya Walimu katika maeneo husika.

Kwa kuwa Walimu hawa ni muhimu katika kuwaelimisha vijana wetu, Kamati inashauri kuwepo na malipo maalum kwa ajili ya Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Ili kuwavutia, ni pamoja na kuwajenga ofisi, nyumba nzuri na kuwapatia vitendea kazi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha Sh. 464,966,000/= kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na kiasi cha Sh.524,220,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Fedha hizi zilizotengwa ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na hali halisi ya mahitajii halisi ya vyuo hivi. Kamati inashauri Serikali kutenga fedha zaidi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa ajili ya kuboresha hali ya vyuo hivi vyenye hadhi ya kutoa stashahada.

Kamati inashauri Wizara ianze kujenga mpango maalum kupitia Halmashauri ili wanawake wasiofikiwa na wadau wa nje waelimishwe na Wizara yenyewe. Aidha, Majumba ya Maendeleo yafufuliwe kwa kazi hiyo ya kuelimisha jamii stadi mbalimbali za maisha na ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo kubwa la upungufu wa watumishi. Mahitaji halisi ya Watumishi wanaotakiwa kuwepo ni 3,300, lakini Wizara kwa sasa ina jumla ya Watumishi 1,095 sawa na robo tu ya watumishi wanaohitajika. Upungufu huu wa watumishi 2,205 unasababisha Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati inashauri Serikali kufanya juhudi za makusudi ili kuongeza watumishi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara, pamoja na Serikali kuongeza fedha katika Bajeti ya Wizara, Kamati inashauri timu ya Wizara kuongeza ubunifu unaoendana na dira na sera za Wizara ili kushawishi Serikali kuongeza fungu la Bajeti la Wizara. Aidha, Kamati pia inashauri Wizara ione uwiano wa miradi inayohitajika kwa maendeleo ya jamii na hivyo itengenezewe utaratibu na kuombwa fedha na sio miradi ya maendeleo kubaki kila siku katika dhana ya ukarabati wa majengo tu. Mfano, Kamati inashauri sasa kitita cha teknolojia rahisi kitafsiriwe kwa vitendo na siyo nadharia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika mpango wa kazi za 2006 imejiwekea lengo la kutoa mafunzo na huduma kwa Wanawake 200 tu. Kamati kwa kuzingatia kuwa Wanawake waishio na virusi vya UKIMWI ni wengi kulingana na takwimu zinazotolewa mara kwa mara na hata jamii nzima ya Tanzania ina asilimia 51 ya Wanawake, Kamati inashauri katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 idadi hiyo ya Wanawake watakaopatiwa mafunzo iongezeke.

Kuhusu kuhamasisha vikundi kuweka akiba, Wizara iweke suala la Vyama vya Akiba na Mikopo kuwa *agenda* maalum ya kuwakomboa Wanawake - mfano: Rombo, Mufindi, Ruvuma na Wilaya zote, Iramba, ambako Vyama hivyo viko tayari. Aidha, Wizara itenge fungu kupitia *W.D.F.* kuvipa nguvu Vyama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005/2010, suala la kuwawezesha Wanawake limepewa kipaumbele. Mchakato wa kuanzisha hiyo, ulianza toka miaka mitano ya Bunge lililopita. Aidha, hatua mbalimbali zichukuliwe ingawa katika mwaka huu wa fedha Wizara imetenga kiasi cha Sh. 102,961,000/= tu, kwa ajili ya uwezeshaji wa uanzishwaji wa Benki ya wanawake, haionyeshi kiasi chochote cha fedha kutengwa kwa ajili ya uanzishwaji wa Benki yenyewe. Kamati inasikitishwa na hatua za polepole za Serikali katika kuchangia uanzishwaji wa Benki hii na inasisitiza kuharakishwa kwa uanzishwaji wa Benki hiyo ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya uanzishaji wa Benki na kushirikisha Wizara nyingine ili wanawake waanzishe Vyama vya Akiba na Mikopo ambavyo vitasaidia sana katika kuunda mitaji ya Benki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria mbalimbali zinazochelewesha usawa wa jinsia, zipo sheria mbalimbali zilizocheleweshwa mahusiano mema ya jinsia miongoni mwa jamii. Mfano wa sheria hizi ni Sheria ya Familia ya mwaka 1971 na sheria nyingine zinazohusiana na sheria hiyo. Lakini ipo sheria inayomlazimisha mwanafunzi wa kike kufukuzwa Shule baada ya kupata mimba. Kufukuzwa Shule kwa sababu ya mimba, ni adhabu isiyo na mafanikio. Kwa mfano, kwa mwaka 2001 hadi mwaka 2005 jumla ya wasichana 12,413 waliondolewa masomoni kwa kupata mimba Shuleni na idadi hii ni ya wale waliojulikana. Wapo wengine waliotoroka kwa kuhofia kujulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watoto waliopata mimba hizo kwa makusudi, lakini wapo waliobakwa na kulazimishwa. Adhabu hiyo husababisha kutofikia lengo la idadi sawa ya wavulana na wasichana katika Elimu ya Juu. Lakini yapo madhara mengine mengi yatokanayo na tatizo hilo. Kamati inashauri Serikali kuiga mfano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuamua kufuta sheria hiyo. Tunaomba mjadala wa wazi kuokoa watoto hao wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya fedha kiasi cha Sh. 15,007,000/=, lakini iliweza kukusanya kiasi cha Sh.3,594,000/= tu. Hiki ni kiasi kidogo sana kwa makusanyo ya mwaka mzima. Bajeti ya mwaka 2006/2007 Wizara imejiwekea malengo ya kukusanya kiasi cha Sh.25,000,000/=. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia

na Watoto kuweka mikakati mizuri itakayowawezesha kukusanya kiasi hicho cha fedha kama walivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongezea Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutoka kiasi cha Sh.8,426,084,000/= mwaka 2005/2006 hadi Sh.10,418,355,600/= mwaka huu wa fedha 2006/2007. Hata hivyo, fedha iliyotolewa, kiasi cha Sh.10,418,355,600/= bado ni ndogo sana ukilinganisha na majukumu mengi iliyonayo Wizara hii. Kiasi cha Sh.2,121,001,000/= kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo ni kidogo sana. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuiongezea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Bajeti na hasa katika fedha ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1960 kulikuwa na sinema ambazo zilikuwa zinatoa elimu kwa Jamii kuhusu afya, lishe bora, matunzo kwa watoto, umuhimu wa elimu na kadhalika. Elimu hii ilikuwa na matokeo mazuri sana katika Jamii. Kwa kuwa Jamii nyingi za Kitanzania bado hazijaendelea na hazijui kinachoendelea, Kamati inashauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii wapatiwe sinema za namna hiyo ili kutoa elimu ya maendeleo ya Jamii, kwani kuona ni kusadiki

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian - Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ndugu Mariam Mwafisi - Katibu Mkuu na Maofisa wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuwasilisha Bajeti hii mbele ya Kamati na hatimaye kufikisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa michango yao wakati wa kujadili Mapendekezo ya Bajeti hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Wajumbe hao ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub S. Masoud - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. V. Komu, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan,

Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Fatma Othmani Ally, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila na Mheshimiwa Dorah H. Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, kwa Uongozi wenu hodari na makini katika kuliendesha Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kukupongeza wewe Mwenyekiti wangu wa Bunge, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwa kuanza uongozi wenu vizuri kwa vikao vyote hasa mnapokasimiwa madaraka, mkawekwa hapo juu. Nawashukuruni. *(Makofi)*

Aidha, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila kukwama. Vile vile, niwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Angelina Sanga na Ndugu Joshua Chamwela kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2006/2007 ambayo ni kiasi cha Sh.10,418,355,000/=. Naomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kuipitisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Othman. Mimi kwa kweli kwa usomaji wako makini, naomba niunge mkono hoja yako kwamba wanawake wanaweza. Sasa namwita Mheshimiwa Anna M. Komu, Mgombea Mwenza wa Chama cha *CHADEMA*. *(Makofi)*

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu kwa kupata wasaa huu ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5) (b) (c) na 81 (1) toleo la 2004, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu binafsi kwa Spika, Naibu wake kwa kuwa viongozi wa kujivunia katika kuongoza chombo hiki chenye hadhi ya kipekee katika nchi yetu. Aidha, nakupongeza wewe na Mheshimiwa Ndugai kwa kuwa Wenyeviti mliochaguliwa kuwasaidia katika kazi ya kuongoza Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kukishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo kwa kuniteua kuwa Mbunge kwa nafasi maalum. Ninaahidi kuwa nitafanya kila niwezalo ndani ya uwezo wangu kutimiza majukumu niliyopewa na Chama pamoja na Watanzania kwa ujumla wake. Nitaitunza imani yao kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, natoa shukrani zangu za dhati kwa *Hans Seidal Foundation,* kwa elimu waliyonipa ya kunijenga kuwa Kiongozi. Aidha,

nina washukuru kwa kutoa elimu hiyo kwa wanawake. Ninaamini kwamba wale wote waliopata elimu hiyo ni viongozi imara kabisa na mifano tunaiona mpaka Wakuu wa Wilaya wamo. *(Makofi)*

Aidha, ninamshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Slaa kwa kuwa na imani na mimi na kuniteua kuiwakilisha Kambi katika Wizara hii nyeti na kubwa. Pia, nashukuru kwa ushirikiano wanaonipa. Bila kumsahau Naibu wangu, Mheshimiwa Salim Yusuf Mohamed kwa ushirikiano alioutoa katika maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina dira iliyo nzuri hasa kwa kuzingatia kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ina mikakati ya kuondoa umaskini kwa wananchi wake japokuwa utekelezaji wa mipango hiyo haupo,bali ni mikakati ambayo hadi sasa imo kwenye makaratasi tu. Ni matumaini yetu kuwa, baada ya Bajeti hii, tutaona utekelezaji wake. Dira inalenga kuwa na Jamii yenye uwezo thabiti na kutambua matatizo yanayoikabili ya kuweka mikakati ya kuyatatua kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa lengo la kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya maendeleo ya jamii ilitungwa mwaka 1996. Maudhui ya sera hiyo ni ushirikishwaji jamii katika sera nyingine za Kiserikali na kijumla, Serikali ilijitahidi kuwa na mipango ya maendeleo, lakini mafanikio yalikuwa hafifu, kwani jamii inaendelea kubweteka kwa kukosa usimamiaji au mwongozo wa jinsi ya kutumia raslimali walizonazo na kujikwamua kiuchumi.
Fedha zilizotengwa kwa utekelezaji wa mipango hiyo haikueleweka vyema kutokana na uwezo mdogo wa utekelezaji *(capacity to implement)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na waelimishaji ambao wataweza kuona *opportunities* ambazo zipo katika jamii na jinsi zitakavyosaidia katika kuendeleza jamii husika.

Kama ambavyo tumekuwa tukisema katika hotuba zetu kadhaa kuwa Watanzania sio maskini kama dhana ilivyojikita katika Watawala wa nchi hii, ila wanachokosa ni mikakati na mbinu zinazoeleweka za kuwafanya watumie ardhi yao na shughuli wanazozifanya ili ziwaingizie kipato. Mfano, kilimo cha mbogamboga kinaweza kuwa mkombozi kwa wakulima wadogo wadogo kama vitaazishwa viwanda vidogo vya kusindika matunda na mboga na kumilikiwa na wakulima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii kama dira ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii inavyosema kwamba ni ya kuleta mabadiliko katika fikra za jamii na kuleta usawa wa kijinsia, haki za watoto na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kushirikisha Asasi zisizo za kiserikali kama wadau wa maendeleo, ni vyema elimu ya kutosha itolewe, kwani ajira sio ya Serikali tu. Lakini dhana hiyo iende sambamba na kuwawezesha ili wabakie huko waliko na sio kukimbilia Mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ni dhana pana inayounganisha mambo mengi sana, lakini katika hotuba hii nitapenda kujikita zaidi kwenye ujenzi wa jamii

inayowajibika *(responsible society).* Ni ukweli kuwa bila ya kuwa na jamii inayowajibika, hatuwezi kujenga Taifa linalojitawala na kujitegemea. Miaka yote tutakuwa tegemezi kwa mambo mengi. Taifa haliwezi kufanya maamuzi yake kulingana na mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa matatizo yote ya kiuchumi, rushwa,ujambazi, matumizi ya madawa ya kulevya na Miji yetu kuwa katika hali mbaya ya uchafu, chanzo chake ni jamii isiyowajibika. Ujenzi wa jamii inayowajibika ni jambo hasa linalotakiwa kuanzia katika ngazi ya familia na halihitaji kuwa familia ni tajiri au maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hili lianzie katika ngazi ya familia, nina maana kuwa, malezi ya sisi tulivyolelewa na ni jinsi gani tunazilea familia zetu ili vijana wetu wawe wawajibikaji. Uwajibikaji ni pamoja na mtu anavyothamini mali ya Umma, anavyotumia madaraka aliyopewa kwa manufaa ya Umma, anavyoiheshimu familia yake, anavyopenda na kutunza mazingira yaliyomzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa mtazamo wa jumla inaitwa jamii ya Watanzania japokuwa tumetoka katika makabila tofauti. Kitu ambacho ni kimoja katika makabila yote ya jamii ya Watanzania ni heshima na kuthamini kitu alichonacho. *(Makofi)*

Sasa hivi tunashuhudia mambo ya ajabu kabisa! Pale watu ambao wanatakiwa kuwa kioo cha jamii wanapotoa rushwa ili wapate madaraka katika medani ya kisiasa, wazazi tumeshindwa kuchukua majukumu yetu ya msingi ya kutunza familia. Naomba hili niliweke sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutunza familia sio tu kuhakikisha kuwa familia imekula na watoto wanalipiwa karo za Shule, bali ni kuhakikisha kuwa kuna ufuatiliaji wa karibu wa wazazi kwa watoto nini wanajifunza Shuleni na watoto wanawajibika vipi kwa mazingira ya Shule na nje ya Shule, kujenga upendo ndani ya familia na kuwashirikisha watoto katika maamuzi ya kuzijenga na kuziendeleza familia husika, ili kuwa jamii inayowajibika na viongozi wenye upendo na nchi yao hapo baadaye. Hili sisi Waheshimiwa Wabunge tunalielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali na hasa sisi ambao ni viongozi kuwa mfano bora katika familia na katika mchakato mzima wa kuwania madaraka ya kisiasa au mengine. Kwani, inaaminika kuwa kiongozi aliyepata madaraka kwa misingi ya kutokuwajibika, hawezi kuwajibika pindi akipata madaraka hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, hatuna budi tujiangalie kwanza sisi viongozi wajibu wetu ni nini katika familia na jamii kwa ujumla? Tunaamini suala la kujenga jamii inayowajibika, sio la Serikali na Wizara husika peke yake bali ni suala la kila mmoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna utafiti kuhusu jinsi gani jamii yetu inavyoishi, inavyoathirika au inavyozama kiuchumi bila ya matumaini ya maisha mazuri kwa sasa na hata hapo baadaye, tayari vimeshakamilika, kwani sisi wote ndio tunaoishi katika jamii hizo na ni mashahidi tosha wa yale yote ambayo jamii imekuwa ikiathirika nayo. Kwani tunaona jinsi gani mambo yanavyoendelea, vyakula bei juu, matibabu ni matatizo, elimu ni mtihani mzito, vifaa vya ujenzi Mtume Muhammad! Baada ya Serikali kuchukua hatua ya kupunguza bei ya mafuta bado mabadiliko hayaonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsia ni neno linalohusu watu wa aina zote, yaani wanawake na wanaume na haina maana ya kuwa ni wanawake kama ambavyo baadhi yetu tunavyolitolea tafsiri. Tunaposema usawa wa kijinsia, haina maana kuwa majukumu ya familia hufanywa na jinsia zote kwa usawa. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa usawa wa kijinsia katika ngazi ya familia ni kwa wanaume au wanawake kutoa *moral support* kwa wenzao katika kazi zile ambazo wao hawazifanyi kutokana na sababu mbalimbali. Tunapokuja katika ngazi ya jamii, tunaamini kabisa kazi zote zinaweza kufanywa na jinsia zote. Kitu kikubwa ni kutoa ushirikiano unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima jamii ikubali kuachana na mfumo dume unaotenganisha kazi za jinsia hizi mbili, shughuli zote ambazo zina mwelekeo wa kujenga jamii zetu kimaendeleo ziwe ni za jinsia zote. Tunapoanza kubagua shughuli za watoto wa kike na wa kiume tunapowalea na kuwakuza, tunaendeleza yale ambayo hayatajenga jamii inayotambua umuhimu wa haya na vile vile jamii inayowajibika. *(Makofi)*

. Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imo katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, hivyo wanawake wengi wamelazimika kuwa wafuasi wa Vyama hivyo, jambo linalowapelekea kutofautiana kimwelekeo kutokana na tofauti hizo za Vyama. Kambi ya Upinzani bado tunasema tena kuwa upo umuhimu mkubwa wa kuwa na chombo huru ambacho kitawaunganisha wanawake wote bila ya kujali itikadi zao za Vyama. Inavyoelekea, Serikali hii hailitaki hili kwa kuhofia kufa kwa matawi ya wanawake ya Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifahamike kuwa chombo huru kitatoa nafasi kubwa zaidi kwa wanawake kusimama kama kundi moja lililoshikamana kwa lengo la kuwa na sauti na kauli moja katika kutetea haki za wanawake kuhusu tafiti kadhaa zinazofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais Jakaya Kikwete, kukubali wito tulioutoa mwaka 2005 wa kuwa Rais yeyote atakayechaguliwa, kutoka Chama chochote kile katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kufikiria umuhimu wa nafasi ya mwanamke kuwa Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Fedha, Waziri wa Ulinzi na nyadhifa za aina hiyo. Hivyo, Mheshimiwa Rais amewateua Mheshimiwa Zakia Meghji kuwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, nafasi ambazo zimechukuliwa na wanawake kwa mara ya kwanza tokea kupata uhuru. Nawapongeza na ninawaombea kazi njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa uzalishaji katika ngazi ya kaya na jamii kwa ujumla, mwanamke ndiye anayetoa mchango mkubwa. Aidha, mwanamke kwa mazingira ya jamii zetu za Kitanzani ndiye aliyelndikiwa mzigo wa kuilea familia, kuuguza wagonjwa na kufanya kazi ngumu za kutafuta kuni na kufuata maji mbali na pale anapoishi. Kama nilivyokwishasema hapo juu, jukumu hili kwa kiasi kikubwa hubebwa na mwanamke, sio haki kabisa na ndio sababu kubwa iliyopelekea hasa kuwa na jamii isiyowajibika, kwani sio rahisi kwa mwanamke kuwa na majukumu makubwa kama ambavyo nimeainisha hapo juu, hapo hapo akaweza kukuza jamii inayowajibika na kujihusisha kwenye maendeleo ya kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa kumekuwepo na mipango mingi ya kumwezesha mwanamke aishie katika jamii zilizo Vijijini kuwa na sauti katika utoaji wa maamuzi, lakini kwa masikitiko makubwa, hali halisi inaonyesha kuwa bado azima hiyo haijakuwa na mafanikio.

. Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kumekuwepo na lengo la kuwaendeleza kiuchumi wanawake na fedha nyingi zimekuwa zikitengwa kwa ajili hiyo. Lakini kosa ambalo limekuwa likifanyika mara zote ni kuwa Serikali imekuwa ikidhani kuwa fedha pekee ndio suluhisho la kumkwamua mwanamke. Kambi ya Upinzani inaona kwanza kabla ya kuweka fedha, jambo la kwanza ni kuwawezesha kubadilika kifikra na kubadili mwelekeo wao kwa ujumla jinsi walivyozoea na kuwafanya kuwajibika zaidi na kuweza kutawala mazingira yaliyowazunguka. Baada ya hapo, ndipo suala la mitaji litakapoingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kujiuliza ni tangu Serikali ianzishe rasmi kutoa fedha kwa ajili ya wanawake, ni kweli maendeleo ambayo yanalingana na fedha zilizotolewa yamepatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kama kweli inahitaji kuleta mabadiliko ya kweli katika jamii zetu za Kitanzania haina budi kuwa na wataalam wa kweli katika nyanja za jamii ambao watakuwa *multi-dimensional*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii vimetengewa Bajeti ndogo sana na fedha iliyotengwa asilimia kubwa ni ukarabati wa Vyuo hivyo. Kambi ya Upinzani, haioni ubaya wa hilo, ila tunaitaka Serikali ione umuhimu wa kuwaenzi Walimu/Wataalam kuwajengea mazingira mazuri ili waone kufanya kazi kwenye Vyuo hivyo si adhabu, tutakapoweza kupata wataalam kwa wingi ndipo tutaweza kujenga jamii yenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003/2004 Wizara ilitoa mafunzo ya rejea kwa mafundi 30 wa vikosi vya Ujenzi na Mafunzo ya Ufundi katika maeneo ya Mkoa wa Tanga na Dar es Salaam. Mafundi hawa walipewa elimu hii nzuri ili wajitegemee katika ujenzi wa madarasa, zahanati na hata kusaidia miradi ya maji na ujenzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Wizara iliweza kufanikisha utoaji wa elimu hii, kwanini basi isiendelee kutoa elimu hiyo Mikoa mingine na kuwatumia katika maendeleo yote na wao hawa wawe wanawajibika moja kwa moja kwa Madiwani na Wabunge wa eneo husika? Jibu la upungufu wa utekelezaji wa maendeleo hayo wahusike Wabunge, Madiwani wangekuwa ndio wa kutoa jibu na wao ndio watakaotakiwa kuhakikisha maendeleo yanayopelekwa kwenye maeneo yao yanatekelezwa na kumalizika kwa wakati uliopangwa. Hata fedha zote za mradi mzima wawe wanaangalia matumizi wakipewa nafasi ya kuhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003/2004 Wizara iliongeza michepuo miwili ya mafunzo ya Stashahada ya juu katika jinsia na maendeleo, upangaji na uendeshaji shirikishi wa miradi katika Chuo cha Tengeru. Kwa ongezeko hilo, Chuo kiliweza kupanua uwezo wake na waliweza kuongeza wanafunzi kutoka 70 hadi kufikia 230 kwa mwaka na kwa mwaka 2005/2006 Wizara ilipanga kupokea wanachuo 700 ambapo ingewezekana kabisa na kwa kuongezeka kwa kozi hizo muhimu Wizara wangepata wataalam wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunaonekana kabisa kwamba Wizara inapanga mikakati mizuri ya kuendeleza jamii, lakini kutokuwepo kwa wataalam kunafanya Wizara kukwama katika mikakati hiyo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti katika hili la kuimarisha Vyuo ili wataalam wapatikane, kwani kama kweli Serikali inaona kuna umuhimu wa kuipa maendeleo jamii nzima, ni lazima kuwe na wataalam wa kutosha ili kuepuka na mwanya wa kuzorotesha miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri, kutokana na Vyuo vingi havina wanafunzi wa kutosha, kwa hiyo, ingechagua Vyuo viwili au vitatu vikakamilika wanafunzi na walimu, baada ya kutumia *resources* chache tulizonazo kwa kusambaa. Sambamba na hatua hiyo, Serikali iongeze juhudi ya kuvitangaza Vyuo hivyo ili vieleweke kwa walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuleta maendeleo, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* vina umuhimu wa pekee. Mafunzo yanayotolewa na Vyuo hivi, yanawasaidia sana walengwa katika shughuli zao za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Kambi ya Upinzani inadhani kinachotakiwa hasa ni wahusika kuwa na uwezo wa kuweza kutambua mazingira yanayowazunguka na jinsi ya kutumia mazingira hayo kuweza kuendeleza ujuzi wake na kuinufaisha jamii husika na sio kuwa na ujuzi wa aina moja tu. Kama ni useremala, basi wasubiri mbao toka sehemu zinapotoka. Hapa bado dhana ya Vyuo hivyo itakuwa haina maana katika jamii kwa ujumla. Kimsingi tunashauri mafunzo yawafanye walengwa kuwa wabunifu *(creative).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa leo ndiye kiongozi wa kesho. Lazima tukuze watoto wetu katika misingi iliyo mizuri. Kwa hiyo, sheria zote ambazo zinawanyima watoto haki zirekebishwe na hili nilizungumza wakati nachangia katika Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba sina haja ya kurudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sera ya Watoto ambayo Serikali inataka kuitoa, mpango wa uhai, ulinzi na maendeleo ya watoto. *CSPD,* hili ni sawa lakini kwanza tuwaenzi hawa watoto. Jamii inashuhudia jinsi watoto wetu wanavyozagaa Mitaani bila ya kupata malezi mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi kuna kawaida ya kuwapeleka watoto wetu kusoma nje ya nchi hii eti kwa sababu hapa kwetu hakuna elimu. Watoto hawa tunapowapeleka huko, wanakwenda kusoma mila, tamaduni na maisha ya wale anaokuwa nao. *Video* nazo zimechukua nafasi yake juu ya makuzi ya watoto. Kanda za michezo ya ajabu, yote haya yanapelekea watoto wetu kukua kwenye makuzi yasiyo na maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuimarisha Shule zetu za Chekechea hadi Vyuo Vikuu ili watoto wetu wapate elimu nzuri hapa hapa kwetu. Kuhusu Kanda, hizo Tume ambazo zimeundwa kwa ajili ya kuangalia hivi vitu wakati havijaangaliwa na walio wengi, basi zifanye kazi yake ya kutoa yale maeneo ambayo siyo mazuri kwa itikadi na jinsi tulivyo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi zimefunguliwa kwa wingi sana hapa nchini. Lakini kitu kinachowashinda wazazi wengi kuandikisha watoto wao katika shule hizo ni malipo yake makubwa. Wwananchi wengi katika nchi hii vipato vyao ni vya chini sana. Hivyo, basi, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kukaa na wamiliki wa shule hizo kutafakari zaidi jinsi ya kuimarisha elimu yetu ili watoto wetu ambao wazazi hawana uwezo na ndio walio wengi na wao wapate elimu bora. Aidha, tunaitaka Serikali iwaangalie waelimishaji kwa ujumla katika nyanja zote ili na wao wawe kioo katika jamii na wasikie fahari katika kazi zao za uelimishaji ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zifuatazo zimekuwa ni kero kubwa katika maendeleo ya jamii kwa ujumla, hivyo basi Serikali iziangalie upya. Sheria hizo ni Sheria ya mirathi ya kimila ya mwaka 1963, imepitwa na wakati na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 nayo pia haifai tena. Kuna *White Paper* inakuja ili tuchangie: Je, hiyo *White Paper* inakuja lini? Tumechoka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi imani na upendo juu ya mtoto vimekwisha kabisa! Manyanyaso na ukatili vimekithiri! Wazazi wamekuwa viumbe wa ajabu! Hii yote inaonyesha dhahiri jinsi watu walivyochoka na kutokuwa na imani. Mikasa mingi inatokea kila siku, ukisoma gazeti unakuta hadithi za kubaka, ndoa za lazima na mambo mengi ya kikatili juu ya watoto. Mfano, mtoto alibakwa na kupigiliwa msumari wa inchi sita. Nashukuru kwamba, mhusika ameshakamatwa na kesi inaendelea. Mwingine alipigwa mpaka kufa eti kakataa kuolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto/vijana wako migodini wanafanyishwa kazi ngumu za kupasua miamba kwa baruti. Hawa hata majina wamebadilishwa, wanaitwa nyoka. Katika utekelezaji wa *MMEM* jamii imeshuhudia watoto wakienda kutafuta maji maeneo ya umbali mrefu na kubebeshwa matofali, eti wanachangia kujenga shule zao.

Je, haya sio mateso? Watoto wanachukuliwa mikononi mwa wazazi wao kwenda kufanyishwa kazi za kuuza miili yao na pato likichukuliwa na mtu mwingine, haya yote lazima yapigiwe kelele za dhati na sheria kali zitungwe ili iwe fundisho na watoto wetu wapumue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukeketaji ni unyanyasaji wa hali ya juu. Tunavishukuru vyombo vyote vilivyojitolea kupiga kelele kuhusu ukeketaji, lakini mpaka leo hii hakuna sheria wala kauli iliyotolewa na Serikali kuhusu haki ya kumlinda mwanamke. *Maputo Protocol*, haki ya kumlinda mwanamke, *Female Genital Mutilation (FGM),* Serikali inabidi ifanye umuhimu wa kuitambua ili iwe na nguvu, ifanye kazi, Serikali iwe na uwezo wa kupiga vita ukeketaji na kuwe na fungu la kushughulikia kutoa elimu kwa wanaokeketa na wanaokeketwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia bajeti ya Wizara, lakini nimeshindwa kuona fungu lililotengwa kwa ajili ya kutoa elimu hiyo. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kunionyesha katika Bajeti yake, fungu hilo liko katika namba ngapi? Inawezekana nimeshazeeka macho hayaoni!! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo yote, naiomba tena Serikali iangalie sana inapopitisha Bajeti ya Wizara hii, kwani mwaka huu wa fedha wa 2006/2007 Bajeti ni ndogo, Sh. 2,121,001,000/= zilizowekwa kwenye maendeleo, kama tunataka hayo maendeleo yapatikane ni ndogo sana hasa ukizingatia zilizo nyingi zinapelekwa kwenye ukarabati wa Vyuo. Ninaiomba Serikali mwaka wa fedha 2007/2008 waweke Bajeti ya kuridhisha ili tuondokane na umaskini na tuyaone hayo maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha haya, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza kabisa kuunga mkono hoja. Lakini suala la pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii ambayo kwa kweli ameiwakilisha kwa umahiri mkubwa. Lakini vile vile natambua mchango mkubwa wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Batilda Burian na vile vile Wataalam wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi kwanza kwa kutuongoza vizuri katika vikao vyetu, lakini vile vile kukupongeza kama Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma uliyepita na kuniachia nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza sana kwa jitihada zako kubwa za kuendelea kunisaidia na kunielimisha katika masuala mbalimbali ya kuwawakilisha wanawake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii vile vile kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na ninaendelea kuwaahidi uwakilishi wangu kwao utakuwa wa nidhamu na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo: Kwanza, napenda sana kulizungumzia suala zima la uwezeshwaji wa wanawake. Kipindi chote cha Kampeni cha Uchaguzi, lakini vile vile katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais na Ilani imeahidi wazi kabisa kwamba wanawake wa Taifa hili la Tanzania watawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi tumekaa makini kabisa kuangalia uwezeshwaji huo utakuwa wa aina gani. Nilikuwa naomba Wizara itueleze mikakati kabisa ambayo itaweza kutekelezeka ya kumwezesha mwanamke huyu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Tanzania tuko wengi na wengi wanakaa Vijijini. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona kabisa watawezeshwa kwa namna gani. Watapewa mafunzo gani? Watapewa mitaji gani? Waende Benki zipi ambazo wanawake hawa wanaweza wakakopa kwa riba nafuu?

Wanawake wanahitaji kuwezeshwa kwa kweli kwa elimu. Wanawake wengi hawana elimu mbalimbali za kuweza kutambua fursa ambazo zinaweza zikawasaidia kujiletea maendeleo yao. Wanawake wengi hawatambui hata sera ya maendeleo ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za Maendeleo ya Wanawake ni chache mno, hata Wizarani huwezi kuzipata za kutosha. Kwa hiyo, wanawake watajuaje mikakati ya maendeleo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera na mikakati mingi sana inayohusu maendeleo ya nchi yetu, lakini wanawake wengi hawajui na hawana fursa ya kuweza kutambua. Kwa hiyo, watawezaje kutambua na watawezaje kuendana na utekelezaji wa sera na mikakati hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja, atueleze kama ameweka mkakati maalum wa kupita Tanzania nzima, Mikoa yote, kuwaelimisha wanawake Sera za Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kuhusu uwezeshwaji wa wananchi na hususan wanawake kiuchumi. Wakati ambao tunategemea kuunda Benki yetu ya wanawake, ni vizuri Serikali ikatamka kabisa kwamba wanawake hao waende katika vyombo hivi vya kifedha wakakope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaendelea kujiboresha sisi wenyewe na mpaka hapo tutakapokuwa tumeunda Benki yetu, labda tutakuwa na tamko rasmi la Serikali. Lakini katika kipindi hiki cha mpito nilikuwa naishauri Serikali kwa kweli ionyeshe vyombo vya kifedha ambavyo wanawake wanaweza wakakopa kwa riba nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala la usimamizi. Wanawake wengi tunapenda kuwezeshwa katika usimamizi. Tukiwezeshwa katika elimu, tukipewa mitaji, tukisimamiwa tutafanya mambo yetu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake sisi tunategemea sana Maofisa wa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Halmashauri zetu. Mimi, wewe na Wabunge wote tunafahamu hali mbaya waliyonayo Maafisa Maendeleo ya Jamii. Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Idara zetu huko Halmashauri zetu wana hali mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nimefurahi kuona katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kuna *OC* ya Sh. 5,042,600,000/= hivi. Nina imani *OC* hiyo itapelekwa mpaka kwenye Halmashauri kwa sababu katika Idara zinazotia huruma katika Halmashauri zetu ni Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hii haina *OC* na hivi zaidi ya mshahara, Afisa Maendeleo ya Jamii haelewi afanye mradi gani, kwa pesa ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba sana Mheshimiwa Waziri anieleze kama sasa Maafisa Maendeleo wetu wa Jamii watapata *OC* ili nao wajione kama ni Idara kamili katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vile vile kuhusu usafiri. Tumeona Wizara nyingi hapa tumepitisha tunaomba magari, magari, magari. Lakini Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ya Wanawake tunaomba pikipiki. Yaani tuna hali mbaya sana kiasi kwamba kwa kweli usafiri hakuna na vile vile Maafisa Maendeleo hawawezi kutembelea hususan wale walioko Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Bajeti bado ni ndogo. Nashukuru kwa mwaka huu imeongezeka, siyo sawa na miaka iliyopita. Lakini iko haja ya kuongeza zaidi Bajeti ya Wizara hii kama Mheshimiwa Waziri, alivyosema Wizara hii ni Wizara mtambuka, kwa hiyo ina-*cut across* Wizara karibu zote. Kwa hiyo, ni vizuri wakaongezewa Bajeti na Bajeti ya Wizara hii ikawa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na *genda desk.* Neno hili la *gender desk* imekuwa kila siku tunalisikia kwamba Wizara zote ziwe na *gender desk.* Napenda kuipongeza Wizara ya Miundombinu kwa kweli, *genda desk* yao tunaiona inavyoweza kuwasaidia wanawake wajiunge katika shughuli za ujenzi wa barabara na mambo mbalimbali. Lakini Wizara nyingine *gender desk* zao zinafanya nini? Mbona hatuelewi? Mbona hatuoni? Kwa hiyo, naomba kila Wizara ituambie kama ina hiyo *gender desk.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Halmashauri zetu hazina *gender desk.* Kwa hiyo, masuala yote katika Halmashauri hayaendi kijinsia. Sisi tunapenda masuala yote kijinsia, ili wanawake na wanaume waweze kufaidi uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza vile vile masuala ya mashirika yasiyo ya kiserikali. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanafanya kazi kubwa na nzuri. Lakini utafiti wao, anaujadili nani? Je, unaingizwa katika Vikao vya Halmashauri? Je, unaingizwa katika masuala mazima ya kuzungumzia maendeleo ya nchi hii? Mimi nafikiri tungekuwa tunaingiza taarifa zao tungeweza kuona *impact* kubwa sana ambayo wananchi wa Taifa hili wanafanya kazi. Kwa hiyo, ninaomba taarifa za Mashirika yasiyo ya Kiserikali ziwekewe utaratibu maalum ili tuweze kuona kila Mtanzania anafanya kazi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi wanapenda kuwa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Lakini hawajui Kanuni wala taratibu za kuanzisha mashirika yasiyo ya kiserikali. Ninaomba Idara hii na Mkurugenzi wa Idara hii apite kuhamasisha na kueleza kanuni na taratibu za kuanzisha masharika yasiyo ya Kiserikali ili wanawake wengi waweze kumiliki mashirika yasiyo ya kiserikali. Lakini kwa kuanzia, ninamwomba aje kuanza na Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala la siku ya Wanawake Duniani. Kwa masikitiko makubwa, mwaka huu siku ya Wanawake Duniani tulikuwa hatujaadhimisha Kitaifa. Mimi ninaona siku zote za maadhimisho ya kidunia siku ya Vijana, siku ya Watoto, yanaadhimishwa kitaifa. Kwa nini siku ya Wanawake isiadhimishwe Kitaifa? *(Makofi)*

Kama Serikali inatoa pesa katika kuadhimisha siku ya Vijana, siku ya Mwenge, siku ya Watoto, hii siku ambayo inatuhusu sisi wanawake, kwa nini haiadhimishwi Kitaifa? Ninaomba siku hii iadhimishwe Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na ninawatakia kila la kheri katika jitihada zao katika kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Ruvuma, unajua jinsi wanavyojiwajibisha katika kijiletea maendeleo. Ninaomba kutoa pongezi kwa Shirika la ARUWASAKI kwa kuanzisha *SACCOS* nyingi Mkoani Ruvuma za wanawake. Lakini ninapenda kutoa pongezi za pekee kwa Shirika la *VIKOBA Sustainable Development Association* ambalo limeanzisha vikundi vingi vya Vikoba na linawasaidia sana wanawake katika Mikoa tisa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe pongezi za dhati kwa Shirika la *DMI* la Ma-*sister* walioko Songea, Ma-*sister* wa Kihindi wanafanya kazi nzuri ya kuwasaidia wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kijiunga katika vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza hawa wanawake kwa kusimamia masuala ya afya za wanawake wa Tanzania. Ninapenda kupongeza *Hansi Foundation* kwa kuwafundisha wanawake wengi waweze kuwa wanasiasa wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza *SUNNY Tanzania* kwa kutekeleza mikakati mingi ya maendeleo ya wanawake. Pamoja na pongezi hizi, napenda kuwapongeza viongozi wote wanawake walioko Tanzania na mimi ninawapenda sana kwa jinsi wanavyowajibika vizuri. Ninawatakia kila la kheri, nawapongeza Wabunge Wanawake, Madiwani Wanawake ninawapenda sana na wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wanaume wote wa Tanzania. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile na mimi nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri, kwa kweli ametoa maelezo anajiamini na ndiyo maana ameleta familia yake leo. Wamwone kwamba kweli anaweza vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile nimshukuru Naibu wake, Mheshimiwa Batilda Burian na Watendaji wote, naona wapo. Naomba watusikilize vizuri ili wamsaidie Waziri isije ikaonekana Waziri sasa hawezi kazi na tunajua Watendaji ndiyo wanaweza wakamwangusha. Sisi tunamjua Sofia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza nizungumzie hasa matatizo ya Idara ya Maendeleo ya Jamii. Mimi natoka Shinyanga. Nitazungumzia zaidi Shinyanga na najua wengine watazungumzia maeneo yao wanayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii kwa kweli ni yatima. Mimi toka nimepata Ubunge, najua hii ndiyo Idara yangu ya kufanyia kazi, kwa kweli ni yatima kama vile hawana mama wa kumsaidia. Kwanza hawana zuruku, Mheshimiwa Mbunge mwenzangu amesema na wengine watakaokuja watasema hayo. Wanapokaa Idara zote, Idara ya Elimu wana ruzuku wanapewa na Wizara yao. Idara ya Kilimo wanapewa. Wao wamekaa kama ombaomba na bahati mbaya sana wamekwenda Shule, *graduates.* Amesema Mwenyekiti wa Kamati hii hapa kwamba, Mkurugenzi hawaoni kama ni watu. Ofisi wanapewa ndogo, wako tisa, viti vitano, mtu akinyanyuka mwingine ndiyo anakaa. Kwa kweli haipendezi, watu wamekwenda Shule, viti hamna. Kila kitu hakipo. Hawaonekani kama ni watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nasikitika kwa hilo. Nasema Waziri atusikilize ili akitoka hapa kwa kweli aweze kutembelea ili aone wenzake wanavyofanya kazi kwa mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, lakini hawa viongozi hawana kabisa usafiri kama alivyosema mwenzangu. Nimeona kwenye hiki kitabu, wamesema pikipiki. Mimi sijaiona, labda kama imeingia jana. Lakini hata hiyo pikipiki yenyewe

wanapandaje watu tisa? Wako watumishi tisa, lakini kwa kawaida kabisa ilitakiwa wawe 18. Sasa tisa sijui wanafanyaje kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu hawana mafunzo yoyote na hawa watu ndio tunaowatarajia waende Vijijini wakaelezee Rais anasema Ari Mpya, Kasi Mpya, Nguvu Mpya. Wanawake wawezeshwe wa kusema ni hawa. Mwenzangu amesema, Waziri tembelea nchi nzima, Waziri hawezi. Hawa ndiyo wakujua. Wapeni magari watu waende wakawaeleze wananchi, watu wamesoma Shule hawana mahala pa kwenda wamekaa tu. Wamekuwa kama ma-*MC. (Makofi)*

Leo hii kama kuna mwenge ndio utawakuta watu wa Idara ya Maendeleo wamekwenda. Wamekwenda kufanya nini mwenge wenu? Waende wachache wengine wafanye kazi za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika Idara zote, hii Idara ndiyo inasikitisha. Idara hii haina kompyuta. Leo tunasema tuwe na vikundi, haya hivyo vikundi vipo, vinaingizwa kwenye nini? Mtandao wa sasa ni kompyuta, hawana. Wanatumia mafaili na *typewriter*. Mtu kamaliza Chuo Kikuu *typewriter* kweli Ofisini!! Hapana. Kwa kweli hii haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nataka nizungumze tena suala la Vyuo vya Wananchi. Shinyanga tuna Vyuo vinne, lakini natakielezea sana Chuo cha Buhangija ambao vinafanana na vile vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Buhangija kiko Mjini na Shinyanga mnajua ni Manispaa, kipo katikati ya Mji, Chuo hicho kwanza hakina vitendea kazi. Nimekuta gari *STG* 7538 msaada wa *SIDA* wa zamani, gari kutoka mwaka 1993, bovu. Juzi wamepeleka baiskeli tatu. Kweli baiskeli tatu kwa Mkuu wa Chuo! Chuo hiki kinahudumia Shinyanga Vijijini kinahudumia Wilaya ya Kishapu, kinahudumia na Manispaa yenyewe. Hivi baiskeli tatu mnatuletea, Kishapu mnajua ilipo? Shinyanga Vijijini mnajua ukubwa wake? Hivi mama yule Mkuu wa Chuo atoke pale na baiskeli, mnamtakia kheri kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie na nimuunge mkono huyu Kiongozi wa Upinzani. Amesema hizi hela mmezitoa, lakini hizi hela ndogo kwa kutengeneza Vyuo vyetu. Ninachosema ndogo, ni haya maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo chetu cha Buhangija kina mabweni ya wavulana na wasichana. Lakini vyumba havina hewa. Nimekwenda mimi mwenyewe, utafikiri watoto wako Magerezani. Wazazi hawaingizwi tu sehemu wanapolala wale watoto. *(Makofi)*

Nyumba ni kubwa, taa iko katikati, moja tu ndefu. Ndiyo inayotumika kwa sababu hawana *ceiling board,* madirisha yako juu utafikiri Magerezani! Hapana. Chuo gani hicho? Naomba Mheshimiwa Waziri aje akione hicho Chuo halafu atakuja kuniambia, kweli Masunga ndiyo maana alikuwa analalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyoo vyote nimevikuta vimefurika, sio nyumba za Walimu, siyo vyoo vya wanafunzi, vyoo vimefurika na nimekuta barua ya Idara ya Afya inasema Chuo chako kifungwe. Nafikiri huku nyuma kitakuwa kimefungwa. Sijapata taarifa hiyo. Lakini nataka nikupe hiyo taarifa.

Sasa twende kwenye vitanda. Vitanda viko vya toka mwaka 1955. Sijui kama mimi nivisemeje hivyo vitanda. Vile vitanda vya *spring* vya *Banko* ndiyo *double deccar* toka *Middle School* vile ndiyo wamerithi ndiyo wanalalia mpaka sasa. Nimekwenda kuona kwa macho Mheshimiwa Waziri. Godoro ni inchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwa masikitiko sana na nashukuru kwa sababu hata Mwenyekiti wa Idara hii ni wewe mwenyewe, Mwenyekiti na ndio leo unaongoza Bunge hili. Naomba wewe na Kamati yako yote muende mkaone vigodoro muwaonee huruma hawa watoto. Bafu hawana, wanaoga machakani. Maji hakuna wanakwenda kuchota kwenye visima. Hiki Chuo hakina maji, halafu mnasema kwenye kitabu *TV* zipelekwe watu waone. Waende waone wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu samani, ukienda kuona pale viti, meza, makabati, ni ya kusikitisha. Ofisi ya Mkuu wa Chuo ni mbaya, afadhali ya Afisa Mtendaji wa Kijiji, ni mzuri. *Typewriter* anachapa ile ya zamani. Mwalimu pale unamkuta hata kutembea hawezi. Anatembeaje Mwalimu Chuo chake kibaya? Hakina chochote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwachekeshe ya mwisho. Pale watumishi wako wachache, lakini Sekretari hayupo. Sasa Mkuu wa Chuo anafanya nini? Hayupo mpishi, Walimu ndio wanakwenda kuweka kuni kule ili watoto wakimaliza ndio wakale. Mlinzi hayupo. Sasa kwa kweli mimi hii inanisikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme, Mheshimiwa Waziri wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Asha Rose-Migiro alifika na akaona hali hiyo. Lakini ninachotaka kusema, kwa nini mtu anakuja anaona na barua tukaandika tarehe tisa Machi, 2004, Katibu yuko ananisikiliza, hajajibu lolote, hajaja kutuambia chochote. Hivi ile ni *Serengeti National Park?* wanakuja kuangalia na kuondoka? *(Makofi)*

Lakini ninachosema mimi, kwa Mheshimiwa Waziri Sofia na Naibu wako najua mtakuja na mimi nasema yafuatayo:- Moja, Waziri yupo tayari kutembelea Mkoa wa Shinyanga kuona Vyuo hivyo? La pili, kwa sababu hela zilizotolewa ni ndogo: Je, anaweza kusaidia hizo hela angalau zijenge Vyuo viwili ili Vyuo viwe safi halafu vingine viendelee baadaye ikiwemo na Buhangija ambayo ipo Mjini kabisa? Manispaa inatia aibu Majengo yakiwa ya udongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutafuta mfadhili atusaidie ili Chuo hicho kiwe cha kimataifa? Sasa hivi watu waende wapi kupata maelekezo? Vyuo ndio, vipo hivyo na majengo mabovu, kila kitu hovyo, havipendezi.

Kwa kweli mimi ingekuwa Mheshimiwa Waziri ana miezi hivi, ningechukua shilingi leo. Lakini kwa vile ana miezi sita, mimi ninamwaminia kazi zake. Najua atakuja na atafanya kazi. Naomba kuunga mkono hoja. Lakini mwaka kesho nitaikatalia shilingi kama hamwezi kutuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkaribisha Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mje muone Buhangija na Vyuo vingine halafu mtuletee vitu tuendelee na kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kunipa afya njema na kuweza kuchangia katika hotuba hii. Nakushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii muhimu. *(Makofi)*

Kwanza nawapongeza wapiga kura wangu walionichagua na nakipongeza Chama changu cha *CUF* kwa kuweza kunichagua mimi na hii leo kuweza kuwa Mbunge wa Bunge hili. *(Makofi)*

Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuongoza Taifa hili. Nampongeza Spika kwa kuweza kuongeza Bunge hili kwa nguvu na ari na nawapongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wake wote wawili kwa kazi zao za ufanisi. Namshukuru Waziri Mkuu kwa kazi zake na kuweza kusimamia baa la njaa na kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Namshukuru Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri wake na Watendaji wote waliomsaidia kuandaa hotuba hii nzuri. Sasa naanza kuchangia Wizara hii. Wizara hii inaitwa Maendeleo ya Jamii na Jinsia. Ni kweli jinsia zote zinahusu na Wizara hii jinsia ni wanawake, jinsia ni wanaume na watoto, wote wawe na haki sawa. *(Makofi)*

Lakini la kusikitisha, Wizara hii imepewa Bajeti ndogo ndogo kabisa, hailingani na Wizara hii, kwa sababu Wizara zote zinabebwa na Wizara hii. Vile vile, naipongeza Serikali kwa kuweza kuwashirikisha wanawake katika vyombo vya uamuzi, kufikia asilimia 30. Lakini hata hivyo tunataka ifike asilimia 50. Ndiyo itakuwa jinsia imekuwa sawa.

Lingine, naja kwenye unyanyasaji wa jinsia. Kwa kweli sisi wanawake wakati mwingine tunanyanyasika kwa vile mwanamme anakuja, anakuoa kwa furaha. Mnakaa pamoja, mnazaa watoto, bahati mbaya mwanamme yule amefariki. Akifariki tu, jamaa wa mume yule wanakuja wanakunyanyasa na wanakutoa ndani ya nyumba na wewe una watoto. Watoto wale uende nao wapi? Watoto wale wanataka kusomeshwa, watoto wale wanataka maisha bora, watoto wale wanataka malezi bora, watoto wale wanataka kuhudumiwa kiafya. Kwa kweli, huo ni moja ya unyanyasaji. Kwa hiyo, Wizara hii naiomba iangalie vizuri sheria iliyopo.

Sijamaliza kunyanyaswa kwa watoto hasa mtoto wa kike. Mtoto wa kike anapopata ujauzito, mtoto huyu hufukuzwa Shule na akifukuzwa Shule anarudi nyumbani

hana la kufanya na huko nyumbani akifika, huyo mtoto wazazi wake wanampa kipigo, wazazi wake pengine wanamfukuza anabakia kutangatanga na baadaye mtoto huyo kupata janga la UKIMWI. Mtoto huyo anapata janga la UKIMWI. Sasa sheria iangalie, anayembebesha mimba pengine ni mzee wa miaka 40 na mtoto ana miaka 15. Je, anambebesha mimba mtoto huyo na mtoto huyu anamlea katika kutangatanga. Kwa hiyo, Serikali iangalie sheria hiyo ya malezi ya mtoto.

Vilevile, watoto ni Taifa letu. Watoto hawa hubebeshwa mizigo mizito, watoto hawa hupewa ajira ambayo hawaiwezi. Utamkuta mtoto tayari anabebeshwa mawe au anabebeshwa matofali hayawezi. Lakini atafanya nini? Wazazi wake, hana pakwenda nao, kwa hiyo hilo ni moja katika kudhalilika kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Benki ya wanawake. Benki ya wanawake ianzishwe ili wanawake nao wapate kujikwamua kwenye maisha yao, waanzishe *SACCOS* na wakopeshwe pesa za kuanzisha hizo *SACCOS* ili Benki hizo nazo zipate tija ndani yake na wanawake wajikwamue katika maisha yao. Tukienda hospitali, watoto wetu wanalazwa kitanda kimoja watoto wawili, watatu na watoto hao wana magonjwa aina kwa aina. Wale wanaharisha, wale wana magonjwa ya kuambukiza, vitanda ni vichafu, nguo zao ni chafu, sasa watafanya nini? Watoto hawa suluhisho lao ni kufa au kuthaminika. Kwa hiyo, Wizara hii iangalie kwa wazi tatizo, wapatiwe mahosptali, kama wao ni Wizara yao ya Jamii, waende mashuleni waangalie vikalio wanavyokalia, watoto wengi wanakaa chini, hata mtoto akivalishwa nguo safi, akifika nguo zote zimechafuka. Hivyo Wizara hii ina haki ya kuliangali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto yatima wana haki ya kuangaliwa kama watoto waliokuwa na baba zao, kwa sababu Serikali na Wizara hii ni sawasawa na baba. Kwa hiyo, iwashughulikie watoto hawa. Tulikwenda kituo kimoja kuangalia watoto hawa Dar es Salaam. Tulipofika, wanaoshughulikia watoto hao ni watu wawili na watoto hao sio chini ya watoto 50. Kwa hiyo, Wizara hii ifanye kila hali iwashughulikie watoto hawa. Naishukuru Wizara hii na naiomba heri, naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Jinsia, Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Kusini Pemba, napenda kuchangia hotuba ya Wizara yetu hii, Wizara mama. Kabla ya kuchangia, kwanza napenda kumpongeza ama kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteua ma-*DC* wa Wilaya mbalimbali wapya wakiwemo wanawake na vijana. Tunajua kwamba wanawake na vijana tunaweza, tunawaomba wanawake na vijana hao wasije wakatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupongeza, napenda kuishukuru sana Serikali, ama napenda kuishukuru Wizara hii. Napenda kumshukuru Waziri Mheshimiwa Sophia Simba, napenda kumshukuru pia, na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr.

Batilda Salha Burian, mama shangazi huyu, kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya na kutayarisha hotuba hii ambayo kwa kweli inatupa moyo hasa sisi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia, nisije nikasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, nakwenda moja kwa moja kwenye *points.* Kwanza *point* yangu ya kwanza inakwenda kwenye ufinyu wa fedha za Bajeti za Wizara hii. Hii Wizara kama tunavyosema kwamba Wizara hii ni mama, Wizara kubwa inajumuisha watu wote jinsia zote na mambo yote, inakuwajekuwaje kila mara hii Wizara inatengewa Bajeti ndogo kama hivi? Hivi kweli tunataka maendeleo kweli ya jinsia? Mimi siamini. Nafikiri tunasema tu hapa, tunataka maendeleo kweli kama Wizara inawekewa fedha kidogo kama hivi, eti Shilingi bilioni 10! Shilingi Bilioni 10 ifanye nini? Mimi naomba hii iwe mara ya mwisho.

Bajeti inayokuja Wizara hii itengewe fedha nyingi kuliko Wizara zote hapa, kwa sababu mimi naifahamu hii Wizara inashughulikia wanawake, wanaume, watoto, walemavu, vijana kila kitu kinashughulikiwa na Wizara hii. Leo, nashangaa, Wizara hii inapewa Shilingi bilioni 10. Ifanye nini? Pesa nyingi hizo zinakwenda kwenye mambo ya Menejimenti, haiendi kwenye mambo ya mikopo na mambo mengine mengine ambayo itawezeshwa wananchi kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni fedha za maendeleo ambazo tuliambiwa hata kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, ilizungumzwa hapa kwamba kutatolewa Shilingi milioni 500 kila Mkoa ambazo zitatayarishwa kupelekwa katika mabenki tofauti ili wananchi wapate mikopo ili iwasaidie.

Mimi napenda kuuliza kupitia hii Wizara, hizi milioni zilitengwa, ambazo zitakwenda katika Mikoa mbalimbali, mabenki mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania: Je, Zanzibar imo? Kama haimo, nije nijibiwe hapa, kwanini isiwemo? Mimi napendekeza hizi Shilingi milioni 500 ambazo zitakwenda katika Mikoa ya Tanzania na Zanzibar, ikiwemo Pemba tukiwemo na sisi wanawake wa kule na vijana na wao ni maskini kama wanawake na vijana wa Tanzania yote. Tunaomba hilo liwemo. Kama halijatayarishwa, hilo naomba liwemo, hizi Shilingi milioni 500 zinazokwenda na sisi Zanzibar tuwekewe fungu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwenye mikopo ya wanawake, wanawake, wanawake kila siku wanawake, wanawake ni maskini, wanawake ni watendaji wakubwa katika nchi hii, lakini wao ndio wanaachwa nyuma katika maendeleo, wanawake ni wakulima wakubwa katika nchi hii, wanawake ni wafanyabiashara, wanawake ni walezi, wazazi walezi wa watoto na walezi wa mababu humo majumbani. Unamlea mtoto asubuhi na usiku unamlea baba, lakini tatizo hatuhurumiwi sisi wanawake! Hatupatiwi mikopo, hasa wanawake wa Vijijini hawapatiwi mikopo! Tunaambiwa tu mikopo, mikopo, wanaisikia tu mikopo kwenye redio, sio kweli, hawapatiwi mikopo. Kama wanapatiwa, hawapatiwi elimu ya mikopo, na kama mwanamke hujampatia elimu ya mikopo, hawezi kuendeleza mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke wa Kijiji ukamchukue huku umpe mkopo, hata kama wa milioni na wala hawapewi kama hizo, wanapewa vilaki laki tu. Unampa mkopo, lakini humpi elimu ya mkopo; tunaomba Maafisa wa Wizara hii waende Vijijini kuelimisha jamii, kuhusiana na mambo ya mikopo hasa wanawake hapo ndio wanawake watafanya miradi yao mizuri na watajikwamua kimaendeleo. Lakini tusibakie kwenye makaratasi tu kila siku mikopo, mikopo wala haiwafikii na hata ikiwafikia elimu hawapati ya mikopo. Wapate elimu ya kuendeleza mikopo na wapate elimu ya kutafuta masoko ya bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabenki mengi yanatoa mikopo. *CRDB* tunaona, *NMB*, kama kule *PDZ* lakini riba ni kubwa. Naomba mikopo ya wanawake ipunguzwe riba. Mwanamke hana uwezo wa kulipa riba kubwa kama hizo ambazo wanaziweka. Tunaomba tuweke Benki yetu basi ya wanawake, kila siku isiwe tu kwenye makaratasi, kila siku Benki itaanzishwa, itaanzishwa, hatuioni, nasema mwisho uwe mwaka huu. Mwaka unaokuja tunaiona Benki ya Wanawake au la sivyo, tutakuja kukamata Shilingi hapa hapa. Hatutaoneana huruma hapa, urafiki utaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wajane, wenzangu wengu wamezungumza kuhusu wanawake wajane, hivyo sisi wanawake tumekosa nini? Kwanini tuolewe, tupendwe, halafu mtu mume wake akifa familia zile za mume zitunyanyase? Kwa nini wanawake wa Tanzania tunanyanyasika? Hatupati urithi; wanawake wa Tanzania wajane, wakifuatilia urithi wa waume zao hawapatiwi na hata wakipatiwa kwa kweli wanapata kazi kubwa sana na wakipata huo urithi unagawanywa mpaka kwa familia; mara mtu akiachwa anafukuzwa katika nyumba, kama wenzangu pale Mheshimiwa Kadika, alivyosema, mwanamke anafukuzwa katika nyumba. Hivi huyu mwanamke anakuwa mzuri akiwa na mume wake tu! Mume wake akiondoka, familia inamtenga, kwanini?

Mimi naomba familia zijirekebishe na Wizara hii itoe elimu kwa jamii kuhusiana na masuala haya ya wanawake wajane. Naomba sana sheria ambazo zinamnyanyasa mwanamke katika mambo ya urithi zirekebishwe, tuletewe hapa sisi tuzirekebishe, tutunge sheria mpya, lakini sasa hivi wanawake wajane, wananyanyasika. Naomba hili lichukuliwe na nije nijibiwe wakati Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwa wanawake na tatizo la ukeketwaji. Kuna kabila nyingine, wanakeketa wanawake. Hivyo Mwenyezi Mungu alivyomuumba mwanamke akampa maumbile yake yote, alifanya makosa? Mimi nauliza, mwanamke kapewa maumbile, maumbile ambayo yanamfanya mwanamke huyo aishi vizuri na akiolewa aishi kwa raha mstarehe na mume wake. Kwa sababu hizo sehemu zinazotolewa ndio zinazoleta hisia ya uke na huyo mwanamke anahitajika azae na ndio wanawake tunapozaa tunapata watoto, ndio jamii inaendelea. Leo inakuwaje? Mtu maumbile yake aliyoumbwa na Mwenyezi Mungu unakwenda kuyatoa yote, yaani inauma, inauma, nakaribia kulia! Haiwezekani! Serikali haijachukua hatua bado. Bado inalegalega kwenye suala hili. Elimu bado haijatolewa, hivyo hivyo vibibi vikongwe na

hivi vibabu vikongwe, maana yake ni sisi wanawake ndio wanakeketa watoto wetu. *(Makofi)*

Mimi nasema, wanawake huko Vijijini mnaokeketa watoto wenu nakwambieni, hiyo ni dhambi. Mwenyezi Mungu hajataka hivyo. Unamfanya mtoto wa kike ajione mnyonge. Mtoto wa kike hataki kukeketwa, lakini inabidi umchukue kwa nguvu unamkeketa, kwanini unamtoa maumbile yake? Mwenyezi Mungu kakosea? Mwenyezi Mungu hajakosea, jikeketeni wenyewe basi. Unajua katika kukeketa kunaleta athari kubwa sana kwa mtoto na hapo anapoolewa hana hamu yoyote na yule mume wake. Kuna hamu gani? Nani asiyejua hizo sehemu zinazotolewa ndio sehemu nyeti za kuleta raha na kila kitu kwa mwanamke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakataa sisi wanawake, nakataa mambo ya ukeketwaji, yakome, elimu ifike Vijijini. Athari ya mwanamke kukeketwa, wakati anapojifungua jamani si tunaona jinsi wanavyopata taabu hawa? Wanakufa! Damu zinawatoka mpaka wanakufa, kwa sababu ile sehemu haipo ya kuwezesha mtoto atoke kirahisi, jamani ni vibaya. Kama wako wenzangu wa makabila hayo, naomba mnisamehe. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini kwa kweli lazima hili jambo tuliseme, kwa sababu Mwenyezi Mungu akifanya jambo, anafanya kwa kutaka yeye mwenyewe na kaliweka hilo jambo na akiliweka yeye mwenyewe Mwenyezi Mungu usiliondoe wewe. Wewe una uwezo gani wa kumpinga Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni watoto yatima. Katika Taifa letu la Tanzania kuna watoto yatima wengi sana. Wengi tunawaona mabarabarani, maskini unawaonea huruma, lakini wakiombaomba wakihangaika hawana elimu, watoto wanadhalilika, ukiwaona kama sisi ni akina mama tunalia na wale watoto, lakini hatuna uwezo wa kuwasaidia, hata ukimpa Sh.10,000/=, ukampa huyu Sh. 2,000/=, Sh.1,000/= utawamaliza? Wako wengi. Naiomba sana jamii, iwatunze watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kwamba mayatima ni wale ambao waliondokewa na wazazi wao kwa ugonjwa wa UKIMWI. Mayatima wote, tuwalinde sisi majumbani mwetu. Sio kila siku tunawapeleka kwenye Vituo vya kulelea jamani. Ni vizuri Serikali ina vituo vingi vya kulelea mayatima lakini tujenge hisia kwamba sisi wenyewe jamii tuwalinde wale watoto, tuwatunze ili wale watoto waje wawe raia wema. Watoto wakitunzwa kwa pamoja kwenye ma-*group* kama hayo hawana kwa kweli malezi ya familia. Familia tuwe na imani na watoto hawa yatima jamani, hawakutaka wao kuondokewa na wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma sana. Kwanini iwe hivi? Nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya amani, ni nchi ya utulivu, ni nchi ya upendo, lakini mimi nashukuru sana kule kwetu Zanzibar, watoto yatima wanalelewa tu na familia, wanatunzwa vizuri, lakini huku Bara jamani hakuna imani hiyo. Naomba sana tusiwatenge watoto yatima na wala tusiwanyanyapae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wanawake na gonjwa la UKIMWI. Sisi wanawake ndio waathirikaji wakubwa wa janga hili la UKIMWI kwa maumbile yetu. Kwa sababu UKIMWI unaweza ukapatikana kwa njia nyingi, lakini kubwa tunaloambiwa ni hilo ambalo tunalijua. Kila mtu analijua hili. Elimu bado haijasambazwa. Mwenyezi Mungu katuletea haya maradhi, hatujui kwa maana gani, pengine tulimkosea, au hatuwezi kujua, ni mambo ya Mwenyezi Mungu. Maradhi yako mengi, *TB*, Malaria, maana yake Malaria nayo kali, kuliko hata maradhi mengine. Lakini hili gonjwa nalo sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iendelee kuelimisha wanawake, na mambo haya mengi yanapatikana kwa lile nililolizungumza la ukeketwaji. Mtu huyu kiwembe hiki kakeketwa huyu, kaja kakeketwa huyu hata maji ya moto hakioshwi na wadudu wa UKIMWI hawafi, anakuja kukeketwa mwingine na mambo mengine ndio nilishayasema , hayo mengine tupunguze ama tuache kabisa. Wanawake tujitahidi kujilinda, sisi wanawake tujitahidi kujilinda na vilevile Serikali itusaidie katika kutoa elimu kuhusu suala hili la UKIMWI na pindi mwenzetu hata sio mwanamke wala sio mwanaume, mtu yoyote kwa sababu hata mtoto mdogo anaweza kuwa UKIMWI, lakini mtu yoyote akipata akishaathirika, tusimtenge, tusimwone kama yeye kakosea, au pengine yeye kamkufuru Mungu au hivyo na hivyo.

Ni kweli, lakini haya maradhi hayachagui. Pengine wewe unamcheka mwenzako, wewe hujaenda kupima, unamcheka mwenzako nini? Umekwenda kupima? Kwa hiyo, mimi naomba wanawake walioathirika na gonjwa hili la UKIMWI tuwapende, tuwapende kama wenzetu, tuwasaidie na tuwape elimu na tuwape misaada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeki, la mwisho ambalo limenikera sana ni tatizo hili la usafiri kwa watoto wetu, wanafunzi wetu hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Hili linakwenda huku kwenye Wizara hii ya wanawake kwa sababu ndio jinsia. Watoto wetu hasa wa kike wananyanyaswa kwa usafiri, madaladala. Makodakta na madereva wanawanyanyasa watoto wetu. Nilikuwa nichangie kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, lakini ilinipita, muda ulikuwa mdogo.

Kwa hiyo, nalizungumzia hapa. Wizara hii ishughulikie suala hili ikishirikiana na Wizara nyingine, watoto wetu hasa wa kike wanaanzia kuharibikia hapo. Mtoto anapanda daladala anatolewa, anapigwa anakwenda kutafuta *lift*. *Lift* wanaijua? *Lift* siku ya kwanza *lift*, siku ya pili *lift*, siku ya tatu liftli, mtoto keshaharibika. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifuatilie suala hili wawekewe kama ni magari yao maalum, au uwepo mpango wowote wa Serikali, lakini watoto wanaharibika sana kutokana na unyanyasaji wa usafiri. Naomba sana, watoto ni wetu sote, tusijione wengine hapa tuna watoto wanapelekwa kwa magari ya mababa zao na mama zao, kuna watoto wa kimaskini wanateseka mabarabarani, wengine mpaka saa tano za usiku hawajarudi nyumbani. Tunasema nasema kwa uchungu mkubwa, Serikali ilione hili watoto wetu wapatiwe usafiri wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Faida. Kwa kweli ya leo kali, haijapata kutokea. Ya leo kali kabisa!

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Mheshimwa Ania Chaurembo, lakini Mheshimiwa Maria Hewa kwa kuwa amesharudi ukumbini, akishamaliza Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Maria Hewa ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, ninaona kwamba tuna mchanganyiko wa Waheshimiwa Wabunge, wanaume, maana yake leo ni jinsia, baada ya hapo taomba mniruhusu niingize na jinsia ya kiume ili kuweka ule uwiano wa jinsia. Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Maria Hewa, halafu muda ukituruhusu tuingize jinsia ya kiume kusudi tuweke ule usawa wa kijinsia.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hoja ya Wizara ya Jamii, Jinsia na Maendeleo ya Watoto. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri mama yetu Sophia Simba, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Buriani, pamoja na Maofisa wote wa Wizara hii walioshiriki katika kutekeleza hotuba hii kwetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza kabisa najikita katika suala zima la mzigo mzito ambao wanaupata wakina mama. Asilimia 90 na asilimia 44 ya Mijini na 90 inaonyesha jinsi gani wanawake wa Mijini na Vijijini wanavyoshiriki katika kuchangia maendeleo ya Taifa hili na katika kuchangia kipato cha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sana wanawake. Kwanza waliokuwepo Vijijini. Wanawake waliokuwepo vijijini wana mzigo mzito sana. Tunasema tunataka kumpa maendeleo mwanamke, lakini wa Mjini sawa tuko Mjini, maendeleo tunayapata kwa kiasi fulani, lakini mimi naamini kabisa wanawake wa Vijijini bado hawajanufaika na Wizara hii ya Maendeleo ya Wanawake. Nasema hivyo kwa sababu mwanamke muda wote anakuwa na masaa mengi katika kutekeleza siku yake nzima katika majukumu yake katika jamii. Anachukua masaa karibu 18 katika kufanya kazi ya kilimo, kutafuta maji masafa marefu, kutafuta nishati ya kuni masafa marefu na hatimaye kurudi nyumbani kushughulikia watoto wetu.

Sasa sijui muda unapatikana wapi kwa mama huyu katika kujiletea maendeleo angalau kwa kufanya biashara ndogo ndogo wakati anachukua zaidi ya masaa matatu kufuata maji tu kwa siku moja na anakuja kwa ndoo moja. Matokeo yake tunapiga kelele, tunaandika vitabu vingi na tunaleta taarifa nyingi, lakini bado hazimsaidii mwanamke wa Kijijini. Tunaomba Wizara hii iangalie upya utaratibu gani utawasaidia akina mama, lakini pamoja na kuwapa elimu kina baba ambao wengi wao wanakwenda katika ulevi na wengi wao wanakaa kucheza bao, lakini kazi zote zinakuwa za akina mama. Elimu hii itasaidia. Ukimwelewesha mwanaume jukumu lake ni nini, nafikiri watasaidia hawa akina mama.

Lakini suala lingine nililokuwa nataka kuzungumzia ni miradi katika Halmashauri. Miradi yote ya akina mama inaelekezwa katika Halmashauri na katika

Halmashauri zetu nataka nimfahamishe Waziri na naomba anisikilize kwa makini. Kuna Ubaguzi ambao unafanywa katika kutoa miradi ya akina mama katika baadhi ya Halmashauri. Ubaguzi huo unakuja pale ambapo fungu la fedha linapelekwa katika Halmashauri kuwasaidia akina mama. Mwanamke akienda pale, anaulizwa yeye anatoka Chama gani? Mheshimiwa Waziri lazima muelewe sasa tuko katika Mfumo wa Vyama Vingi na waeleshwe Watendaji wetu kwamba mikopo hiyo iliyokuja haikutoka katika Chama Tawala, imekuja kwa ajili ya wananchi wote waliokuwa na Vyama na wasiokuwa na Vyama.

Kwa hiyo, wanawake wapate haki yao ya msingi ya kukopa. Kuna matatizo ambayo yamejitokeza katika Mkoa wa Dar es Salaam na nitamwomba Mheshimiwa Waziri tukirudi Dar es Salaam, tufanye ziara katika baadhi ya maeneo athibitishe usemi wangu. *(Makofi)*

Kuna watu wamejiweka katika vikundi na tayari wamekwenda kupitia Serikali ya Mtaa na hatimaye Kata ili kupata ufafanuzi, jinsi gani wapate mikopo hiyo. Lakini kwa sababu tu ya itikadi zao, wamekosa haki ya kupata mikopo hiyo. Hii ni aibu kubwa na fedheha kubwa na ni kashfa kubwa na uonevu mkubwa ambao wanafanyiwa baadhi wanawake ambao hawapo katika Vyama au wanaitikadi ya Vyama vingine, kinyume na Chama Tawala. Nataka suala hili liangaliwe kwa undani kabisa. *(Makofi)*

Tuangalie upya, jinsi gani ya kuwasaidia akina mama hawa kwa kuwapa elimu. Tatizo kubwa ni elimu. Akina mama tunasema tunawapa elimu, lakini ukiangalia huko chini, jamani hawa akina mama hawana elimu na ndio maana unakuta mtu anakopeshwa Sh. 50,000/= na akishakukopeshwa baada ya wiki tatu, anakuja kuchukuliwa godoro, kitanda, mto wake wa kulalia, kwa hiyo hii ni udhalilishaji mkubwa. Badala ya kuwasaidia akina mama inakuwa tunawadhalilisha.

Tunaomba Wizara hii iweke mikakati jinsi gani hasa ya kuwafikia walengwa kwa elimu na awape majaribio bila kuwapa pesa kwanza. Mitihani ya kufanya kuona jinsi gani atafanya biashara na kurudisha. Lakini mnawapa elimu ya kijuu juu, matokeo yake mnawadhalilisha akina mama. Wakati umefika sasa wa kupewa mikopo mikubwa kinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa wanawake, mimi nina mashaka kidogo, nikiangalia katika kitabu hapa naona Wizara hii inatoa Shilingi milioni nne kila Halmashauri. Jamani Shilingi milioni nne ni pesa ndogo sana. Sasa Halmashauri, Shilingi milioni nne ni wanawake wangapi wako katika Halmashauri wanazihitaji hizo pesa? Matokeo yake ni kikundi cha watu wachache ndio kinachofaidika na mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya Bajeti hii. Ni finyu kama wenzangu wanavyosema, Bajeti inayokuja ihakikishe Wizara hii inapewa fungu kubwa ili kuwasaidia akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusu watu ambao wanachukua wasichana Vijijini na kuwaleta Mjini kuwafundisha ukahaba, tatizo

hili limejitokeza na watoto wetu, ndugu zetu, jamaa na watoto wengi tumewakuta wakidhalilika katika adha ya Jiji la Dar es Salaam. Watoto wanafanya vitendo vya ngono katika makaburi, hii ni aibu kubwa. Tunaiomba Wizara ishirikiane na Taasisi ya vyombo vya sheria, usalama wa raia, jamani makaburini kuwekwe ulinzi. Ile ni sehemu ambayo watu wamehifadhiwa, lakini sio sehemu ya kwenda kufanya mambo ya uzalilishaji.

Hili ni tatizo limekuwa sugu kabisa katika Jiji la Dar es Salaam na vilevile watoto wetu hawa wanapata maradhi ya UKIMWI kwa sababu mtu anachagua kutoa pesa nyingi au kidogo, pesa kidogo na *condom* pesa nyingi bila *condom*. Sasa wakati mwingine mtoto wa kike kashaathirika, anaamua kutoa tamko hilo kwa mteja wake ili apate zaidi sasa akifa ni hiari yake, kwa sababu yeye tayari kashapata uchungu wa kutolewa kule na kudanganywa kuwa Mjini kuna maisha mazuri na baadaye akaingizwa katika wimbi hilo ovu na matokeo yake anakuwa na hasira ya kusambaza ugonjwa. Tutaimba tu janga la UKIMWI, lakini kwa kweli hatutafikia muafaka kwa sababu watoto wengi ni wadogo na wanasema: sifi peke yangu, abiria wangu wawe basi zima na wengine wamesimama. Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, vilevile nilikuwa nataka kuzungumzia suala la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Watoto hawa kuna baadhi ya wananchi hasa katika Jiji la Dar es Salaam kuwalea kwa nia nzuri tu ya kuwasaidia, jamani watoto wale lakini kuna matamko mbalimbali yametolewa kwamba Vituo hivi baadhi yao vinataka kufungwa. Lakini mimi nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi: Je, wamefanya utafiti kiasi gani kabla ya kufunga Vituo ambavyo vinalea watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu na watoto yatima na wengine siyo yatima wana wazazi wao? Kwa sababu ni maskini, wanashindwa maisha, wanaingia Mijini kuombaomba.

Vilevile, naomba Serikali itengeneze basi vituo vya kukidhi kukusanya watoto na kuwaweka pamoja kwa sababu inaonekana Serikali mpaka sasa hivi bado haijaamua kutangeneza vituo ambavyo vitalea watoto hawa. Kwa hiyo, bado nashauri wawasaidie wale akina mama au akina baba ambao wamejitolea wanalea watoto. Mtu anajitolea kulea mtoto kwa imani yake, lakini hana uwezo wa kulisha watoto 50, anategemea misaada ya raia wengine wampelekee ili watoto wale wajikimu na mambo muhimu kwa mfano chakula, elimu na mambo mengine. Kwa hiyo, Vituo hivi vipitiwe vyote na Serikali, mimi naamini kabisa haishindwi kujenga Shule kubwa za kuweka watoto hawa pamoja badala ya kuwa wanahangaikahangaika.

Lakini Mheshimiwa Waziri, kitu kingine ambacho nilikuwa naomba nipate ufafanuzi, kuna baadhi ya *NGOs* ambazo hupata ruzuku kutoka kwa wafadhili, kwa mfano vifaa au fedha ambazo wanasema wanawasaidia wanawake na kuna wakati Serikali ilisema kwamba *NGOs* hizi hazitoi taarifa ni Vituo gani au ni wanawake wa aina gani ambao wamepata fedha hizi. Sasa nataka kujua toka wakati huo mpaka sasa hivi: Je, Wizara imepata taarifa yoyote au kuna *NGOs* ngapi mpaka sasa hivi ambazo zinatoa taarifa za za misaada ambayo inapata kwa ajili ya kuwasaidia akina mama?

Kitu kingine vilevile nilikuwa nataka kujua katika sera nakumbuka mimi mwenyewe nilipokuwa Mkurugenzi wa wanawake tuliitwa Wizarani, kuna chombo cha Wanawake ambacho kinataka kutengenezwa ambacho sio cha kisiasa wala sio cha Serikali ambacho kitahusisha watu mbalimbali ili kufuatilia shughuli za Vyama vya Siasa na Mashirika ya Jumuiya za wanawake kwa lengo la kupeleka taarifa katika Serikali na sasa nataka kuuliza chombo hiki kimefikia wapi na kama kimeshaanza kazi nilikuwa nataka ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia hasa kwa leo ni suala zima la kisiasa. Tumeingia katika mfumo wa Vyama Vingi sasa hivi, bado wanawake hawajapewa elimu ya siasa, wanawake wanakuwa hawajiamini, wanakuwa waoga, anaona akiingia Chama cha Siasa ambacho sicho kinachotawala inakuwa ni tatizo kwake.

Kwa hiyo, tunaomba Wizara hii kwa sababu ndiyo Wizara ya Wanawake, basi ielimishe wanawake umuhimu wa kujiunga na Vyama vya Siasa ambavyo wenyewe wanavipenda, Wizara hii ndiyo ifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara hii muhimu sana kwa wanawake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ania Chaurembo. Baada ya Mheshimiwa Ania Chaurembo, naomba nimwite Mheshimiwa Hewa, halafu kwa dakika chache zozote zitakazobakia Mheshimiwa Keenja atachangia ili ku-*balance* ile jinsia ya siku yetu ya leo.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natafuta wapi nisimame. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru tu kwa kuniruhusu niweze kuongea ndani ya Ukumbi huu wa Bunge suala zima linalohusu Wizara ya Maendeleo ya Wanawake Jinsia na Watoto katika kuchangia siku ya leo.

Lingine, napenda tu kuendelea kuwapongeza Waheshimiwa waliochaguliwa kuwa Mawaziri katika Wizara hii, wanawake wote hawa wawili nadhani wanafaa, siyo nadhani ni kwamba wanafaa. Nasema wanafaa kabisa kwamba wanastahili yao kuibeba Wizara hii ili waweze kutufikisha mahali tunakoelekea katika miaka mitano au kumi na kuendelea. Sera ya Chama cha Mapinduzi ni miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hotuba hii kwa maana ya asilimia mia, ni lazima ipite tu leo jioni. Itapita tu msiwe na hofu, itapita. Lakini mturuhusu tu tudodose kidogo ili kusudi kesho na kesho kutwa kama sio katika Bajeti hii, basi kipindi kijacho muweze kuyafanyia kazi masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayazungumza. Tuna nia ya kuiendeleza nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii wanaochangia wengi ni wanawake, kwa nini? Wizara hii siyo ya Wanawake tu, kuna jinsia. Tunaposema jinsia, wanaume mbona

hamsimami kutuunga mkono? Inapozungumzwa maendeleo ya wanawake, sasa watu wanaweka hapo *full stop,* ni koma, tunaendelea jinsia na dume limo na watoto. Au mnataka tuiweke iwe Wizara ya Maendeleo ya Jamii *full stop.* Hatutaki hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninavyoona hivi tangu tuanze kusimama, nimesimama mimi sasa, bahati mbaya nilitoka kidogo, hivi amesimama dume nani? Amesimama mwanaume? Jamani siyo ya wanawake, kuna jinsia, wanaume muelewe hii Wizara sio ya wanawake tu, naomba tuungane nanyi wanaume, mtuunge mkono wanawake jinsia mmo na watoto ndiyo mnaowazaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendelee. Nilikuwa na hoja ya kwanza kabisa niongelee masuala ya ukeketaji. Lakini ukeketaji umeongelewa na Mzanzibari *original,* sitaki kuendelea mumshangilie tu mama wa watu, yeye ameongelea vizuri suala zima la ukeketaji sitaki nilirudie.

Mimi ninaanza na suala la Mafisa Maendeleo ya Jamii. Niombe wote jamani muangalie kati ya ukurasa wa 12 na wa 14 katika hiki alichokisoma Mheshimiwa Waziri. Kinaongelea masuala mazima ya Maafisa Maendeleo katika kitabu hiki au katika hoja hii, au katika hotuba hii, kwamba Maafisa Maendeleo hawa hawapokelewi vizuri na Halmashauri.

Vivyo hivyo wanaendelea kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa hawapokelewi vizuri na Wizara. Naomba msome tu kuanzia ukurasa wa 12. Wanasema, Maafisa Maendeleo ya Jamii hawatoshi. Hawa watumishi hivi mbona tunacheza nao kama vile wenyewe hawakwenda Shuleni jamani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hetu tuwaone hawa watu kama walikwenda Shuleni wanapoajiriwa wanakwenda kwenye Halmashauri wanasemwa, Wizara hawana mawasiliano ya moja kwa moja imeandikwa humu. Halmashauri hawawapokei vizuri wanalalamika, Kamati na Wizara hawana mawasiliano ya moja kwa moja imeandika humu katika kitabu. Hivi na uchache wao Halmshauri haiwapokei, ni wachache, wafanye nini hawa watu? Hii Wizara ifutwe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa hoja kabisa moja kwa moja, hawa nao walikwenda Shule jamani wakiwa wanajua Wizara hii ni ya muhimu. Naomba Halmashauri iwapokee. Kama ndiyo mmewaweka kwenye Halmashauri, naomba kama kuna mawasiliano ya Wizara wapokelewe na niombe kwamba wawe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mwanza, unakuta wanaita Ma – *CDA,* Kingereza hicho! Yaani *Community Development.* Sasa katika haya, naomba hewala tusitafute kutafsiri, hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii sisi Mwanza unakuta Mtendaji mmoja, yaani huyu Afisa anapewa Kata mbili ndiyo za mwisho, lakini ana Kata tatu na ana Kata nne, atafanya nini? Kesho anaambiwa hana mahusiano mazuri na Halmashauri na wala Wizara haimpokei na bado anapewa pikipiki, unasema nini juu ya hili? Tukubaliane leo katika Bunge hili hawa watu wazalishwe wawe wengi watufae katika nchi hii kama kweli hii Wizara inataka itoke mahali ilipo si wanachuo wapo?!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe hawa watu wasije wakanyanyasika katika Halmashauri zao na Wizara iwapokee na niombe kabisa kwamba, kila kitu kilichopo na wote wakubaliane wawe wengi, tupate wataalam walio wengi *so long as* kuna *Institute* ambayo inawatoa hawa Maafisa waweze kuwa wengi wa kutosha kutuletea maendeleo ndani ya Wizara hii, vinginevyo tutaimba nani atatuongoza? Tutaendelea kuwa duni tu ndani ya Wizara hii na hivi ndiyo ndani ya wanawake maana walio wengi humu wanadhani hii Wizara ya wanawake tu kumbe na madume yamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda la pili, nalo ni suala la *FDC* hizi yaani, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, mwaka 2005 mimi nilizunguka katika Mkoa wa Mwanza nikiwa na Waziri aliyekuwepo kipindi kile. Jamani Vyuo hivi vimeshakwisha, lakini nimeona kwenye vitabu mnasema waliomo humu wanafunzi wabebe *tender,* mimi ninakubaliana nayo asilima mia kwa mia maana kweli tunakaribisha watu wenye utaalamu humu, lakini kuna Vyuo kwa mfano kwetu Mwanza Malya wako karibu kabisa na Chuo cha Ufundi, Wazanzibar wanajua nikizungumza hivyo. Magereza, hivi kwa nini tusitumie Magereza hao ambao wako karibu wakafanya shughuli za kuboresha haya maeneo, yaani wakawatumia wataalam waliomo ndani ya hayo maeneo wakaja wakaboresha maeneo haya yakawa mazuri tu. Si ni ubunifu mnasema! Watoke huko waweze kwenda kutoa ufundi wao, maana watu hawa wanachohitaji ni chakula tu, wanahitaji nini pale? Tutumie maeneo haya kuboresha maeneo haya ambayo wako karibu ili haya maeneo yawe mazuri.

Mimi nimelizungumza hilo na nitaona kama kweli mmelipokea au hamkulipokea, lakini hawa wenzetu ambao wako kwenye Vyuo vya Mafunzo kwa nini wasifanye mambo ya utalaam katika maeneo ya *FDC*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake jamani tumesoma humo kwenye kitabu, kuna michakato, itatoka michakato kutakuja Mkakati, wakitoka mkakati, watakuja tunaboresha, yaani viswahili vinaongoza! Naomba tuviache hivi viswahili kama mchakato, kuboresha, mikakati, ufunguzi na kadhalika.

**MBUNGE FULANI:** Mkurabita.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Unaona, wananipa wenyewe na Mkurabita. Niombe jamani, hebu achaneni viswahili, kweli fungueni Benki za Wanawake, wanawake wapo, tumewaambia jiungeni kwenye vikundi na wameshajiunga, leo wanawake wanajua kila kitu, sasa mnasema kuna mchakato. Kwanza neno hili mchakato, Kiswahili gani kinaeleweka Usukumani hicho? Naomba hayo masuala yaishe, leteni Benki tuone na tufeli wenyewe wanawake mahali tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, madanguro haya yameanza kusambaratishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ndio! Kwamba hataki. Sasa, kama hataki wameshasambaratishwa hawa watoto? Nani kawadaka hawa watoto ili kusudi baadaye wawe katika maadili mazuri? *Iam saying this* tukubaliane, vinginevyo watadakwa na wale wanaofanya shughuli hizi Mikoani, watawadaka waendeleze, sasa tukubaliane hawa

ni watoto pamoja na wenye umri lakini watoto ndiyo wanaotumika zaidi. Hebu Serikali ilidake basi haraka. Tunapaswa kufanya nini?

Tumeanza na Dare es Salaam, Mwanza wapo, Kagera wapo, Mtwara wapo na Ruvuma wapo. Hebu tuwadake hawa watoto, tunawabeba vipi ghafla ili kusudi tuwafikishe mahali watulie? Je tuna wa-*counsel* vipi? Ni Wizara hii hii, maana tunazuia hapa na kwingine je? Watawapokea kabla ya kuwapokea, *let us do something* ili kusudi hili suala kama kweli limeanzishwa, ninampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika kulianzisha hili, lakini sasa tukubaliane tupambane nalo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lingine. Kawaida yangu mimi sitaki kupigiwa kengele ya pili. Napenda kukushukuru kwa kunipokea na mimi nimezungumza kwa uchungu katika haya, lakini ninaamini mtayafanyia kazi kama sio leo, lakini basi katika Bajeti ijayo, tukubaliane, jamani tutoke mahali tulipo Wizara hii tunaimba mno na isieleweke kwamba ni Wizara ya wanawake kwa sababu wachangiaji wakubwa wanakuwa wanawake na madume yamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Maria Hewa. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Keenja. Naomba mkubali kwamba Mheshimiwa Keenja ameridhia kuchangia kwa dakika zilizosalia.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru na nimhakikishie Maria Hewa kwamba wanaume na sisi tupo na akina mama katika kutetea maendeleo ya nchi hii.

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ndefu na nzuri inayoomba pesa kidogo sana za Maendeleo na pia za Matumizi ya kawaida. Katika Wizara zote nafikiri hawa ndio wanaoomba pesa kidogo kuliko wengine wote. Kwa hiyo, la kwangu la mwanzo kabisa ni kuiomba Serikali iangalie jinsi itakavyoiongezea Wizara hii raslimali kwa sababu kazi zilizopo mbele yao ni muhimu na zinahitaji fedha nyingi sana kuzitekeleza kama kweli itatekeleza ipasavyo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yenye lengo la kuondoa umaskini na kuhakikisha kwamba hali za kila Mtanzania zinakuwa bora zaidi.

Naomba pia niwapongeze akina mama wote waliochangia. Ni kweli wamechangia kwa nguvu kweli kweli, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, ameshatoka, lakini alizungumza kwa bidii, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa amezungumza kwa bidii kabisa. Nawapongeza kwa dhati, lakini hili la Benki wasitegemee Serikali kuwaanzishia. Wapo wengi na wote wana waume wengi. Tukiungana pamoja, hiyo Benki itaanzishwa na itatusaidia kutatua matatizo katika familia zetu. Nataka niwahakikishie kwamba tutawaunga mkono, lakini anzeni basi. Mkiendelea kuzungumza tu, sasa hivi ni zaidi ya miaka mitano. Itapita mingine mitano kabla ya hii Benki haijakuwepo na Benki ingetusaidia sana kusomesha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu nililotaka kuzungumzia ni hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni watu muhimu sana katika Jamii na wametoa viongozi wengi sana katika nchi hii na hata sasa hivi katika Bunge kuna waliotokana na Idara hii ya Maendeleo ya Jamii, ni Idara ambayo kwa mafunzo yake inalea Viongozi, Walimu na wanamaendeleo pia. Lakini sasa hivi ukiwatafuta huwaoni na ukitafuta fedha zilizotengwa kwa ajili yao, kwenye vitabu hivi hakuna na ninafikiri ndiyo sababu hawaonekani.

Kwa hiyo, ukienda kule kwenye Jimbo langu la Ubungo ukatafuta Maafisa Maendeleo ya Jamii ili wakae na akina mama waandae mipango ya kuwaendeleza, hawapo. Kwa hiyo, akina mama inabakia sasa wabuni ni nini wafanye ama waajiri mtu ili awaandalie mipango yao ndipo waweze kwenda kuomba misaada kuitekeleza.

Kazi ya kwanza kabisa ambayo nafikiri Wizara ingefanya mapema kabisa ni kuhakikisha kwamba Idara hii inaanza kufanya kazi kama inavyotakiwa kufanya kazi na tutaomba kwa kweli, mwaka kesho tutakapokutana hapa ili tusishike Shilingi yao, hii Idara iwe imeshaanza kufanya majukumu yake. Tumezungumza kwamba tutatoa Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ili ziende zikabadilishe hali zetu ziweze kuwa nzuri zaidi. Ni nani watakaotuandalia mipango ya kutumia fedha hizi kama siyo Idara ya Maendeleo ya Jamii? Hii Idara ya Maendeleo ya Jamii miaka yote imekuwa ndiyo Idara inayotufundisha hata jinsi ya kuishi, jinsi ya kulea watoto, jinsi ya kujenga nyumba zetu na kuzitunza, jinsi ya kuandaa chakula tunachokula na jinsi ya kupambana na matatizo yote katika jamii na kuratibu Idara nyingine.

Lakini sasa hivi ukiitafuta, haipo! Huioni na Mheshimiwa Hewa anasema hawakubaliki kwenye Halmashauri. Hawakubaliki kwenye Wizara pengine kwa kuwa hawaonekani. Maana wangejitokeza wakafanya majukumu yao ipasavyo, kila mtu angewatafuta. *Demand* yao ingekuwa kubwa sana. Nami nataka niseme, Mheshimiwa Waziri, hebu tumia mwaka huu basi kwa hivi vipesa vidogo ulivyopewa, uhakikishe kwamba Idara hii inaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Kuna vikosi vya ujenzi vinavyofundishwa kwenye Chuo chetu cha Misungwi, Mheshimiwa Jacob Shibiliti ametetea sana Chuo hiki hapa Bungeni. Wale walikuwa muhimu sana ndio waliotufundisha kujenga nyumba za kuishi, kujenga barabara na madaraja, kuchimba visima na kadhalika. Nani ameona siku hizi vikosi vya mafundi hao? Wamekwenda wapi? Lakini nikiangalia katika hotuba ya Waziri, bado tunawafundisha halafu tukishawafundisha wanaishia wapi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana hii Idara ya Maendeleo ya Jamii ipewe uhai mpya, ianze kufanya kazi zake ipasavyo hata kama itakuwa na maana ya kubadilisha matumizi ya vipesa hivi walivyopewa ili kuipa Idara hii uhai na sisi tutakaporudi kule kwetu naomba tutafute Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo, tukae nao tuwahimize waanze kufanya kazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kwenda kuomba mkopo mpaka uwe una *write up. Write up* ingeandaliwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii wakishirikiana na sisi, maana

hilo wamefundishwa, tumejaribu kuanzisha kilimo cha mazao katika baadhi ya maeneo hatukufanikiwa kwa sababu hakuna *Sociologist* aliyetangulia kule kwenda kuangalia wananchi wanahitaji nini na ni njia gani tutumie ili tuweze kufanikisha mazao hayo. Hawa ndio wangetusaidia kufanya kazi hizi na wanaandaliwa Maalum kwa ajili hiyo.

Lakini nikiangalia Chuo cha Tengeru, kimepewa Shilingi milioni 300 kusomesha vijana 810. Sijui muujiza gani utakuwa wamepewa pesa kidogo sana na nyingine kidogo sana zimetokewa kwa vile Vyuo vingine vya Buhare, Lungemba na hizi Malya zinazozungumziwa na kadhalika hamna pesa zilizotengwa hapa kuendeleza wananchi wa nchi kwa kweli na mimi nafikiri ni jambo la kusikitisha sana. Kwa kuwa muda wangu ni mfupi, naomba niruke. Nitaruka jinsia maana wanawake wamezungumzia kweli! Jinsia, lakini wamejizungumzia wenyewe hawakuzungumzia wanaume, potelea kwa pote lakini nitawaruka hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Wizara ya Watoto na kule Jimboni kwangu tulikwenda Makuburi kwenye Shule moja tukakuta asilimia 10 ya watoto ni yatima, yaani hawana baba wala mama na wengine wanaishi maisha magumu kweli kweli. Nimesoma hotuba ya Waziri tangu mwanzo, maana bahati nzuri iligawiwa mapema, tangu mwanzo, mpaka mwisho sioni mkakati wa kushughulika na yatima katika nchi hii, sioni mkakati unaowekwa na Wizara hii wa kushughulikia yatima.

Hivi karibuni nilikuwa nasikiliza redio, kuna watu walifanya utafiti wanasema asilimia 24 ya watoto wa Tanzania ni yatima kutokana na utafiti waliofanya Kibondo na Wilaya nyingine kama Kilimanjaro na Dar es Salaam. Asilimia 24 ya watoto ni yatima, yaani robo ya watoto wetu ni yatima. Huwezi kuachia vyombo ambavyo huna uhakika navyo vishughulikie, suala hili limekuwa kubwa. Ni lazima Serikali iweke utaratibu wa kushughulika na watoto yatima kuhakikisha wana malezi, chakula, mahali pa kulala, wanasoma, wanalelewa katika maadili ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, tumeonyeshwa hapa, ukienda Makete kuna familia nyingi sana ambazo watoto wanalea watoto, tumeonyeshwa picha za watoto wakifanyishwa kazi za kubeba matofali kupeleka kujenga kwa pesa kidogo kabisa. Ile tunayosema unyanyasaji watoto, wanapokuwa hawana mlezi, hali inakuwa mbaya zaidi. Sasa tunaomba Wizara hii iweke utaratibu na ije na mkakati wa kutuwezesha kushughulika na hawa watoto yatima walio wengi na wanaozidi kuongezeka. Mwaka kesho hauko mbali, ni miezi 12 kuanzia sasa. Tutakutana tena hapa. Tunaomba tukutane hapa tukiwa na mpango wa kusaidia hawa watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinaitwa *FDCs,* vile Vyuo ambavyo Mheshimiwa Joyce Massunga amezungumzia hali yake. Vile Vyuo ndio vya kufundisha akina mama, vijana na sisi wengine *skills,* taaluma za kutuwezesha kufanya shughuli zetu, ndivyo Vyuo vya wale wote ambao hawakujifunza mambo fulani fulani Shuleni, wanaotaka kujifunza sasa, ndio Vyuo vya kujifunza kilimo, userumala, ujenzi, upishi, jinsi ya kulea watoto na kadhalika. Lakini vile Vyuo 58 viko katika hali mbaya sana. Vitanda ndiyo hivyo vya *Banco* ambavyo *spring* zenyewe zimeshaachia. Vinatumika kwa muda mdogo sana katika mwaka.

Sasa nilikuwa naangalia katika Bajeti, hivi vingetengewa Shilingi ngapi? Mafunzo yametengewa Shilingi milioni 15 kwa Vyuo 58. Labda tuombe Malaika washuke kutoka Mbinguni watusaidie kufundisha katika hivi Vyuo. Maana sioni Shilingi milioni 15 zitakavyotosha kufundisha. Takrima katika fungu hili ni Shilingi milioni 13, mafunzo ni Shilingi milioni 15, yaani unaangalia mambo mengine huku duniani wala huyaelewi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimeomba hivi Vyuo vifanyiwe kazi na vitumike mwaka mzima kutufundisha zile *skills* tunazohitaji. Nataka kufanya biashara, sijui kufanya biashara, niende *FDC* nikutane na Mwalimu anifundishe kufanya biashara. Hakuna mahali pengine naweza kwenda. Kuna *Community Centers*, mwaka 2005 Wizara iliahidi kwamba ingefanya uchunguzi wa *Community Centers* na kuhakikisha zinafufuliwa. Mwaka huu wala hazizungumziwi. Sasa tunaomba hizo nazo zifanyiwe kazi kwa sababu sababu ni vitu ambavyo vinatuleta, vinatukusanya na kutupa mafunzo ya kutuwezesha kuendesha shughuli zetu kwa uhakika zaidi na kwa ujuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika ulizonipa nikiangalia saa, zimekwisha. Naunga mkono hoja, lakini naomba haya niliyoomba yafanyiwe kazi ili mwaka kesho tutakapokutana hapa tusigombane, bali tupongezane, tuondoke hapa tukiwa marafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Keenja.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba niseme kwamba, ili tuweze kuendana na shughuli yetu ya jioni ya leo vizuri, ninaomba sana kwa heshima yote tukajaribu kusoma na kujiandaa kwa kulingana na maelekezo ambayo niliyatoa pale saa 4.00 asubuhi wakati tumemaliza kipindi cha maswali kwamba, kila mtu ajitahidi kuangalia anataka maelezo ya ziada kuhusu nini na yanaendana na kifungu kipi. Hiyo itanisaidia kunipa ushirikiano katika kupitisha zile *votes* za matumizi, vinginevyo itakuwa ngumu kufikia *Development Book* na kujua yaliyomo mle na hivyo tutaishia tu katika kipengele kimoja kitu ambacho hatujitendei haki sisi wenyewe wala Mwenyekiti anayeendesha Kikao, wala Wizara kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuzingatie hilo.

Lakini mchana tutakuwa na wasemaji wawili. Tutakuwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Jacob Shibiliti ama mmoja ama wote wawili tutaangalia muda wetu mchana tutakavyoutengeneza, lakini tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri. Yeye ataanza saa 11:15 jioni na Mheshimiwa Waziri ataanza saa 11:30 jioni.

Wakati nipo hapa mezani nimepokea viji-*note* kama vitatu kwa Waheshimiwa Wabunge wa jinsia ya kiume wakilalamika, mbona wanaume hawachangii? Sasa naomba niseme kwamba walioomba kuchangia, kwanza miongoni mwa wale walioniletea viji-*note* kwamba wanaume hawachangii hawakuomba. Hilo kwanza naomba muelewe kwamba hata wao hawakuomba.

Lakini la pili, walioomba walikuwa ni hao ambao nimewapa nafasi za kusema, lakini pia wao walishachangia mara nyingi kwenye hotuba zilizopita. Tatu, naomba niendelee kusema kwamba, wanawake walioitwa mwanzo, wao waliacha kuchangia hoja nyingine wakiweka makusudio ya kuchangia hoja hii. Kwa hiyo, nafikiri nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wanaume mwakani na wao waweke nia ya kuchangia hotuba hii ili kuweka usawa wa jinsia.

Mwisho, niseme marekebisho machache kwamba wengi wakati wanachangia hoja wamekuwa wakiitaja Wizara hii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto. Hapana. Wizara hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na tunapozungumza jinsia tunazungumza jinsia ya Me na ke kwa ujumla wao. *(Makofi)*

Naomba kusitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07:00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa leo jioni tumekubaliana ama Mheshimiwa Jacob Shibiliti ama Mheshimiwa Bujiku Sakila. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Bujiku Sakila na baada ya yeye, Mheshimiwa Naibu Waziri ataanza kujibu hoja zetu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niwe kama mchangiaji wa mwisho katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu kwa mambo mawili, kwanza, labda niseme kwamba mimi ni mmoja wa wajumbe katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Nimeona Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na wafanyakazi wa Wizara hii jinsi wanavyohangaika kuiweka sawa Wizara hii. Nawapongeza sana kwanza kwa harakati walizozionesha tangu mwanzo. Nawapongeza, wameanza kuonesha mifano, kuna Chuo cha Misungwi, walikuwa wametoa ahadi nyingi sana, wamefanya kazi nzuri sana, sasa hivi mambo mengi waliokuwa wameahidi tangu wameteuliwa mambo mengi yameshatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasiliana na Mheshimiwa Jacob Shibiliti na amethibitisha hivyo. Kwa hiyo, kwa niaba yake natoa shukrani kwa Wizara hii, kwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wa Wizara hii kwa kutimiza yote ambayo yalikuwa yameahidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichobaki kwenye Chuo hii ni viti na meza hasa sehemu ambazo zinahitaji viti na meza ndivyo vitu pekee vilivyobakia. Tulikuwa tunafikiri ni vyema Mheshimiwa Waziri akipata nafasi ya kutembelea Misungwi akaenda kuangalia Chuo chake kinavyopendeza hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pia kwa hotuba yake nzuri. Hotuba nzuri ni mwanzo mzuri wa Awamu ya Nne, inatia matumaini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kwanza nikushukuru wewe kwa ufafanuzi wako ulioutoa ulipokuwa unasitisha Shughuli za Bunge mchana kwamba Wizara hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii siyo Maendeleo ya Wanawake pekee yao ni Wizara ya Jinsia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kuzipongeza Awamu Tatu za Serikali zilizopita za nchi yetu. Wamekuwa wakionesha juhudi hatua kwa hatua katika kuleta usawa wa wananchi wao. Hivi sasa tuko kwenye hatua nzuri, ni matokeo ya juhudi nzuri zilizofanywa. Mimi naamini katika Awamu hii ya Nne mambo yataenda haraka zaidi ili kukaribia zaidi usawa wa jinsia zote mbili. Nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Wizara hii. Wizara hii kama walivyokwishasema wenzangu ni Wizara muhimu sana. Wizara hii tunapoongea, tunaongelea juu ya maendeleo ya wananchi. Maendeleo lazima yawe na kitu cha kusukuma mbele. Wizara hii ni kama dereva wa gari. Gari haliwezi kwenda bila dereva. Kwa maana ya maendeleo, Wizara hii ndiyo inayotakiwa kusukuma maendeleo. Tunapongea juu ya elimu, lakini watu wa kuhamasisha mambo ya elimu ni ya Wizara hii. Tunapongea juu ya maji, wanaoweza kuhamasisha miradi ikakamilika ya maji ni Wizara hii hasa katika kipindi hiki ambacho tunaongea juu ya maendeleo shirikishi ya wananchi, kuwashirikisha wananchi wenyewe katika upangaji wa mipango ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa tano wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaelezea majukumu ya watendaji wa Wizara hii. Hapo ndipo tunaona umuhimu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kuelezea upande wa Wizara. Tukirudi nyuma miaka ya 1960 kama alivyojaribu kuelezea Mheshimiwa Waziri mtaona jinsi ambavyo Wizara hii inavyosaidia kuleta maendeleo katika hatua za mwanzo mara baada ya kupata Uhuru wetu. Lakini hapo katikati kwa bahati mbaya sana ni kama tulijisahau, Wizara hii ilikuwa imesahaulika kidogo, ikapoteza majukumu yake, karibu miaka 30 Wizara hii haijaonyesha uwepo wake katika jamii ya Tanzania. Mtaona hata bajeti yake ni ndogo sana. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote waliosema bajeti yake ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie Wizara hii ili mwaka ujao wa fedha ije na kiasi cha kutosha cha fedha za bajeti. Nafahamu kwamba kila Wizara ingependa kupata fedha nyingi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ingependa kupata fedha nyingi, Wizara ya Maji ingependa kupata fedha nyingi, lakini mipango hii tunaifanya tukiwa ofisini. Lakini

tunatakiwa kuifikisha kwa wananchi, ikasimamiwa na watu. Wahamasishaji wakuu wa miradi yetu hiyo ni wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii iongezewe fedha hasa kwa upande wa usafiri. Wawezeshwe waweze kusafiri, Wizara hii siyo ya kukaa ofisini, Wizara hii ni ya kukutana na wananchi mara kwa mara kwa kufanya mikutano, kwa kufanya semina, kwa kuwatembelea katika miradi mbalimbali hapo ndipo wananchi wataona kwamba wako pamoja na Serikali yao. Lakini bila kuwezeshwa katika usafiri hii Wizara haiwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna pikipiki kumi, kuna Wilaya nyingi sana ambazo hazina usafiri katika Idara hii, maana yake ni kwamba Idara hizi katika Halmashauri zetu hazitafanya vizuri sana kama hazitawezeshwa kusafiri. Usafiri wa kusubiri fadhila kwa Wizara hii haufai. Wanatakiwa kuwa na vyombo vyao vya usafiri. Kwa hiyo, mimi natarajia kwamba mwaka kesho watakuja na taarifa kwamba wamepata kama ni pikipiki basi kwa Halmashauri zote. Kama ni magari wapate angalau Wilaya zote, waweze kutembea na kukutana na wananchi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri za Wilaya tunawaombea fedha ili waweze kufanya kazi, lakini ipo haja vile vile watumishi hasa katika Halmashauri waoneshe uwezo wao na uwepo wao katika Halmashauri hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea ni kwamba wao ni wanyonge huwa wanakaa wanasubiri miradi ya Idara zingine, wapewe nafasi ya kusimamia. Ushauri wangu ni vizuri Idara hizi zenyewe ziwe zinabuni miradi kwa niaba ya Halmashauri, waweze kubuni, waoneshe njia ili hata Idara zingine ziweze kufuata mifano yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vyema kama nilivyosema mwanzo dereva akiingia kwenye gari akakaa tu, gari haliwezi kutembea liende mpaka aendeshe, ndiyo wenyewe wanatakiwa kuonyesha njia. Kwa hiyo, lazima waoneshe uwepo wao katika Halmashauri, waoneshe kwamba wanaweza. Lakini ili waweze kufanya hivyo pamoja na hilo nililosema la usafiri wanatakiwa wawezeshwe kielimu. Kuna wakati mwingine wanajisikia wanyonge kwa sababu tu hawalingani. Ukimchukua Mkuu wa Idara fulani na ukamlinganisha na Mkuu wa Idara wa Maendeleo ya Jamii unaona kwamba kielimu anaweza kuwa chini, akiwa chini hatakuwa na uwezo wa kukutana na wadau na wenzake hatajisikia vizuri.Kama kuna *degree* tukubaliane kwamba basi Wakuu wa Idara wafikie katika kiwango cha *Degree* ili Wakuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu wasiwe na ule unyonge mbele ya wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja nyingine moja inayohusiana na wasichana wanaopata mimba. Hawa ni watoto wetu na tunawahitaji. Kwanza niseme kwamba binti hawa siwalaani ni kwamba wamekosea, lakini siwalaani. Mimi nimekuwa katika Wizara ya Elimu na Utamaduni wakati uliopita kwa kipindi kirefu sana. Tumejitahidi sana kuwarudisha watoto hao mashuleni. Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, akiwa Waziri

wa Elimu na Utamaduni wakati huo amejitahidi sana kutafuta njia za kuwarudisha watoto hao shuleni, haikuwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Joseph Mungai amejitahidi sana kama Waziri wa Elimu na Utamaduni wakati huo kuwarudisha watoto hao mashuleni haikuwezekana. Napenda kusema kwamba pamoja na kwamba safari zote hizo haikuwezekana, si mara zote haitawezekana, inawezekana. Tatizo lililopo lazima tujiulize tunaambiwa mtoto huyo arudi shuleni kwa sababu gani? Kwa sababu tunamhitaji baadaye aje alitumikie Taifa, kama si yeye basi ni mtoto wake aje alitumikie Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuangalie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tumeikabidhi mamlaka ya kukaa na watoto wetu kuwalinda, tujaribu kufikiria kwa mfano, wewe una mtoto wako mzuri sana, darasani anajitahidi na unampenda sana, je, akipata mimba utajisikiaje? Utaumia sana. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na yenyewe inaumia hivyo hivyo. Lakini tulichokuwa tunaogopa na kinachoshindikana ni kwamba je, athari zake zitakuwaje?

Ni kweli ni vyema kuthubutu, lakini tatizo la maamuzi ya kielimu madhara yake huwa yanakuja kuonekana baada ya kipindi kirefu sana. Unaweza kuamua leo, nafahamu Zanzibar wenzetu wameshaamua kwamba watoto hao warudi shuleni. Athari yake sio ya leo, sio ya kesho, wala sio ya kesho kutwa. Mimi wala sijasema kwamba wamefanya kosa, wala sijasema kwamba wamefanya vizuri, ila athari zake ninavyosema zinaweza kutokea baadaye sana na jinsi ya kusahihisha inachukua muda mrefu sana.

Mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo na Ufundi ajaribu kuangalia vizuri sana jinsi ya kuwasaidia watoto hawa, hawa ni watoto waliokosea kama binadamu mwingine. Wanahitaji kusamehewa, kupewa nafasi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba Serikali ijaribu kuangalia pamoja na juhudi nyingine zinazofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo na Ufundi kujaribu kuangalia uwezekano wa kuwarudisha watoto hawa kama Waheshimiwa Wabunge wengi wanavyoomba. Ni vyema vile vile ikaangalia uwezekano wa kuwasaidia *UMATI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UMATI* wanafanya kazi nzuri sana ya kuwasaidia watoto hao. Tusiangalie tu uwezekano wa kuwarudisha watoto hawa shuleni, tuangalie njia zingine ambazo zinaweza kuwasaidia watoto hao, tuwatie moyo, waweze kuingia katika njia zingine ili waweze kuendelea kutoka pale walipoachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Lakini kama nilivyosema nilikuwa naiomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. VEDUSTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu, kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Wizara yake kwa kazi nzuri zinazoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu pamoja na kuipongeza Wizara kukubali kuwezesha Chuo cha Buhare kutoa *Diploma* ifikapo mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua kwa mpango huo ni maandalizi gani yamefanyika kuhakikisha kuwa *Diploma* zinatolewa? Chuo kina wanachuo zaidi ya 800 ni lini chuo kitapata gari la ofisi kwa ajili ya Chuo cha Shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bweri *FDC,* Wizara bado haijatamka lolote namna ya kukiendeleza huku chuo kina matatizo ya kila aina naomba Waziri anileleze mpango kamili wa kuendeleza chuo.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii ya pekee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi pamoja na safu nzima ya uongozi wa juu wa Taifa. Nawatakia afya njema katika kutekeleza majukumu walio nayo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, pamoja na wewe Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuwasilisha hotuba nzuri mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia na swala la umaskini wa kipato kwa Watanzania hususan wanawake. Naomba nichukue nafasi hii kutoa rai na kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika kampeni zake za uchaguzi kwa kusema, Watanzania wengi ni maskini lakini wanawake ni maskini zaidi. Niipongeze pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuandaa mkakati mzuri wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu ukitekelezwa vizuri utasaidia sana kuboresha maisha ya Watanzania hususan mwanamke. Naomba Wizara husika iandae utaratibu mzuri utakaowawezesha akinamama wengi kujiunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa *SACCOS* na *SACCAS.* Pia afisa maendeleo ya jamii watoe mafunzo kwa wanawake wajasiriamali ili kuwawezesha kubuni mbinu mbalimbali za kuweza kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi zaidi, kuboresha jitihada zilizopo ili kuwawezesha wanawake wajasiariamali kupata masoko ya ndani na ya nje ya nchi yetu pamoja na kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ili kuweza kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swala la maafisa maendeleo ya jamii, watumishi hawa wapo karibu sana na wananchi. Tena wana wajibu mkubwa sana kwenye Halmashauri kutokana na wajibu walio nao hasa kwa kipindi hiki cha kuwahamasisha wananchi katika swala hili la kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na MKURABITA. Naomba Serikali iwaonee huruma Maafisa Ustawi wa Jamii kwa kuwapatia angalau usafiri na kuwaongezea mishahara mizuri ili wapate moyo wa kuwafikia wananchi wengi katika falsafa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, kwa maendeleo ya Mtanzania inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwafukuza watoto wa kike wanaopata mimba shuleni, naomba nichukue nafasi hii kuiomba Serikali iangalie sana suala la watoto wa kike wanaofukuzwa shuleni kwa kosa la kupata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtoto kupata mimba ni kosa kubwa kuliko mwizi au jambazi anayevunja na kuiba? Jambazi akikamatwa anapelekwa penye usalama, mahali ambapo atakula, atalala, akiugua atatibiwa na anashauriwa, mtoto wa kike akipata mimba anafukuzwa shule, akirudi anafukuzwa nyumbani, aliyempa mimba pia anamfukuza. Hivi mtoto huyu tunamfukuza aende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga walisema, uchungu wa mwana aujua mzazi. Imekuwaje leo wazazi mnawafanyia watoto ukatili mkubwa hivi? Hatuoni kwamba sisi ndio tunachangia ongezeko la watoto wa mtaani. Serikali inapiga vita ajira mbaya ya watoto na huku Serikali hiyo inawafukuza shule, je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina mpango gani wa kusaidia watoto hawa wanaopata mimba shuleni na hatimaye kufukuzwa? Naomba wapewe *maternity leave* akishajifungua arudi kuendelea na shule.

Mheshimiwa Mwenyekti, kuhusu watoto walio katika mazingira magumu, naomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na *NGOs* iliangalie hili kwa karibu sana kwa kuwa wazazi pia wanachangia kutuma watoto waende katika mazingira magumu kuwatafutia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa migodi, natoa wito kwa jamii na pia wachimbaji waweze kuwaondoa watoto walioko katika maeneo ya karibu na migodi wawashawishi ili watoto waende shuleni badala ya kwenda machimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongeza zangu za dhati kwa Waziri na Naibu waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hoja hii kuhusu suala la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali sambamba na uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu na mikoa kwa ujumla

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiuliza Serikali inafanya nini ili kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa mashirika haya ili kuweza kujua shughuli ambazo zimekuwa zikifanywa na mashirika haya katika usimamzi na utekelezaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika haya yamekuwa yakifungua vituo vya kulelea watoto yatima bila kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa Wizara hali inayosababisha wao kujiamulia jinsi ya kuwatunza sambamba na idadi yao katika kuwahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia masuala haya hasa ikizingatiwa kwa baadhi ambao si waaminifu wamekuwa wakitumia mwanya huu kujinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua ni jinsi gani Serikali itafufua uwepo hai wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Maafisa Maendeleo ya Jamii halina budi kuangaliwa upya kwa Serikali kufufua upya idara hiyo kutokana na wimbi la ongezeko la watoto yatima kutokana na ugonjwa huu wa UKIMWI.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kupata fursa ya kuchangia hoja hii. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba inayogusa masuala muhimu ya maendeleo ya ustawi wa jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yaliyoelezwa napenda kuchagia kwa kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mmomonyoko wa maadili kwa watoto, vijana na watu wazima limeongezeka kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya mmomonyoko huu ni kuongezeka kwa mwenendo na tabia mbaya, ukosefu wa adabu baina ya watoto, vijana na watu wazima, vitendo vya uhalifu, rushwa, ubakaji, ngono na UKIMWI. Ili kukabiliana na matatizo haya, naishauri Wizara hii ipendekeze kuwepo kwa mitaala katika *syllabus* za shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu itakayotoa elimu kwa uwazi zaidi, mahsusi inayohusiana na maadili mema yanayolenga mambo niliyoelekeza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu iwapo Serikali inazo takwimu za idadi ya vilema wote waliomo nchini mwetu na *classification* ya aina ya vilema walivyonavyo, mgawanyiko ulivyo katika Mikoa/Wilaya/Kata mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo takwimu hizi zinajulikana, naomba zisambazwe kwa Wabunge na ofisi zote husika. Takwimu hizi zitasaidia watendaji mbalimbali na hata taasisi za Serikali, binafsi na sisizo za Serikali kuelewa na kutafakari namna michango yao kwa mawazo, ushauri kwa hali na mali inavyoweza kuwasaidia kimaendeleo au vinginevyo. Ikiwa takwimu hizi hazipo, naishauri Serikali ichukue hatua za kufanya sensa ya walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhana hiyo hiyo ni muhimu Serikali ikaelekeza kila Wilaya iorodheshe idadi au kundi la wananchi/wazee wasiojiweza ili kuratibu na kuandaa mipango ya awali ya kuwasaidia hususan katika mahitaji ya elimu kwa watoto wao halisi wanaowategemea. Kwa njia hii taratibu za zimamoto katika kutoa misaada zitaepukwa na pia tutaepuka kupoteza *potential* ya watoto wenye akili wenye wazazi wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi vijijini, utaratibu wa kupewa msaada wa kuelimishwa na Serikali kwa watoto wa wazazi wasiojiweza, haujasambaa vya kutosha na kwa uwazi. Naiomba Wizara husika iongeze juhudi za kutangaza taratibu za kueneza taratibu hizi kwa kutawanya vipeperushi Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya *population* na *family life education* ni muhimu sana kwa jamii nzima nchini. Nampongeza Waziri kwa kupania kuendeleza elimu hii kwa maafisa maendeleo nchini. Kutokana na umuhimu na unyeti wa suala hili, napendekeza Waziri awasiliane na Taasisi mahsusi inayohusika na somo hili, aandae na kutoa semina ya elimu hii kwa Wabunge wote, ili wasaidie kutoa elimu kwa karibu zaidi katika jamii zao. Naunga mkono hoja hii na kutakia mafanikio na ahsante sana.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni, Zanzibar napongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na pia kuwa msimamizi mkuu wa CCM (Mwenyekiti), hivyo sina budi kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, kwa kuwasilisha hotuba nzuri Bungeni, napongeza sana pamoja na watendaji wote nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali Maofisa na watendaji wakuu wa Maendeleo ya Jamii wapatiwe elimu, vitendea kazi, mikopo na akiba pamoja na huduma safi ili kumudu kazi zao vizuri na kuhudumia wananchi vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya wanawake na watoto, Serikali itowe umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya mfuko wa wanawake na watoto, kwa sasa huduma hazitoshi kwa hiyo, wakipatiwa fedha wanawake wanaweza kwenda na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya na kuendeleza maendeleo na pia kuleta malezi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamasisha vikundi vya kuweka Akiba *SACCOS,* wananchi wote kupitia Mikoa, Wilaya, Majimbo, vijiji hadi kaya. Wahamasishwe kuunda vikundi vya *SACCOS)* na Kuweka *(Account Bank)* na kuweza kupata mikopo jiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, viongezwe vyuo vya maendeleo ya jamii hasa menejimenti, uandaaji wa mradi, takwimu, mawasiliano, utunzaji wa watoto na mazingira ya walimu na kuwaelimisha vijana wetu.

Kwa niaba ya wananchi wa Magogoni na kwa niaba yangu naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na lengo zuri la kuwahamasisha na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali ili kupewa mikopo, ni lini na kwa utaratibu gani wajasiriamali wa Ludewa watafikiriwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atembelee Wilaya ya Ludewa ili ajionee hali ilivyo huko. Ili kuelekeza juhudi za Wizara, Waziri awatembelee akinamama wa Kata ya Lumbila katika mwambao wa Ziwa Nyasa wanaojishughulisha na ufinyanzi vyungu vya kupikia na kuwasaidia elimu ya ufinyanzi vyungu vya mapambo na namna ya kupata masoko ya vyungu vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubainishaji wa mahitaji ya wanawake wajane na wale waishio na virusi vya UKIMWI haukufanywa kisayansi. Maeneo yaliyofanyiwa majaribio hayawakilishi maeneo ya kutosha ya nchi yetu. Uteuzi wa maeneo haya ulikuwa ya upendeleo *(biased).* Mbona kwa mfano Nyanda za Juu Kusini hawakuhusishwa? Je, katika wanawake hao wamo wa Ludewa? Hawa watafikiriwa lini na vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pikipiki 15 zitakazonunuliwa kwanza zipelekwe kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi na yaliyo nyuma kimaendeleo ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ludewa. Je, itakuwa hivyo?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya awamu ya nne yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya imeamua kuwasaidia watoto yatima, je, Serikali ina mpango gani katika kuwasaidia watoto hao ambao wako vijijini hasa Mkoa wa Kigoma na wakati huo huo Serikali ina mpango gani kuhusu kupatiwa matibabu bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kigoma akinamama wengi kipato chao ni cha chini kabisa na wengine hawana kipato chochote. Je, huyo mama asiyekuwa na kipato chochote Serikali inamsaidiaje?

Kwa kuwa watumishi hawa bado wanang'ang'ania maofisini kama ndio muda muafaka wa kwenda vijijini, kata hadi kata kuwaelimisha akinamama kuhusu *SACCOS?* Maafisa hawa hawaendi vijijini kutoa elimu hiyo bali wanasubiri mpaka Mbunge akiwa na ziara ndio wanaandamana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwape mwongozo kuwa kazi yao sasa hivi siyo ya ofisini, bali ni ya kijijini kuhamasisha akinamama kuhusu mikopo, asiyeweza aachie ngazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kigoma kuna watoto wanaosoma pale Kibirizi ambao ni watoto wa mitaani na ambao wazazi wao hawana uwezo kabisa. Malazi yao kwa kweli siyo mazuri, godoro zimechanika, vitanda havitoshelezi, je, kwa hilo serikali inasemaje?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni nyeti kati ya Wizara nyingine iliyo na majukumu makubwa katika nchi yetu. Wizara hii inasimamia Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Jukumu la Wizara hii ni ngumu, inagusa wananchi wengi Bajeti yake ni ndogo sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwe na maendeleo kwa wananchi, lazima uwawezeshe. Wizara hii inategemewa sana katika kutoa elimu, mikopo na ulezi wa watoto yatima. Hivi shilingi 10,418,353/= zitatosha nini? Hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Wizara hii inapuuzwa kuwa eti ni ya wanawake, si kweli. Wizara hii inasimamia Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mfuko wa mkopo uongezwe toka shilingi 4,000,000/= kila Halmashauri ya Wilaya angalau shilingi 10,000,000/= huu ni mfuko unaorudishwa, si hasara. Wanawake ni waaminifu sana katika kurudisha mikopo. Nashauri Wizara hii ifanye tathmini upya juu ya mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri vyuo vingi vifufuliwe tena na ufanye kazi ya kuelimisha vikundi vya miradi ya wanawake huko vijijini. Wanawake ni waelewa kama watapewa elimu ya kutosha. Nashauri vyuo hivi vipewe nyenzo hasa chuo cha Maendeleo cha MALYA katika Jimbo la Sumve.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Benki ya Wanawake sasa ianzishwe haraka, sisi wanawake tuko tayari hata ukisema tuanze sisi wenyewe kuchangia angalau kila mwanamke kima cha chini shilingi 1,000 tutafanikiwa kukusanaya pesa nyingi sana, wanawake ni wengi sana Tanzania hii.

Namshukuru Waziri kwa kutambua kuwa kuna *NGOs* zinazosaidia kutoa misaada kwa wanawake zinazosimamiwa na wanachi wenyewe kwa kutoa elimu, kusaidia sheria zinazomdhalilisha mwanmke na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF).* Naomba nipendekeze mambo yafuatayo ili huduma hizi ziwafikie wananchi, wanawake na watoto vijijini.

Kwanza, *NGOs* hizi sasa zihame mijini zielekeze elimu vijijini, pili, Mfuko wa Fursa Sawa Wote tumwombe Mama Anna Mkapa, aelekeze huduma zake Mikoani, Wilaya zote hadi vijijini, huduma hii isiishie miji mikubwa tu, tatu, sheria zilizopitwa na wakati za kumdhalilisha mwanamke na mtoto ziletwe Bungeni zirekebishwe ili wapate haki zao na nne, sheria ya ubakaji kwa watoto na wazee wakongwe ziletwe Bungeni na zirekebishwe miaka 30 kifungo haikomeshi vitendo hivi vya kinyama, wanastahili nao tuwahukumu kutokana na tendo hilo baya (wanyongwe).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa Bungeni leo hii asubuhi.

Hata hivyo katika kipengele cha 62, Mheshimiwa Waziri ameweka dhamira ya kukamilisha mitaala kukiwezesha Chuo cha Tengeru kutoa mafunzo ya Shahada katika mwaka wa masomo 2006/2007? Utoaji elimu ya shahada ni sehemu ya Elimu ya Juu na chombo pekee husika katika taratibu hizi ni Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU).* Aidha, vyuo vyote vya Elimu ya Juu vinavyotoa elimu ya Shahada ambavyo viko chini ya Serikali, vinakuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imejitayarishaje kwa hili?

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri iliyowasilishwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi kubwa wanayoifanya kutembelea mikoani kuona taasisi za Wizara yao zinavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi katika utendaji wao wa kazi. Pamoja na pongezi hizi sasa nianze kutoa maoni yangu kama ifuatavyo nikiwa na imani kuwa hoja zangu zitapatiwa ufafanuzi ama majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali itoe maelezo kwa nini kila mwaka bajeti ya Wizara hii huwa ndogo kuliko Wizara zote wakati majukumu ya Wizara hii ni mengi na mazito, mfano ruzuku ya mfuko wa wanawake kwa ajili ya kukopesha na kutoa elimu, ruzuku kwenye vyuo vya maendeleo, vituo vya watoto wadogo, kuwawezesha maafisa maendeleo na kadhalika. Naomba tabia hii ya kuinyima fedha za kutosha isirudiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa itambue kuwa Vyuo vya Maendeleo vinahitaji ruzuku ya Serikali ili viweze kujiendesha na kutoa huduma ipasavyo. Nimeamua kusema haya kwa sababu vyuo vya Mkoa wa Singida havijapata ruzuku tangu mwaka 2004 hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itazame upya ajira ya watumishi wa Vyuo vya Maendeleo kwani kila mmoja yupo chini ya Wizara tofauti na mwingine mfano wapo ambao wapo chini ya Wizara ya Kilimo, wengine chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wengine wapo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili watumishi hawa wasipoteze haki zao wakati wa kustaafu bora wawe chini ya Wizara yao ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuwajali watumishi bali maslahi ya watumishi hawa ni madogo sana, hali hii inawafanya watumishi hawa washindwe kumudu maisha kwa ajili ya mishahara kuwa midogo sana ukizingatia kazi zao ni nzito sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itenge fedha za kuwasaidia wanawake wajane wakati wanapodai mirathi kwani wengi wao hawajui sheria na uwezo wa kuweka wakili hawana. Serikali isipofanya hivi wajane wengi watapoteza haki zao na watashindwa kulea watoto na kuwapa elimu ambayo ni dhamana yao ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiojificha kuwa mikopo wanayopewa wanawake walioanzisha miradi ya uzalishaji mali ni midogo sana. Kwa kuwa uchumi wa nchi sasa unakuwa na akinamama sasa wamestaarabika, naishauri sana Serikali itoe mikopo mikubwa tofauti na tulikotoka ili akinamama waweze kumudu suala zima la kuongeza pato la familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwapa wanawake uwezo wa kushiriki kikamilifu na kwenda sambamba na wanaume katika kuzalisha mali ni muhimu sana kufungua benki ya wanawake ili waweze kukopa na kuweka kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwani sasa inawatambua watoto waliotoka kwenye mazingra magumu, vile vile naipongeza sana Serikali kusaidia Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kulea watoto hawa. Naiomba Serikali sasa ni wakati muafaka kuanzisha vituo vya Serikali vya kulea watoto hawa na kuwapa elimu kwa asilimia mia moja kwani watoto hawa hawakuomba kukosa wazazi au kuzaliwa na wazazi wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana kwani imejitahidi sana katika kutoa semina, dawa za kurefusha maisha kwa waathirika na Watanzania kwa ujumla. Naitaka Serikali sasa semina basi zinatosha fedha nyingi zitoe huduma ya dawa na lishe kwa waathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri Serikali elimu ya UKIMWI itolewe kwa nguvu shuleni yaani shule za misingi na sekondari kwa wasichana wakubwa hata wavulana pia. Pia ihimize Serikali kujenga mabweni ili wasichana wetu walio shuleni kuachana na vishawishi vya njiani vya kila siku wanapokwenda shule na warudipo nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiojificha kuwa mila hii potofu sasa ikomeshwe kabisa na itakomeshwa tu kupitia semina ama elimu kutolewa kwa nguvu sana kwa makabila yanayoendeleza mila hii na adhabu kali sasa itolewe kwa wale watakaobainika kuendeleza mila hii chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya mchango huu sasa napenda kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR.DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza viongozi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kuendeleza jamii katika jimbo la Nkenge kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera. Chuo hicho kinafanya kazi nzuri ya kutoa elimu kwa wananchi na kusaidia harakati za kupambana na umaskini.

Pamoja na kutoa elimu nzuri, chuo kinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa umeme wa uhakika. Umeme wa *TANESCO* unapita mita chache toka chuo kilipo. Naomba sana Wizara isaidie kuwezesha chuo kupata umeme wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kusisitiza kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa ubunifu na kazi nzuri mnayoifanya kila siku. Naomba kuchagia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na dira ya Serikali ya awamu ya nne ya kuwawezesha wanawake, vijana, wazee kama ilivyo kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama chetu cha CCM, kuna umuhimu wa kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na hasa kila Wilaya ili kushirikiana na sekretariati ya mikoa na wilaya (Halmashauri) waweze kuwa waratibu na wafuatiliaji wa miradi mbalimbali inayoibuliwa na mamlaka husika kwa ajili ya kuwawezesha makundi niliyoyataja hapo juu. Hii ni pamojana kuratibu na kuunganisha vikundi mbalimbali vya wanajamii (wanawake, vijana na kadhalika).

Aidha Maafisa Maendeleo hawa wasiwe ni lazima wawe wanawake bali jinsia zote na kigezo kiwe ni taaluma kuhusu maendeleo ya jamii, jinsia na watoto. Sasa hivi tunao vijana wengi waliomaliza vyuo vikuu waliochukua masomo yanayohusiana na Wizara yenu, nashauri waajiriwe kwenye nafasi hizo na uzoefu wa kazi watakuta huko huko kazini. Nina wasiwasi tukiendelea kuwatafuta wenye uzoefu tutaendelea kuwatumia wasio na taaluma bali uzoefu tu! Hii haitoshi, bali taaluma kwanza, maana uzoefu ni rahisi kuupata ukiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara uwezeshwe kuajiri Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa. Ni miaka zaidi ya mitatu sasa tangu astaafu mama aliyekuwepo. Naomba sana jamani tumpate huyu mtu kwa umuhimu wa kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, pia kumpongeza Katibu Mkuu, Mariam Mwafisi na watumishi wote wa Wizara kwa maandalizi ya hotuba ya Bajeti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa familia yoyote ni mama na mtoto. Watoto wetu, malezi yao na jinsi utandawazi unavyokwenda kwa kasi tunaweza kushindwa kumudu usimamizi wao wa kujenga tabia njema kwa maslahi ya baadaye ya nchi hii. Nashauri Wizara iendeshe mafunzo maalum kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhusiana na mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana wetu.

(ii) Athari ya utanadawazi kwa jamii na uzuri wake/ubaya wake.

(iii) Mafunzo ya walimu hasa katika shule za msingi kuhusu somo la Uraia mwema ili tuanze kwa kasi kujenga jamii yetu ya kesho. Wasiwasi wa Rais wetu amelisema hili jana mjini Mwanza.

(iv) Magonjwa ya UKIMWI na athari zake kiuchumi ipewe umuhimu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,afya ya mama na mtoto nayo isibaki kwa Wizara ya Afya, hapa ndipo penyewe. Mafunzo haya yapewe umuhimu siyo tu kwa wanawake, bali kwa wanaume pia. Nchi hii iliendelea sana miaka 1960 na 1970 kutokana na jinsi mkazo ulivyowekwa kwa maafisa maendeleo, walifanya mengi mazuri na hivyo vyuo vyote vya Tengeru, Rungemba, Buhare na Misungwi vitumike kwa kozi ndefu, fupi na semina za viongozi mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Ilani ya Uchaguzi itategemea sana jinsi tutakavyojiandaa kwa kuwaandaa wananchi na hasa akinamama katika kutekeleza maelekezo yote yaliyomo katika dira ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Jamii, iangaliwe upya ili ioane na hali halisi ya sasa ili kusiwe, kutoeleweka kwa baadhi ya Wizara na Idara, wakati Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ikiangilia shughuli za Wizara nyingi katika kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii.

Nashauri kuundwe kamati ndogo ndani ya Wizara itakayokuwa inaratibu hatua kwa hatua, mafanikio/matatizo yanayojitokeza katika kusimamia utekelezaji wa maendeleo yetu kwa nia ya kutafuta njia mbadala ya kuboresha mipango yetu. Sheria zilizopitwa na wakati zichunguzwe zote na zibadilishwe haraka iwezekanavyo ama sivyo utekelezaji wa baadhi ya mipango inaweza kukwama. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tafadhali naomba upokee mkono wangu kwa vile nimeamua kwa dhati kukuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Kwa nini? Kwa sababu hotuba yako ni nzuri 100%. Vile vile kwa kuwa nimekuwa nikinong'ona mara kwa mara tena kwa uzuri wote na Naibu wako Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kuhusu matatizo ya Ruangwa kwa akinamama na watoto. Matatizo hayo ni mengi lakini yaliyo balaa sana ni haya yafuatayo:-

(a) Sisi wana Ruangwa tunaongoza hapa nchini yaani ni vinara wa vifo vya watoto. Kila watoto wanaozaliwa 1000 watoto 250 hawafiki umri wa mwaka mmoja, wanakufa sana.

(b) Nao akinamama wanaokufa wakiwa wajawazito na hasa wanapojifungua ni wengi. Hadi kuna jina maalum la Kimwera la *kuwa kuutanda,* likimaanisha tukio hilo la kuhuzunisha sana yaani kifo wakati wa ujauzito na hasa wakati wa kujifungua.

(c) Ukosefu wa elimu kwa akinamama kuhusu ulimwengu wa ujauzito, hakuna wataalamu kwa kuwa hata Wilaya yenyewe ya Ruangwa haina Hospitali ya Wilaya.

(d) Lipo pia tatizo la kijadi, wanawake hawaruhusiwi kutoka nje hasa kama ameolewa ni balaa tupu. Kwa vile hata kama akipata fedha haruhusiwi kuzishika ni lazima ampe mumewe azitunze. Kama unaamini kuwa wanaume ni mabingwa wa kutunza fedha za wake zao, sawa, lakini mimi naamini wanaume wana tabia ya kulewea fedha hizo na hata kwenda kuolea mke mwingine. Hata ikitokea mkopo mama huyu anakuwa *victimised* tu, kwa kweli rasilimali za akinamama haziko salama. Nadhani mazingira haya yamepitwa na wakati na yanahitaji elimu tena ya hali ya juu.

(e) Kwa kweli Naibu wako ameahidi kutembelea Jimbo hili la Ruangwa mapema sana iwezekanavyo, nami nitaandika vizuri zaidi kwako kuhusu kero hizi ili tuziweke vizuri wakati wa ujio wake na Naibu wako au wewe mwenyewe utakapoona inafaa. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuwa naunga mkono hoja yako kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni yangu katika Wizara hii. Wizara hii ni muhimu kwa Watanzania wote, hivyo basi naiomba iwe makini sana kwani ndio kioo cha jamii.

Kuhusu wanawake, watu hawa wamekuwa ndio kiungo kikubwa kwa jamii, pia sasa hivi wamebeba mzigo mkubwa sana, kwani akina baba wengi hukimbia familia zao kwa sasa na kuwaachia jukumu hilo akinamama. Akinamama wengi hushindwa kujimudu kwa sababu ya kukosa mitaji ya kujiendesha na kwa kuwa pesa za mikopo ya akinamama haiwafikii akinamama wengi, kutokana na ukiritimba ulioko katika Halmashauri au Jiji, naomba kuuliza Wizara hii imejipanga vipi sasa ili ukiritimba huo kuuondoa na kuwapatia akinamama hawa mikopo?

Pia naomba wahusika wasiwasumbue akinamama hawa kama wametimiza masharti. Mama ni kiungo muhimu sana na mama amebeba mzigo mzito, kulea watoto pamoja na baba yao pia, lakini mama huyu hana thamani mbele ya jamii. Akinamama hawa huchukua jukumu la kuomba mikopo katika taasisi zinazotoa mikopo, kwa kuwa majukumu yao ni makubwa katika kulea familia, mara nyingine hushindwa kurudisha mikopo hiyo na kubebewa hata vitanda. Tunaiomba Serikali watupie jicho akinamama

ambao wana mzigo mkubwa wa majukumu ya familia na kuweza kuwapunguzia mzigo wa elimu kwa watoto wao.

Kuhusu watoto, hili ni kundi kubwa sana hapa nchini, linatakiwa kuangaliwa kwa upendo kwa wanajamii nzima, wapewe haki zao na haki za binadamu zichukuwe mkondo wake kwa atakae kiuka haki hizo. Tarehe 14 Julai, 2006. Niliuliza swali ambalo askari wanapowakamata watoto na kuwachanganya na watu wazima hapo rumande, hiyo nimeona kwa macho, ninyi kama Wizara hamlijui hilo? Naomba wakati wa majumuisho nipate maelezo ya kina na haki ya binadamu inasemaje kwa swala hilo. Pia kuna akina baba ambao hutelekeza watoto na kuwanyima elimu watoto wao kwa makusudi sio kama hawana uwezo, ila ni kwa roho mbaya tu. Ugomvi wa baba na mama unazaa chuki kwa watoto, ninyi kama Wizara mnatoa tamko gani kwa akina baba kama hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtafaruku katika ndoa, ndio adhabu kwa watoto hawa kwa kukosa elimu na hatimaye kuingia mitaani na kujiunga na uvutaji wa bangi, dawa za kulevya, wizi na biashara za ngono, hivyo tunaiomba Wizara iwahamasishe akina baba na waweze kuwa na upendo kwa watoto wao na waweze kusomesha na kuwatunza watoto wao, hata kama ndoa zao zimevunjika.

Mwisho naiomba Wizara hii ilete Muswada wa Sheria ambayo wanaume ambao hawataki kutunza watoto wao, wanapopelekwa katika Ustawi wa Jamii, basi wafikishwe mahakamani labda ongezeko la watoto wa mitaani litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika jamii. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba aliyoiwasilisha, aidha, nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian na watendaji wote wa Wizara kwa kumsaidia Waziri kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara hii ni makubwa sana ukizingatia historia yake lakini yaelekea yanaendelea kupotoshwa kadri tunavyoendelea. Dhana ya ushirikishwaji kwa hivi sasa inaonekana ni mpya lakini dhana hii ilikuwa ndiyo msingi mkubwa wa Idara/Wizara Maendeleo ya Jamii.

Kwa kutumia dhana hiyo ya ushirikishwaji wa watumishi wa Idara (Wizara) waliweza kuhamasisha wananchi katika maeneo ili watambue matatizo yao, kupanga matatizo yao katika umuhimu na pia kubuni au kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo hayo.

______Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kuliona suala ili watumishi wa Wizara wapewe nyenzo na fursa ya kufanya kazi zao kulingana na taaluma yao. Hivi sasa watumishi hawa hawatumiwi ipasavyo na Halmashauri husika na hawapewi kipaumbele katika kupewa rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake, yaelekea mchakato wa uanzishwaji wake unasua sua na umekuwa wimbo masikioni mwa wanawake walio na hamu kubwa ya kupata huduma ya benki hiyo. Pamoja na kwamba hatujajua benki hiyo itafunguliwa wapi (mji gani) lakini hisia za wengi ni mjini Dar es Salaam, sasa tunajiuliza wanawake walio maeneo ya mbali mfano Ngara, Karagwe lakini hata Wilaya zilizo katika mikoa mingine ya pembezoni mbali na Dar es Salaam watapata huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionavyo mimi ni kwamba benki hiyo baada ya kuanzia juu ingeanzia chini, iundwe na vikundi vingi vya wanawake ambavyo vimetapakaa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara hii ifanye kazi inavyotakiwa ningeshauri watumishi waongezwe ili waonekane vijijini, Idara hii ipewe ruzuku ya matumizi mengineyo *(OC)* kama Idara za Afya, Elimu, Ujenzi na Kilimo, kKwa jumla Bajeti ya Wizara iongezwe ili majukumu ya idara yatekelezwe ipasavyo na uwepo uhusiano wa moja kwa moja wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Watumishi wa Wizara hiyo walioko katika Halmashauri za Miji na Wilaya. Naunga mkono hoja!

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba nzuri ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara yao. Pongezi maalum zimfikie Mheshimiwa Sophia samba, Waziri na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la wimbi la watoto yatima hasa wanaotokana na kufariki kwa wazazi wao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Naelewa Serikali inajitahidi kuwasaida watoto wa aina hii lakini naomba kuishauri Serikali kuanzisha Mfuko Maalum wa Serikali kwa ajili ya kuhudumia watoto yatima nchini. Mfuko huo pia katika muundo wake uwashirikishe Waheshimiwa Wabunge pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la utunzaji wa watoto wanaotekelezwa na wazazi wao ambao hupelekwa kwenye vituo mbalimbali hapa nchini. Naomba kutoa ushauri pia kwa Serikali kufikiria kutoa ruzuku kwa vituo hivyo kwa mfano Kituo cha Malezi cha *Msimbazi Centre* na vyengine pamoja na vya watu binafsi. Kutekeleza hili ni moja ya baraka kubwa itakayopata Serikali kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Watoto yatima Mwenyezi anawathamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, bado naendelea kuishauri na kuiomba Serikali kuihamisha ya Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Afya kuhamia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuwa inahusiana sana.

**MHE. KIUMBWA M. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezeshaa kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri pamoja na Naibu wake kwa Wizara yake iliyopangika na kutetea jamii pamoja na watoto kwa mtizamo wa Wizara hii inachukua mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto, Wizara naiomba wale yatima na walemavu Wizara hii ndio dhamana yake na kwa wale watoto wanopata mimba kabla ya kumaliza masomo naiomba Serikali iwatizame watoto hawa kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jamii wanaoishi vijijini na hao wafikiriwe kimaisha kwa sababu mambo yote yanaishia mijini tu kwa wale wa vijijini kuhusu mikopo inayotolewa na Serikali au *NGO* nayo ifike vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi wanajishughulisha na shughuli zao za maendeleo lakini hawana nyenzo za kuendeshea kazi zao. Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto iwaone akinamama hao ili wapate kujiimarisha kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu janga la UKIMWI Serikali naiomba iwapatie semina watoto kuanzia miaka kumi na kuendelea ili wapate kujua athari ya UKIMWI unaathiri namna gani.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niwapongeze wote Wizarani nikianiza kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo ninayo machache ambayo naomba ufafanuzi. Je, kuina mpango au utaratibu gani wa kuwahudumia akinamama ambao hupata ujauzito wakati hawana akili timamu yaani vichaa ambapo tumeshuhudia wengine wakitembea mitaani na hao watoto wao lakini katika mazingira magumu sana kwao wenyewe pamoja na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni nini ufumbuzi wa tatizo la watoto wanaopita mitaa mbalimbali humu nchini haswa Dar es Salaam wakiomba omba na ilhali hawapati elimu wala huduma muhimu kwa maisha yao ikiwa ni pamoja na kulelewa katika maadili mema?

Je, Wizara inalo kusudio la kupiga marufuku wazazi wanaowatuma watoto wao kuuza biashara ndogo ndogo maeneo mbalimbali hapa nchini? Wengine hata wakati wa usiku utawakuta mitaani pia hata nyakati za shule wanauza vitu mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoa elimu kuanzia kwenye shule za msingi kuhusu maadili mema, kwani kuna baadhi ya watoto hawana mtu wa kuwafundisha chochote maishani kwa sababu mbalimbali za kimaisha na kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa niaba ya wananchi wa Wilaya na Jimbo la Hai, nawakaribisha sana kwetu na kuwaahidini ushirikiano wetu daima. Mwenyenzi Mungu azidi kuwabariki.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mzima na afya kamili na kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kuwapongeza Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuweza kutayarisha na kuiwasilisha bajeti yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita katika suala la watoto yatima. Watoto yatima wanapata taabu sana kwani Serikali haijaweka mkakati maalum kuhusu watoto hawa, watoto hawa wanataka Serikali iwajengee makazi mazuri tena ya uhakika, kwani wengi wa watoto hawa wamefiwa na wazazi wao ambao wamekufa katika janga la UKIMWI na pengine familia zao ni maskini sana ambao hawawezi kuwatunza vizuri na watoto wanaweza kuathirika kisaikolojia na ambao tunawategemea kuwa Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kuwa sekta binafsi zinajitahidi katika suala hili la kuwalea watoto hawa lakini Serikali haijatoa kipaumbele katika suala hili kwa hiyo, naiomba Serikali itowe msaada wa hali ya juu ili waweze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanataka elimu ya kutosha kuhusu maendeleo yao na jinsi ya kuwaondolea umaskini. Wizara hii isimamie kikamilifu katika kubadilishwa sheria ambazo zinamkandamiza mwanamke. Ahsante sana na nashukuru.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina mikakati gani ya kuanzisha vikundi vya kijamii hasa walemavu, yatima, wajane na wazee vikongwe kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi?

Kwa vile jimbo la Njombe Magharibi liko mpakani mwa Mkoa wa Mbeya na liko mbali na Makao Makao Makuu ya Wilaya ya Njombe na Mkoa wa Iringa, je, Waziri au Naibu Waziri anakuja lini ili aje kuhamasisha vikundi vya kijamii kwani itakuwa faraja kwa wananchi wangu wapiga kura kuwa wana serikali inayowajali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Magharibi lina Tarafa tatu za Mdaudu, Wanging’ombe na Imalinyi. Endapo Waziri au Naibu Waziri atakubali kutembelea vikundi vya kijamii basi tutamwomba atembelee Kata ya Ilembula, Kata ya Igosi na Kata ya Saja ambako kuna mahitaji makubwa ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wake katika mishahara, nyumba na usafiri ili wafanye kazi kwa kujituma.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Awamu ya Nne wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukuteuwa wewe kuwa Mbunge na hatimaye kukuteuwa kuwa Waziri na pia nampongeza Rais kumteuwa Naibu Waziri wako.

Tunapozungumzia Maendeleo ya Jamii yetu lazima tuangalie Nyanda zote kuanzia jinsia na umri. Maendeleo hayawezi kupatikana kama msingi wa maisha haukuboreshwa. Watoto wanategemea kupata malezi bora kutoka kwenye familia zao, jirani na Serikali ambayo inatakiwa iweke misingi madhubuti katika kuwalinda kuwatetea na kuwapatia ulinzi.

Je, Serikali imeibuwa mkakati gani wa kufufua utendaji kazi kwa ufanisi kwa jamii kwani tunataka na tunategemea nchi yetu iwe na maendeleo endelevu kwa kila mmoja wetu. Kwa maana hiyo ni lini Serikali itaboresha na kuanza kutekeleza sheria ambazo zitamlinda mtoto toka akiwa mdogo na vile ni lini Serikali itakuwa na sheria na mikakati ambayo itawalinda wazee hasa wale ambao hawana watu wanaowategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuwajengea makazi mazuri wazee wetu ambapo watatunzwa vema na Serikali hadi maisha yao yanapoishia hapa duniani?

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kupongeza hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Ninaamini hotuba hii tutaitumia kama dira katika kuchochea maendeleo ya jamii. Naunga mkono hoja.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mzigo mzito wanaopata akina mama, wanawake wa vijijini wana mzigo mkubwa, wanawake wa vijijini hawajapata maendeleo yoyote kutoka Wizara hii (kuni, maji masafa marefu na kadhalika). Wizara iangalie upya utaratibu gani watawasaidia akinamama wapewe elimu kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nyingine zinaleta ubaguzi wa wanawake kwa itikadi ya chama. Waziri ashirikiane na Mbunge Ania Chaurembo kuthibitisha hili. Mikopo kwa wanawake wa Chama Tawala tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WDF* hutolewa kwa uchache kama shilingi 50,000/= hadi 100,000/=, hii haisaidii kabisa. Akinamama wapatiwe elimu hii kama anashindwa kulipa hudhalilishwa kwa kuchukuliwa vyombo vyake vya nyumbani. Shilingi milioni nne kwa Halmashauri ni kidogo. Serikali iangalie upya kiasi cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya watoto wa vijijini kupelekwa mjini kwa biashara ya ukahaba, hawa husambaza UKIMWI.

Kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Kuna kauli za kufunga vituo vya kulelea watoto ni sahihi. Serikali hadi leo haijatayarisha vituo hivyo. Wanaojitolea kuanzisha vituo inafaa wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya *NGO* zinazosaidia wanawake zinazoshindwa kutoa taarifa, je, kuna *NGO* ngapi zimetoa taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha wanawake kimefikia wapi? Je, kimekwishaanza kazi? Wanawake hawajiamini kujiunga na vyama.

Kuhusu ugonjwa wa UKIMWI Wizara iendelee kuelimisha wanawake. Wanawake wajilinde na kutoa elimu. Waathirika tusiwatenge, tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri kwa watoto hasa Dar es Salaam wananyanyaswa. Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa unyanyasaji wa watoto na watoto wapatiwe usafiri.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufinyu wa fedha za Bajeti, Wizara itengewe fedha zaidi. Fedha za maendeleo ya mikopo katika mikoa, je, Zanzibar na Pemba pia watapatiwa shilingi milioni 500? Zanzibar ipewe fungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *WDF* , wanawake maskini lakini ni walezi. Hakuna elimu ya mikopo kwa akinamama. Maafisa wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto waende vijijini kuwapa elimu ya mikopo na masoko. Mikopo ya wanawake ipunguzwe robo. Benki ya wanawake iwepo vinginevyo mwakani shilingi ichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufukuzwa wajane majumbani, sheria ya urithi zirekebishwe na lijibiwe wakati wa kujibu maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukeketa wanawake, Serikali haijachukua hatua zipaswavyo na elimu hii ipelekwe vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto yatima wengi Tanzania, Serikali na jamii iwajali na kuwashughulikia na kuwatunza. Tusiwatenge na kuwanyanyapaa.

**MHE.ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupiga vita ajira za watoto, tunaiomba Serikali iwachukulie hatua za kisheria wale wote wanaogunduliwa katika kuajiri watoto, kwani wanaowaajiri watoto ni watu wazima na akili zao na wanafanya hivyo kwa maslahi yao zaidi.

Kuhusu maendeleo ya wanawake ni dhana pana sana, hivyo Serikali tunaiomba iandae programu maalum ya kuwaelimisha wanawake wote hasa vijijini kuhusu sheria mbalimbali na haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto. Ingawa Serikali imeridhia Mikataba inayopiga vita ukatili na unyanyasaji wa wanawake na watoto na inasimamia utekelezaji wake katika nchi yetu, tunaipongeza kwa hilo, lakini bado unyanyasaji na ukatili huo unaendelezwa, tunaomba Serikali sasa itowe adhabu kali kwa wanaothibitika kufanya ukatili huo ili kukomesha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanawake/watoto walioathirika na UKIMWI. Baadhi ya wanawake hawa ni maskini mno, hivyo Serikali tunaiomba itenge fungu maalum la kuwaendeleza kwa mahitaji yao yote pamoja na watoto. Vile vile kama wanawake hao wanao uwezo basi Serikali iwasaidie, ili uwezo wao uwafae wenyewe na watoto wao kwani baadhi ya jamii huwanyanyasa waathirika kwa kuzichukua mali zao na kuwatelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu uwekwe kwa wanawake kuelimishwa zaidi ili waweze kujua mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujiamini, kuwa wabunifu na kuwa na mipango ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki ya elimu kwa watoto. Serikali ni vyema ikalichukulia kwa ukaribu zaidi kwani bado watoto wengi hasa walio katika familia maskini na zaidi vijijini wanakosa haki hii muhimu ya msingi wa maisha kwa watoto kupatiwa elimu. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. CASTOR R. LIGALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya Uhuru, Wizara hii hasa Idara ya Maendeleo ilitoa mchango mkubwa katika kuhamasisha wananchi kwa mambo mengi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule Bwana na Bibi Maendeleo alikuwa ni mgeni mkubwa kwa masuala yote mtambuka. Ili kuwezesha kurudi katika hali ile ya zamani, ningependekeza miaka ijayo Wizara ifanye yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii iongezwe ili kama ikitoa vitendea kazi kama vile pikipiki au baiskeli basi ziweze kugawiwa Wilaya zote. Tukifanya hivi, tutakuwa tunaleta *impact* ya elimu ile ambayo tunakusudia kuipa jamii. Kugawa pikipiki 15 kati ya Wilaya zaidi ya 120, hakutaleta changamoto ya haraka kwa jamii.

(ii) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri zetu ni mzuri lakini kiasi cha pesa kinachotolewa ni kidogo. Napendekeza zile Halmashauri ambazo zimeonyesha kufanya vizuri, zipewe motisha wa kuwaongezewa mara dugu ya kiwango walichopewa. Aidha, napendekeza mfuko huu uwe wa kuzunguka yaani *Revolving Fund,* baada ya marejesho ili mradi Wizara iwe inapewa taarifa ya marejesho mara kwa mara na wanawake ni waaminifu kwa asili na wanaweza wakaiteua miradi mingi yenye kuwawezesha kujitegemea kwa kuanzisha miradi midogo midogo *(Income generating activities)* kutegemea na sehemu wanajamii hao wanapoishi.

Kuhusu Vyuo vya Maendeleo vimekuwa tanuru kubwa tangu tupate Uhuru la kutoa wataalam wa elimu ya maendeleo ya jamii. Katika Wilaya yangu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *FDC* Ifakara, kina upungufu mkubwa wa walimu.

Kwa vile kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali imetenga fedha za ukarabati wa chuo hiki, (Jedwali Na.1). Ombi langu ni kuwa ukarabati huu ukiisha, uendane na Ikama mpya ambayo itakidhi malengo ya kusomesha vijana wengi waliomaliza shule za msingi na sekondari, kupata ujuzi wa stadi za kazi na kujiajiri. Wilaya yangu haina Chuo cha *VETA*.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa nikiwa mzima na kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Pia sina budi kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara na wale wote waliochangia kutengeneza na kufanikisha kitabu hiki cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara mama ambayo moja kwa moja inajihusisha na maisha na malezi ya binadamu kwa hivyo jamii yote inahusika kuisaidia Wizara hii ili majukumu yaliyojipangia yalete ufanisi. Kwa hivyo, nawaomba wazazi tuwe kitu kimoja katika kuwalea watoto wetu malezi mazuri yenye huruma na mapenzi makubwa kwa kujali watoto ndio Taifa la kesho na inapaswa kuwalea na kuwasomesha. Lakini kutokana na malezi tunayowalea hivi sasa ya kila mzee na mtoto wake hatuwezi kuwalea watoto wetu vizuri na Taifa la kesho litapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa imefika wakati ukimtia adabu mtoto kwa lengo la kumuelimisha mzazi anamjia juu mhusika na wakati mwingine kumshtaki au kuhasiana sababu ni mtoto. Pia walimu wanapojaribu kuwaelimisha wanafunzi wao ambao ndio jukumu lake mwalimu anashtakiwa au kupigana na mzee wa mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siku hizi kuna sheria mtoto asipigwe fimbo au viboko na Serikali inaridhia suala hili, hapa tunalea au tunawapotosha watoto? Mbona sisi hatukulelewa malezi kama hayo? Tusitafute mchawi, mchawi ni sisi wenyewe kwa kufuata mambo ya nje na kuacha ya kwetu. Kuna watoto wengi wa mitaani sababu ni malezi yetu tumeenda kinyume na maadili na mila zetu za Kitanzania.

Kwa hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara hii kurudisha yale mazuri ya zamani katika malezi yetu. Hivi sasa watoto wetu hawana heshima, wamejiingiza katika vitendo vya wizi, ulevi na uvutaji bangi na dawa za kulevya na kusababisha watoto wengi kuharibika akili zao na hivi sasa wanahangaika mitaani na kutia aibu Taifa letu. Kwa kuwa wahenga wamesema usipoziba ufa utajenga ukuta, bado muda upo wa kuwakusanya watoto wa mitaani na kuwaweka sehemu makusudi na kuwasomesha na kuwapa maadili mema pamoja na kuwaelimisha wazee vijijini kote. Isiwe wanaopata elimu ni wale wanaoishi mijini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara iajiri maafisa wengi pamoja na kuwapatia vyombo vya usafiri kwa kutoa elimu hiyo. Ahsante,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilishwa na Mheshimiwa Waziri kwau makini na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba Wizara hii ni muhimu katika kuendeleza wananchi kwani kuanzia mwanzo ilipoundwa Wizara hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi juu ya zana ya kila mwananchi anapaswa kujielimisha na kutafuta mbinu mbalimbali za kutatua tatizo lake mwenyewe katika familia na vijiji. Naomba nishauri yafuatayo ili kuboresha Wizara hii:-

(i) Watumishi wa Wizara hii waendelezwe kielimu.

(ii) Watumishi wapewe majukumu yao ya kuelimisha wananchi juu ya zana ya ushirikishwaji wa wananchi katika kujiletea maendeleo na hasa wanawake, hasa suala la kuanzisha *SACCOS* ambazo zinaweza ikawa ni chanzo kikubwa cha kuanzisha Benki ya Wanawake.

(iii) Serikali iongeze fedha katika mfuko wa kukopesha wanawake ambao hauna riba na unawasaidia.

(iv) Wizara itoe elimu na ufafanuzi juu ya dhana ya Wizara hii hasa neno jinsia kwani wengi bado wanashindwa kuelewa kwamba Wizara hii sio ya wanawake na watoto tu.

Mwisho, naomba Wizara hii iongezewe fedha iweze kuwajibika vizuri, vile vile iweze kununua mahitaji mbalimbali kama gari, pikipiki, baiskeli na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kunipa fursa ya kuchangia. Pili, niipongeze hotuba hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilivyo nzuri na inayolea matumaini ndani ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pia nawapongeza wataalam wake wote pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanza kuchangia kuhusu kuwawezesha akina mama kiuchumi ni jambo muhimu sana kwa sababu akinamama ndio wa mwanzo kutoa huduma majumbani. Ni wajibu wa Serikali kuweza kuongeza mkopo kwa akinamama ili mkopo huo uendane na wakati shilingi 50,000/= au 30,000/= haba sana kwa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu hasa kwa akinamama na watoto na hasa kwa wale wanaume ambao wanawatelekeza wake zao na watoto. Je, Wizara ina mpango gani kwa wanaume ambao wanawatelekeza wake zao na watoto kwa sababu wanawake hutelekezwa na waume wao na kuwaachia watoto kwa hivyo Serikali iwe na mkakati ya kuwadhibiti watu kama hao ili tatizo la watoto wa mitaani lipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nazidi kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuandaa hoja nzito ambayo imesisimua Ukumbi wa Bunge hasa katika hoja ya kufufua Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, niunge mkono hoja hii mia kwa mia kabla sijasahau.

Kwanza kabisa napenda kuishukuru Wizara kwa kuongeza idadi ya viongozi mbalimbali katika ngazi ya maamuzi, hongera sana. Ila sasa tunataka kujua tutafikaje katika kuwa Wabunge asilimia 50? Kama njia hiyo imepatikana basi itolewe mapema ili watu wajiandae, maana mwisho wa Uchaguzi ndio mwanzo wa Uchaguzi. Tutafute hiyo njia na tuelezwe mapema.

Mheshimiwa mwenyekiti, kuhusu Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali *(NGOs),* Mashirika haya yamekuwa ni ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Arusha, Moshi, Iringa na Mwanza. Mikoa mingine hawaji, tunataka sasa *NGOs* zilizosajiliwa zije pia katika Mikoa ya Kusini kufanya kazi. Vile vile Wizara ichukuwe nafasi ya makusudi kuwapa mafunzo Mikoa ya pembezoni ya kuanzisha *NGOs* zao Mikoani, badala ya kungojea *NGO* kutoka Dar es Salaam tu.

Kuhusu mikopo, mikopo inakuwa kidogo inayopelekwa katika Halmashauri za Wilaya, shilingi milioni nne, hazitoshi na hazikidhi haja, fedha ziongezwe.

Pia kuwapa uwezo wanawake *(Women Empowerment)* wa kujiamini kuomba uongozi. Wanawake wapewe semina za kuwafanya waweze kujiamini kisiasa, kijamii na kiuchumi. Imeshaonekana kuwa wanawake wanaweza kuongoza kama tunavyowaona Waziri na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wanavyoweza kuongoza, kujibu maswali na kujenga hoja mbalimbali, Waziri Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, wanachapa kazi nzuri sana, tunaridhika na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wanawake walibaki nyuma si kwa uzembe tu, bali ni mfumo wa kikoloni uliorithiwa huko nyuma wa kutenga wanawake na kutowapa elimu na hivyo kuwa nyuma kisiasa, kiuchumi na kijamii na kujiona wao ni watu wa nyumbani tu, wa kupika, kuzaa na kulea watoto na wanaume kuwa ndio kinara wa kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu sisi wanawake ni nyenzo za kufanyia kazi, tupewe elimu, tuelimishwe *(Women Empowerment),* tupewe nafasi zaidi za kazi, tupewe nafasi za ngazi za maamuzi na tupewe mikopo, tunaweza, mtajaribu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo vya akinamama na watoto, vifo vingi vya akinamama na watoto hutokea katika maeneo kadhaa nchini, kutokana na akinamama hao kujifungulia watoto hao katika maeneo yasiyo salama, hasa kwa wakunga wa jadi *(T.B.A)* ambao Serikali haijawaona hawa na kuwapa uwezo zaidi wa kumudu kazi zao.

Tunashauri Serikali iwaone wakunga wa jadi kwa kuwapa nyenzo za kufanyia kazi za usalama kwani sasa hutumia zana ambazo si salama. Tunafahamu kuwa wanawake karibuni 45% ya Watanzania hujifungulia watoto kwa wakunga wa jadi *(T.B.A.)* kwa sababu zifuatazo:-

(i) Wao ni rahisi, hawatozi bei kubwa ya kujifungulia, upande wa kanga, chumvi na sio pesa.

(ii) Wao wapo karibu na jamii wametapakaa maeneo mengi katika jamii. Kwa hiyo, wapo karibu kuliko hospitali au zahanati, zipo mbali na jamii.

(iii) Lugha yao nzuri na huzalisha kwa upendo.

Mwisho, watoto wasajiliwe wakati wanapozaliwa, kwani wanapata taabu sana wanapokuwa watu wazima kutaka kusoma au kuomba kazi kwani kitu cha kwanza wanaulizwa Je, una cheti cha kuzaliwa? Wengi wao wanakuwa hawana vyeti vya kuzaliwa! Kwa hiyo, tunataka uandikishaji wa watoto ni muhimu kwa shughuli za baadaye. Baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono tena mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii angalau kwa maandishi, hivyo basi nataka nianze kwa kusema kwamba idadi kubwa ya wananchi wa Tanzania ni wanawake. Ukiangalia takwimu zinazoonyesha kwamba asilimia 51ya wananchi ni wanawake. Kwa maana ushirikishwaji zaidi katika maeneo yote na hata katika ngazi ya maamuzi bado unahitaji kuboreshwa ili uendane na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu haijaweza kutoa fursa sawa pamoja na wingi huo wa jinsia hii. Mwanamke ni mtu anayenyanyasika kila mara kutokana na mfumo dume uliozoeleka wa mila, silka na tamaduni kwamba mwanamke hawezi na ndiyo maana hata fursa nyingi hunyimwa. Tunaomba Wizara kutoa taaluma zaidi kwa

wanawake ili waweze kuongeza vipaji vyao na kuweza kujua haki zao na kuzidai pale zinapokiukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kutoa 30% katika Bunge bado uwakilishi wao ni mdogo mno na kwa hiyo, hata Bunge lako hili Tukufu wanawake wakihitaji kupitisha jambo fulani linalowahusu wao basi haitakuwa rahisi kuweza kupitisha kwa vile idadi yao ni ndogo sana, haki sawa kwa wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wa Kitanzania wengi mno wanaishi katika mazingira magumu. Maisha hayo huwanyima fursa nyingi ikiwemo ile muhimu ya kupata elimu ambayo ndio ufunguo wa maisha. Naiomba Serikali kutoa kipaumbele kuwasaidia watoto hawa kuhakikisha wanapata elimu ili waondokane na unyanyasaji, kwani kukosa elimu ni unyonge wa milele na hilo humfanya mtu yeyote kudharaulika mbele ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu janga la UKIMWI ni tishio kwa Tanzania na duniani kote. Hivyo Wizara hii ina wajibu mkubwa kufuatilia kwa karibu sana kwani ni angamizo kwa nguvu kazi ya Taifa. Vijana wetu wanaendelea kuathirika kila uchao na hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kuiga tamaduni za nchi nyingine na kuacha mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kuweka sheria madhubuti ya mtu yeyote atakayebainika anatumia dawa za kulevya, kwani tunapopaka mkate siagi, basi tupake pande zote yaani tumuadhibu anayeleta na anayetumia la si hivyo Taifa linaendelea kuangamia. Nashukuru sana.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua Mkoa wa Kagera ulipatwa na janga la UKIMWI siku nyingi na kuwa na watoto wengi wanaokosa msaada, Wizara hii inawasaidiaje, Serikali hivi haioni kuwa wakati umefika kuweza kuwa na kituo cha Serikali cha kulea watoto hao kuliko kusubiri msaada na kuwafanyia mpango wa kuwawekea kituo cha kuwasaidia kama kilichokuwa Bukoba Mjini kilikuwa kinaitwa Bonabana. Kituo hiki kilikuwa kinasaidia sana kuwakusanya pamoja. Hata watu walivyokuwa wanajitokeza kusaidia ilikuwa ni rahisi sana. Hata jana nimechangia kwa Waziri wa Afya kuhusu watoto wa shule ya Mgeza viziwi, vipofu wale watoto yatima na wale wazazi wao hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Wizara haioni kwa sasa kwenda kutembelea vituo au shule hizo na kuweza kuwasaidia hao watoto kuna wanawake wengi wananyanyaswa kwa kutojua sheria. Kwa mfano, anakwenda Ustawi wa Jamii anazungushwa mpaka huyo mama anakata tamaa baada ya kupewa msaada inakua kumchezea, mpaka sasa mwanamke akipata shida kwa mume wake ukimshauri kwenda huko Ustawi wa Jamii anakataa kwa kuogopa kuzungushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu kwa Wizara hii ni kushirikiana pamoja, Mkoa huo unasahaulika sana, una matatizo mengi kuhusu Wizara yako ni watoto

wengi wanapa shida. Kama mnavyojua matatizo yale yalianzia huko. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Nawashukuru wapiga kura wangu kwa kunichagua kwa kura nyingi na nashukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili na kufanya kazi zake kwa ufanisi na ubora na kutuunganisha kuwa ndugu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake na kwa kusimamia suala la njaa. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuweza kutunga hotuba hii na wote walioshirikiana nao, pamoja na Kamati yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia hotuba hii, kwanza Wizara hii ya Jinsia inahusika na jinsia zote mwanamke, mwanamme au watoto wote wana haki sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuwashirikisha wanawake kwenye vyombo vya maamuzi kufikia asilimia 30 na kuongeza Mawaziri wanawake na kuchaguliwa pia Naibu Spika mwanamke hiyo ni historia kwa nchi hii. Lakini bado tunaiomba Serikali ifikie kutoa nafasi ya rasilimali 50% ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha Wizara hii imepewa bajeti ndogo sana kulinganisha na bajeti nyingine je, tutafika kuleta maendeleo? Shughuli zake ni nyingi za kuleta maendeleo kwa hiyo Serikali iangalie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake tunaiomba Wizara ya Fedha uanzishaji wa Benki hiyo haraka iwezekanavyo iharakishe ili wanawake waanzishe *SACCOS* na kuinua mtaji wa Benki hiyo ili nao wanawake wajikwamue katika maisha yao ili kuleta maendeleo, naiomba Serikali Benki hizo zipelekwe Mikoa mbalimbali wanawake wawe na ari ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna unyanyasaji wa kijinsia kwa mfano mume anaoa mwanamke na amezaa watoto wengi baadae bahati mbaya mume amefariki, jamaa wa mume wanamnyanyasa mke na watoto hao na kumfukuza ndani ya nyumba, je, huo si unyanyasaji wa kijinsia? Kwa hiyo, Serikali iangalie sheria kwa upana zaidi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara na kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia machache kwa lengo la kuishauri Wizara. Kuhusu uanzishwaji wa *SACCOS* za wanawake, nashauri Wizara ishirikiane kwa karibu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuhamasisha kwa nguvu kubwa uanzishaji wa uimarishaji wa *SACCOS* za wanawake katika ngazi ya kata. *SACCOS* imara ndizo zinazotazamiwa kuwa wanahisa wakuu wa Benki ya Wanawake inayotazamiwa kuanzishwa na kukamilika mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya Wizara, ingawa Bunge hili limekuwa likilalamikia ufinyu wa Bajeti ya Wizara hii, mabadiliko ya kuongeza kiwango cha fedha ni kidogo sana. Kuna haja ya Wizara kuendelea kujenga hoja yenye uzito zaidi kwa Tume ya Mipango sasa waone umuhimu wa Wizara hii kama Wizara ina kazi kubwa ya kuanzisha Benki ya Wanawake, kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* na vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii na kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii au ndio chachu cha maendeleo kuanzia ngazi ya kaya. Serikali ilione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria zinazowanyima wanawake haki, naipongeza Wizara kwa kuahidi kulivalia njuga suala hili. Pamoja na sheria zilizotajwa naomba kuikumbusha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuikumbusha Serikali na kuikumbusha kuidhinisha Itifaki ya Mapato kuhusu haki za wanawake wa Afrika yaani *Mapato Protocol* iliyosainiwa na nchi za Kiafrika Julai, 2003. Tanzania ni moja ya nchi za Afrika ambazo bado hazijaidhinisha Itifaki hii mpaka ilipofika tarehe 30 Juni, 2006.

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ambayo inajali na inatambua mchango wa wanawake, sasa muda umefika wa kulitekeleza hilo. Matatizo ya watoto yatima, naipongeza Wizara kwa kufuatilia maisha ya watoto yatima walio katika mazingira magumu. Nashauri Wizara iweke utaratibu wa kutembelea Shule au Taasisi za watu au Mashirika binafsi zinazoleta watoto hawa katika mabweni. Ni lazima Serikali iridhike kuona watoto hao wanapatiwa malezi ya kindugu, wanapewa matibabu mazuri, chakula na malazi bora. Hali katika baadhi ya vituo si nzuri. Baada ya ushauri huo mdogo. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia naishukuru Wizara hii kwa jitihada inazoonyesha katika kuboresha jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Mheshimiwa Sophia Simba, kuwa Waziri wa Wizara hii nyeti ya wanawake, jinsia na watoto ili aweze kuiongoza hasa ukizingatia mwanamke ni mtu muhimu katika jamii ya Kitanzania na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi naomba sasa nijikite zaidi katika suala zima la kumwezesha mwanamke, hasa katika suala la mikopo. Mikopo inayotolewa kwa mwanamke bado haikidhi mahitaji ya jamii hii kwani kiasi anachokopeshwa mwanamke ni kidogo kama shilingi 50,000/= mpaka shilingi 100,000/= haitoshi kwa biashara

inayotegemewa kumpa mafanikio mwanamke. Naomba Serikali iliangalie upya suala la viwango vya mikopo kwa wanawake angalau kiwango cha chini kiwe shililingi 500,000/= kwa mtu mmoja mmoja na kwa vikundi. Kiwango cha chini kiwe shilingi milioni moja laki tano. Hapa Serikali ikikubaliana na ombi langu itakuwa inawezesha wanawake kujikwamua na umaskini kulingana na mfumo mzima wa mfumuko wa bei wa bidhaa mbalimbali. Hivyo kuwapa kiasi kidogo cha mikopo kama shilingi 50,000/= na shilingi 100,000/= ni kumwongozea mwanamke mzigo tu bila kupata faida na kuwa ni mzalishaji wa vyombo vya fedha tu.

naomba pia Serikali iangalie sana tena kwa kina suala la hii mifuko ya uwezeshaji kama Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote na kadhalika itawanywe pote ili kutoa na kutenda haki kwa wanawake wote nchini, unakuta kwamba Mifuko ya uwezeshaji imekuwa hailingani na hivyo kujikuta kumekuwepo na hisia tofauti kwa watu hawa kuwa maeneo mengine ni bora na mengine si bora kitu ambacho hakifai kabisa naomba kiboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko hii ipelekwe mpaka kule chini vijijini ambako ndiko kuna wanawake waliochoka, wanahitaji kuinuliwa kimaisha hasa kielimu na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumwezesha mwanamke pia suala la riba katika vyombo vya fedha liangaliwe ili viweze kumsaidia mwanamke kutokana na mikopo atakayopata kwani sasa bado ni kubwa mno.

Mwisho, naomba Serikali kama kweli tumedhamiria kuwainua wanawake kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kuiwezesha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kiasi kikubwa cha fedha kulikoni kiasi cha sasa cha shilingi billioni kumi, milioni mia nne na kumi na nane, mia tatu hamsini na tano elfu. Fedha hizi ni kiasi kidogo mno kwa Wizara mama iboreshe bajeti ya mwaka 2007/2008. Nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Usimamizi wa Mirathi irekebishwe.

(b) Sheria ya mgawanyo wa mali kwa wanandoa bado haiko wazi, irekebishwe ili kuleta haki sawa kwa mwanaume na mwanamke. Mfano, kesi inapokuwa Mahakamani, mwanaume hubaki ndani ya nyumba wanayoishi na mali zote wakati wote wa kusikilizwa kwa kesi hali mwanamke akiendelea kukaa kwa ndugu zake au kwao kwa shida. Hali hiyo ni ya udhalilishwaji kwa mwanamke. Hivyo sheria irekebishwe.

(c) Sheria ya watoto wadogo ambao wazazi wao wametalikiana irekebishwe. Watoto wanaishi na mama hadi kufikia umri wa miaka 17. Kwani watoto hawa wanapobaki wa baba chini ya miaka sita au saba wanaathirika sana kimalezi na hasa watoto wa kike wafikiapo umri wa kuvunja ungo, baba hawezi kumsaidia mwanae. Sheria irekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wote huo wa kuwa kwa mama, baba aendelee kutoa matunzo kwa kila mtoto kwa kiwango cha asilimia fulani kutokana na mshahara au kipato cha baba kwa kila mtoto.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na kitengo maalumu cha kuhakiki na kutambua kesi zote za mirathi pamoja na ndoa zilizoko Mahakamani ili kufuatilia mwenendo wa kesi hizo na kukomesha kabisa vitendo vya rushwa na dhuluma kwa wanawake. Kwa hali hiyo kutakuwa na ukombozi halisi juu ya haki za wanawake katika masuala ya ndoa na mirathi.

Suala la watoto yatima na walioko katika mazingira magumu, Wizara ijenge Shule za Msingi katika kila Mkoa ili angalau kutoa elimu kwa wachache hasa walioko mitaani na kupunguza wingu la kulea Taifa la kesho litakalokuwa na tabia za kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa. Shule hizi zikijengwa, Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kama mtakubaliana nami, mimi niko tayari kuungana na Wizara kwa kuanza ujenzi katika Mkoa wa Singida. Nashauri wekeni kitengo, hakika tutaweza tu, ili tunusuru angalau wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Kuhusu wanawake, wanawake wanabeba jukumu kubwa sana kama kulea watoto, kusomesha na kuingoza nyumba kwa ujumla. Ni kweli usiopingika kuwa kina baba walio wengi wanazitelekeza familia zao, kitu ambacho mama hawezi kufanya. Hali za akinamama ni duni kiasi ambacho wanajiingiza kwenye matatizo ambayo matokeo yake ni chimbuko la gonjwa hatari la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wanajiunga na vyama mbalimbali vya kuweka na kukopa. Vyama hivi vimekuwa ni bugudha kwa akinamama, wengine wanashindwa kulipia mikopo wanayokopa na hatimaye kufikia kunyang'anywa vitanda, kabati, viti na kadhalika na kupelekea akinamama hao kuishi maisha duni baada ya kunyang'anywa vyombo vyao. Naiomba Serikali iwafikirie njia bora ya kukopa na kuweza kurudisha mikopo katika njia nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wale akinamama katika baadhi ya miji ambayo hali zao kiafya ukiziangalia ni watu ambao wanamudu kufanya shughuli mbalimbali za kuwaingiazia kipato. Akinamama hawa badala ya kutafuta riziki zao kwa kufanya shughuli kwa mikono yao, akinamama hao badala yake wanakuwa ombaomba na mara nyingi wanaitumia siku ya Ijumaa ndio siku yao rasmi ya kuomba.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupiga marufuku tabia hii ya ombaomba?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaorodhesha akinamama hawa omba omba na baadae kuwafanyia mpango wa kuwapatia maendeleo ili waweze kuanzisha kilimo cha mboga na mazao mengine ili waweze kujipatia vipato vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia hii ni aibu kwa nchi yetu kuona akinamama ambao ni wazima kiafya na umri unawaruhusu hufanya kazi mbalimbali lakini wanaamua kuwa omba omba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na nategemea kupata majibu ya maswali yangu niliyouliza wakati wa kipindi cha kujibu hoja.

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi wamezoea kwamba miradi yao ya kujiongezea kipato ni ile midogo midogo tu ya kujikimu. Nashauri, Wizara iimarishe wataalamu wanaoweza kuandika *project proposals* ili wanawake washiriki katika miradi mingine itakayowatoa katika kilimo cha kujikimu waingie katika kilimo cha kibiashara. Wataalamu waliopo vijijini hawana ujuzi wa kutosha kuandaa w*rite ups* zinazoweza kuwavutia wafadhili kutoa fedha. Mifano ya miradi ambayo nashauri vikundi vianzishe ni kama ifuatavyo:-

(a) Kukopa kutoka katika Mfuko wa Pembejeo za kilimo ili waweze kuuza mbegu, mbolea, dawa za kilimo na mifugo.

(b) Kukopa katika mfuko wa pembejeo au katika vyanzo vingine ili waanzishe *Women Tractor Hire Service Centres* zitakazohudumia wakulima wengi.

(c) Naamini yako maeneo mengi ambayo yanaweza kuwa ya manufaa kwa vikundi mbalimbali vya jamii. Tatizo ni utaalamu wa kuandaa miradi kitaalamu.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri jinsi alivyoweza kuiwasilisha vizuri hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, itakumbukwa kuwa katika hotuba ya Waziri Mkuu katika kipengele hicho kumetengewa shilingi 500,000,000/= kila Mkoa kwa ajili ya uwezeshwaji wananchi kiuchumi.

Ushauri wangu naomba Wizara iweze kushirikiana na Wizara kama hii huko Zanzibar ili fedha hizo ziweze kuwafikia wanawake Zanzibar ambao wana uwezo mkubwa wa kibiashara lakini huwa wanakwama kutokana na mitaji. Kwa vile lengo ni kumkwamua mwananchi kiuchumi, naomba na Mikoa ya Zanzibar iweze kufikiriwa katika fungu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhalilishwaji wa watoto, mara nyingi mijini na vijijini hutokea kesi kama hizo za udhalilishwaji wa watoto kijinsia katika vitendo vya ubakaji, lakini mara nyingi huwa kesi hizo zinapopelekwa katika vyombo vya sheria, kunakuwa na uzorotaji katika hukumu za kesi hizo.

Naishauri Serikali kuwa na ufuatiliaji mzuri wa kesi hizo kwani watoto wengi na wazee mitaani huwa wanalalamika kutokana na kutotendewa haki kwa mujibu wa sheria na hiyo hutokana na vitendo vya ulaji rushwa wahusika wa kesi hizo.

Kuhusu UKIMWI, naendelea kuishauri Serikali, vijijini na mijini wapo wanawake ambao wanaendelea kujificha ambao wameathirika na ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI. Wizara iendelee kuwahamasisha wanawake kujitokeza katika vituo vya ushauri nasaha na kupima afya zao, kama wameathirika au hawajaathirika. Wale walioathirika tuwahamasishe kuanzia vikundi vya kujiendeleza kiuchumi na kuweza kutumia dawa ili kuweza kuishi kwa matumaini. Bila shaka wale wanaoendelea kujificha watavutika na kuweza kujitokeza na kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuweke mikakati kabambe kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kuweka vituo vya muda vijijini na mijini kwa madhumuni ya kutoa semina na vituo vya ushauri nasaha kwa wanawake ili kuondoa uoga katika familia mbalimbali.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimuombe Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ni msimamizi mkuu wa haki na maendeleo ndani ya jamii zetu nchini ni vyema Wizara iende sambamba na mazingira ya wazee na watoto kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi zito katika maisha duni humfikia mzee na mtoto jambo ambalo humpelekea mzee kumlea mtoto kwa kumtegemeza ili mtoto aishi kimategemeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hili, sasa wakati umefika Serikali ya awamu ya nne itekeleze mazuri yote na iachane na kutoa maelezo katika makaratasi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumkomboa mwanamke mmoja katika umaskini ni kusema umewakomboa watu kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia hali ya watoto nchini mwetu utaona wanaishi kama hawana wazee. Hii iko wazi kama Wizara hii itafanya sensa nyumba hadi nyumba utaona waajiriwa katika nyumba ni watoto wadogo sana. Matendo haya sio mazuri kwani humpelekea mtoto kukosa elimu pia na kufanyishwa kazi asizo na uwezo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee ana haki kubwa juu ya mtoto wake asiye wake kumsimamia katika malezi, kumsomesha pia na kumpa huduma. Kwa kuwa mwanamke ni mwenye majukumu makubwa pale ambapo ndani ya jamii kuna utofauti wa mke na mume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana ndoa inapovunjika mzigo mkubwa hubebeshwa mwanamke. Nyumba ikikosa maji, moto, kuni, mtoto anaumwa yote haya hutupiwa mwanamke. Iko haja sasa Serikali iwatazame kwa jicho la rehema wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhiki juu ya mwanamke, kuna mila ya kukeketwa kwa mwanamke, jambo hili ni la mila, ambalo linadhalilisha heshima ya mwanamke na kubakwa kwa wanawake. Tatizo hili ni tishio kubwa kwani hupelekea mwanamke kupewa maradhi kwa nguvu. Ni vyema Serikali ikomeshe mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa wanawake, ipo haja ya Serikali itoe taaluma kwa akinamama pale ambapo watapatiwa msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, pia Wizara hii ipo haja ya kuwapa taaluma akinamama, wanawake mara nyingine wao wenyewe hujidhalilisha kwa biashara ya mwili sio biashara nzuri. Ni vyema Serikali ipige vita magenge ya ukahaba mijini.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Katibu Mkuu Bibi Mariam Mwafisi, wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kutoa matumaini kwa wananchi wa Tanzania.

Baada ya pongezi hizi natarajia kuchangia hoja katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jukumu la Wizara ni kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika mipango na miradi ya maendeleo itakayofaidisha wananchi wote Tanzania. Hili ni jukumu kubwa na la msingi. Hata hivyo, napenda kupata ufafanuzi wa jinsi Wizara inavyotoa maelekezo kuhusu ushirikishwaji wa wanaume na wanawake wenye ulemavu katika uhamasishaji na uwezeshaji huo. Nimeomba ufafanuzi huo kwa sababu huko katika ngazi za Wilaya na vijiji kundi hili la jamii bado linatengwa kwa kudharauliwa, hivyo yafaa Wizara itoe mwongozo mahususi ili walemavu nao wafaidike katika kuwezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hoja za Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Wanawake nchini. Ni kweli mchakato wake unachukua muda mrefu sasa na daima Serikali ikieleza kuwa mtaalamu anafanya uchambuzi tangu mwaka 2004, yafaa sasa Wizara ihimize zaidi juu ya suala hili kwa vile wanawake kila tunapowaeleza sisi Wabunge wanaona kama tunawadanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo kutokana na fedha za Wizara na Halmashauri, kwa muda sasa mikopo toka mfuko wa wanawake na vijana watu wenye ulemavu bado hawajafaidika kwa sababu hawaelekezwi wala kuhamasishwa kufahamu taratibu zinazotumika ili kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwamba kundi la jamii ya watu wenye ulemavu lishughulikiwe kwa kutumia mikakati maalum kwa sababu wana matatizo maalum na kwa kiasi kikubwa wanasahaulika katika nyanja nyingi za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo naunga mkono hoja hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza napenda, kumshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa kutembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chisalu na kuona mazingira, majengo ya chuo hicho kuona vitendea kazi na pia kuzungumza na wafanyakazi wa chuo hicho kilichopo Wilayani Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Chisalu kina matatizo yafuatayo:-

(i) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya uendeshaji ni kidogo sana. Bajeti hiyo iongezwe.

(ii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa majengo.

(iii) Serikali iboreshe vitendea kazi kama vile gari, trekta, kuweka umeme wa gridi ili Chuo hicho kiweze kutumia kompyuta na vifaa vingine vya kisasa.

(iv) Serikali iweke mikakati ya kuboresha mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo yanayotolewa hayaendani na karne. Vyuo vipatiwe walimu wenye taaluma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maendeleo ya Jamii, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo kwenye kata kwa kuwapatia mishahara mizuri, vitendea kazi, pikipiki na kadhalika? Pia Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza Maafisa hao kitaaluma? Kwa kuwa fedha inayotengwa na Serikali kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya akinamama ni kidogo sana, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mikopo? Je, Halmashauri za Wilaya ngapi zinadaiwa mchango wa asilimia kumi na ni kiasi gani zinadaiwa Halmashauri hizo? Je, marejesho ya mikopo hiyo ni kiasi gani na asilimia ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika kikao cha leo cha Bunge tukiwa wazima na afya njema. Namwomba Mwenyezi Mungu atuzidishie uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kuandaa sera, kuzisimamia, kuziratibu pamoja na kutathmini utekelezaji wake. Wizara iandae utaratibu wa kuwashirikisha wananchi wote katika maendeleo ya jamii. Wizara ijenge uwezo kwa wananchi wote ili waweze kushiriki katika utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo kwa faida yao wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itoe taaluma kwa jamii itakayojenga imani kwa jamii hiyo kuwapatia watoto haki yao ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kutobaguliwa pamoja na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itoe taaluma kwa wanawake juu ya kuweka na kukopa ili waweze kuitumia mikopo hiyo kwa kufanya biashara zitakazowaletea tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iwapatie usafiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ili waweze kufika vijijini kwa wanawake walio wengi kwa kutoa taaluma kuhusu mikopo na akiba na namna gani ya kuitumia mikopo hiyo iweze kuzalisha na kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna matatizo mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia kuna matatizo ya utumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa vijana wetu, rushwa, ujambazi, ubakaji na kadhalika, chanzo cha matatizo hayo na mengine mengi ni kutokuwajibika ipasavyo kwa watendaji wanaohusika katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mikakati mbalimbali iandaliwe ili kukabiliana na matatizo niliyoyataja mfano umeoneshwa katika kupambana na suala zima la ujambazi hapa nchini. Ikiwa ujambazi umeweza kuondolewa au kupunguzwa kwa kiasi kikubwa na mengine yaliyobakia yanawezekana pia, lililobakia ni uamuzi tu. Penye nia pana njia.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napongeza hotuba nzuri ya Wizara hii ambayo ina mipango mizuri ya kuhakikisha ukombozi na ustawi wa maendeleo ya wanawake, jinsia na watoto.

Vile vile napenda kukiri kwamba uongozi mkuu wa Wizara hii ambao unaongozwa na Mheshimiwa Sophia Simba, kweli ni pambazuko jipya la nuru ya tumaini kwa maslahi ya ustawi wa maendeleo ya wanawake, jinsia na watoto hapa Tanzania.

Aidha, leo napenda kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, ambaye ni kiongozi mwenye nuru na bashasha ya wito wa kupenda jamii na kupenda kujituma kutumikia wanawake, wanaume na watoto bila ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwapongeza watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazotenda kwa maendeleo ya wanawake Tanzania. Wahenga husema kila ndege hupenda kujisikia anajiimbia wimbo ili kiajifariji kwa shida zake. Kwa kutambua hii Wizara ni Wizara mtambuka, naomba Wizara hii inisaidie kusadiki pana juhudi na jitihada za kupambana na mauaji ya imani potofu za uchawi wa wakongwe. Wahenga husema umoja ni nguvu na Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Maswa tupo tayari kuibua matembezi ya vijana ya kuamsha mapinduzi ya fikra dhidi ya imani potofu za kusababisha mauaji ya vikongwe kwani vijana wa leo ndio vikongwe wa kesho. Je, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wapo tayari kuratibu na kusimamia azma na maudhui ya vijana wa Maswa ambao ndio vikongwe wa kesho waibue nguvu ya umoja ya kuzaa uvumbuzi wa hoja asilia za mila za kumaliza mauaji ya vikongwe?

Je, Wizara itakuwa tayari kushirikiana na Mbunge wa Jimbo na uongozi wa Serikali wa Wilaya ya Maswa kwa yeye Waziri kutumia hao wafadhili wa Wizara mfano *NGOs* ili wafaulishe kutoa michango ya dawa na vitendea kazi kwa vituo vyao ili tupambane na maradhi yanayotibika hospitali ili jamii waondokane na tiba za ramli? Wahenga husema muungwana hajibu swali bila kuulizwa swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kuhusu kusadikisha mapinduzi ya fikra za desturi potofu kwa mila na utamaduni potofu wa leo ambao unaongozwa na mfumo dume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, uwezeshaji wa kujenga uwezo vijijini wa kuibua miradi kwa wanawake utafaulishwa vipi na Wizara hii ili tusifadhaike ndani ya jamii hii hasa kwa wanawake wa Maswa ambao mradi wao ni kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kale waliwaasa vijana kwamba chagua mwenza kabla ya kilevi, aidha, walisema taarabu sio bustani ya haiba ya mwandani wa maisha.

Baada ya utangulizi wa nasaha za wazee wetu sasa naiomba Wizara hii ituarifu kama ina utafiti wa kutueleza kuhusu hao wenye kusema ubaya wa wanaume, je, ni wangapi wapo katika maisha ya ndoa kuepusha Taifa kuwa ni mapokeo ya taarifa ya hasira binafsi za tabia binafsi dhaifu za kujenga maisha ya ndoa hadi udhoofu ukawa huruma kwa wanawake wanaotamba kwa raha zao na waume zao?

Mheshimiwa Mwenyekiit, je, wanawake ni wangapi wakipata fursa ya madaraka wanaridhia kuteka mimba? Je, Wizara hii ina mpango gani wa kuendeleza makungwi ili washauri vema maandalizi ya ndoa kwa kutambua msingi wa kungwi wa elimu ya leo ni kauli ya ushauri mwema hupatikana juu ya mchango

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushauri kwa maswali haya kwa sababu kila jambo na mbegu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kufikiri ni tofauti na kuelewa, mashaka ni hasara ya kutopata maarifa, naiomba Serikali iboreshe mtaji wa mitaji kwa wanawake kwa sababu mtaji wa utajiri ni utajiri wa mbegu za utajiri.

Naiomba Serikali isikie kilio cha akinamama, tupate malinganisho ya faraja kwa wanawake na wanaume kwa sababu ukuni na ukuni huivisha chungu.

Naomba kuhitimisha kwa kuwapongeza wote wale waliochagia. Kweli kila ngoma ina hadithi yake. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye msemaji wetu wa mwisho wa leo jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niwatangazie kwamba viongozi wa Kambi ya Upinzani wako kwenye Kikao Maalum na kwa nafasi hiyo jioni ya leo nimeletewa taarifa kwamba Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum ndiyo anakaimu nafasi hiyo ya Kiongozi wa Upinzani ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Sasa baada ya kumtambua Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama naye ameniambia kwamba ana mgeni wake Katibu wa Chama cha Mapinduzi Msaidizi wa Wilaya yake. Naomba tuendelee na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitamuita sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aanze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa huruma na upendo wake kwake na kwetu sote, naomba azidi kuniongoza niweze kumudu kazi hii kwa ujasiri, hekima, busara na unyenyekevu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa dhati ya moyo wangu napenda nimshukuru sana mume wangu mpenzi Bwana Othman Masoud Othman, kwa kunitia nguvu, kunifariji na kunishauri kila mara, upendo wake umenifanya niweze kukabiliana na changamoto za kazi hii kwa utulivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Sophia Simba, kwa ushirikiano wake na uongozi wake mzuri. Aidha, namshukuru sana Katibu Mkuu Mariam Mwafisi, wataalam wote wa Wizara bila kumsahau msaidizi wangu wa masuala ya Bunge, Ndugu Paul Eranga na dereva wangu Ndugu Abdulinur Kirua, kwa ushirikiano wao mkubwa na kunielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi na Wanawake wote wa Mkoa wa Arusha hususan UWT kwa kunipa ridhaa yao ya kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Ninachoweza kusema ni kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri, katika kuwapongeza viongozi wote katika nafasi mbalimbali walizopata kuanzia Mwenyekiti wetu mpya wa Chama cha Mapinduzi, Katibu Mkuu na Sekretarieti nzima. Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika, viongozi wote wakiwemo Wakuu wa Wilaya wote walioteuliwa hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupongeze sana wewe binafsi siyo tu kwa sababu ni Mwenyekiti wa Shughuli za Bunge na kwamba unaendesha kikao hiki bali zaidi kwa nafasi yako kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kupitia kwako nashukuru sana Kamati nzima kwa michango na maelekezo yao ambayo yameboresha kwa kiasi kikubwa hotuba yetu na mipango mbalimbali ya ndani ya Wizara yetu. Vile vile nawashukuru sana Kamati kwani mmenipa elimu kubwa ya jinsi ya kutekeleza MKUKUTA kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nina dakika trakriban 13 sasa naomba nijielekeze katika kujaribu kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa humu Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kujielekeza katika zile hoja ambazo zimechangiwa kwa maandishi. Kwa jumla hoja ambazo zimechangiwa ama kwa hotuba zilizotangulia au zilizochangiwa kwa maandishi ama kwa kuongea humu Bungeni zinaweza zikagawanywa katika maeneo makuu matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, ni hali ya Wizara kumudu majukumu yake kwa maana ya ufinyu wa bajeti na eneo la pili, uwezeshaji wa wanawake kwa kuwapatia fursa mbalimbali za mikopo, mafunzo, masoko na kadhalika pamoja na sheria mbalimbali zinazohusu wanawake na watoto.

Eneo la tatu, ni masuala ya watoto hasa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu na eneo la nne, ni masuala ya maendeleo ya jamii kwa maana ya wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, majumba ya maendeleo ya jamii, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vile vya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano, ni utendaji na uratibu wa baadhi ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali yaani *NGOs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu kwa ujumla hoja hizi hasa zile zilizochangiwa kwenye bajeti zilizotangulia pamoja na baadhi za zile zilizoandikwa kwa maandishi na Mheshimiwa Waziri wangu ataendelea kupitia hoja zote zitakazokuwa zimebakia. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangu Mawaziri na Naibu Mawaziri waliotangulia katika Wizara hii, nao ni Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Kate Kamba, Mheshimiwa Kijazi Kyelula, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Mheshimiwa Shamim Khan, kusema kweli wamejenga misingi imara imetufanya nasi kuendelea tukiwa na dira na mwelekeo thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa njia ya kipekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuitetea Wizara hii, na hata pale ilipobidi kuboreshwa zaidi kwa kubadilisha mwelekeo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, na kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wengi mlisimama kidete kutetea hoja na kuunga mkono. Ushahidi wa kuiva kwenu kama wanajinsia unajidhihirisha sio tu katika namna Waheshimiwa Wabunge wanawake na wanaume wanavyochaguliwa humu Bungeni katika nafasi mbalimbali na nje ya Bunge, lakini pia kuna mfano mzuri ni kama vile wewe Mheshimiwa Mwenyekiti ulivyokubaliwa vizuri na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Mwenyekiti wenzako Mheshimiwa Job Ndugai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuiva huku kunadhihirishwa pamoja na maswali na michango inayotolewa humu Bungeni kwani imekuwa kawaida sasa kwa Waheshimiwa Wabunge wanaume kuhoji masuala yanayohusu ukatili dhidi ya wanawake au watoto au unyanyasaji na udhalilishaji wa wasichana katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile Waheshimiwa Wabunge wanawake kwa upande wao tumewasikia wakihoji mambo mbalimbali ya jamii kwa ujumla hata wakapendekeza kwamba Benki ya Wanawake itakapoanzishwa washirikishwe na

wanaume. Kwa hivyo, haya yote yanaonyesha kuiva kwetu sisi kama wanajinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika hali ya Wizara kumudu majukumu yake kwa maana ya ufinyu wa bajeti, tumepata michango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi sana, tunapenda kwa dhati ya moyo wetu tuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walioweza kutetea Wizara yetu ili iweze kuongezewa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara hii ina majukumu mengi na yanahitaji fedha za kutosha. Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya Wizara hii kidogo kidogo kwa mfano, mwaka 2005/2006 bajeti yetu ilikuwa shilingi bilioni 8.3. Mwaka 2006/2007 bajeti yetu ni shilingi bilioni 10.3. Hata hivyo tunakiri kwamba mahitaji halisi ya Wizara hii si chini ya bilioni 18 kwa upungufu na tukitaka tuendesha shughuli zetu vizuri, basi tunahitaji shilingi bilioni 34. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wote kwa ujumla wao, lakini wale ambao walipata nafasi ya kuchangia katika kuweza kutetea hoja hii ya bajeti ni pamoja Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na wengine wengi ambao Mheshimiwa Waziri wangu ataweza kuwataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wa wanawake kwa kuwapatia fursa mbalimbali za mikopo, mafunzo na masoko na kadhalika. Suala kuu lilikuwa ni uanzishaji wa benki, kwa nini Benki inachelewa au inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na kulithibitishia kwamba Wizara inajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu tuweze tukaanzisha Benki hii mwaka huu kama tulivyoahidi. Waziri wangu ameweza kuzungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na tumeweza kupata ahadi kwamba Serikali inaweza ikatenga fedha ya mwanzo ya kuanzisha Benki hii katika kipindi hii baada ya kuweza kufanya marekebisho ya bajeti.

Aidha, majadiliano ya Wizara pamoja na Benki ya Dunia yanaendelea na yanaendelea kwa vizuri baada ya kuwa na mazungumzo nao na kufanya *video conference* hapo juzi. Lakini lengo kubwa tunachotaka kufanya ni kuhakikisha kwamba Benki hii mara itakapoanza basi itakwenda katika ngazi ya vijijini na kuwafaidisha akinamama wengi walioko katika vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikupongeza sana wewe mwenyewe binafsi kwa ushauri wako wa kutaka tuzitumie *SACCOS* hizi tuweze kupitisha fedha zetu ili ziwafikie akinamama wengi walioko vijijini. Nasi tunasema Benki itakapoanza itaanza kama *Non Financial Institutions* yaani Mfumo ule wa Benki ya Posta ambao hauna hundi kwa kuanzia na mtaji wake ni mdogo wa shilingi milioni 500. Tutaanza hivyo

kidogo, lakini tutatumia zile *SACCOS* zetu kuweza kuwafikia akinamama wengi walioko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatumia basi mtaji wa Benki ya Dunia kukuza Benki hii na ikawa na mtaji mkubwa ili akinamama waweze kupata mikopo mikubwa na sio shilingi 50,000/= au shilingi 100,000/= kama wanavyopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la masoko kwa bidhaa za wanawake. Napenda nilieleza Bunge hili Tukufu kwamba Wizara yetu kwa mara ya kwanza kwa ushirikiano na Balozi wa Zimbabwe tuliweza kuwaalika wanawake wafanyabiashara kutoka Zimbabwe kuja kushiriki katika Maonyesho ya Sabasaba na lengo ilikuwa ni kuwa na utaratibu wa kutoa fursa kwa wanawake wa Tanzania na sisi waweze kushiriki katika maonyesha ya biashara kwenye nchi zingine za Kiafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ambaye ametaka sisi tuweze kuwasaidia akinamama wa Wilaya yake iliyoko mpakani mwa *Lake Nyasa* wanaotengeneza vyungu na Waheshimiwa Wabunge wengine akina Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Fatma Mikidadi wote wa maeneo hayo ya Kusini kwamba tutatumia fursa hii muweze nanyi mkawashawishi akinamama wakatengeneze bidhaa zenye hadhi ili na sisi tuwapeleke akinamama wetu wakafanye maonyesho yao katika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mafunzo ya miradi kwa ajili ya akinamama. Kwa ujumla wanawake wanapatiwa mafunzo ya ujasiriamali na hata tutakapoanzisha Benki hii kuna *component* au kipengele ambacho kinahusu ujasiriamali na hilo litazidi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile napenda niwapongeze na niwashukuru sana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wametaka sisi tuweze tukaliangalia suala zima la mikopo hii ya maendeleo ya wanawake yaani *WDF*. Nimpongeze Mheshimiwa George Lubeleje, kwa njia ya kipekee, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Cynthia Ngoye, kwa ushauri wao kuhusu asilimia kumi ambayo inapaswa kila Halmashauri iweze kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa tutamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati ili basi Halmashauri ziweze kuchangia asilimia kumi bila ya *excuses* zozote. Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru yupo hapa na anatusikiliza na *inshallah* tutazidi kuongea naye na tutamwomba na ni msikivu tutaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa ushauri wa Mheshimiwa Christopher Chiza, ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na wengine tunawashukuru vile vile kwa michango yao. Lakini napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Christopher Chiza kwamba ushauri wake wa kutaka akinamama tuwahusishe katika miradi ya kilimo tumeuchukua na tumeupokea na sisi Wizara yetu tutashirikiana naye ili kuhakikisha kwamba akinamama na wenyewe wafanya miradi ya kuweza kuuza pembejeo na vifaa vingine.

Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, alielezea kuhusu uwezeshaji wa wananchi yaani wanawake na vijana kupata fedha za wastani wa milioni 500 kwa kila Mkoa, akihoji kwamba fedha hizo zitafika Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa vile Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alikuwa anahimiza uwezeshaji wa wanawake na alipita Tanzania nzima ikiwa ni mpaka Zanzibar na Pemba tutaongea na Waziri Mkuu na wengine kwa vile Wizara yetu ni mjumbe katika Kamati hiyo ya Uwezeshaji ili kuhakikisha kwamba basi akinamama wa Zanzibar na Pemba wanapata fursa hii japo wastani sio lazima ifike hiyo milioni 500, lakini wastani kulingana na eneo na watu waliopo kule. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zingine zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na masuala ya watoto na hasa watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu. Watoto kwa ujumla wanagusa katika Wizara zote. Sisi tunakiri kwamba tutaendelea kuratibu kwamba watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu wanapata haki zao za msingi ikiwemo elimu, afya na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wetu wakati wa hotuba yake ya kuzindua Bunge mwaka jana, hadi sasa mpango wa kazi tumeshauandaa na tumeanza kwa kushirikiana ambao utakuwa umepangiwa na fedha za kuweza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, kwa ushauri wake wa kuanzisha mfuko kwa ajili ya watoto yatima. Wizara tumeupokea ushauri huu na tutauweka katika mikakati yetu ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kupitia Bunge hili Tukufu ya kuyapongeza mashirika binafsi, taasisi za watu binafasi wote waliosaidia watoto kama vile *Geita Goldmine, VODACOM, CELTEL, Tanga Cement, CRDB* na mengine mengi ikiwa ni pamoja na baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vina uchungu mkubwa na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo napenda kutoa rai kwa makampuni yote nchini kujilenga katika kuchangia mfuko huu mara tutakapouanzisha. Mchango wenu kwa watoto hautakuwa na nongwa kama mtakavyochangia maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa basi muda wangu unakaribia kwisha naomba nimshukuru sana Bibi Rose Kaaya maarufu kama Mama Jordan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kunilelea wanangu wakati mimi niko Bungeni na baba yao akiwa kazini Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najua adha na changamoto kubwa wanazozipata akinamama na akinababa wanapokuwa mbali na familia zao kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na niwaombe kwa unyenyekevu mkubwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtuunge mkono.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi ya kwanza kabisa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja hapa Bungeni leo jioni. Napenda kuchukua nafasi pia kuwashukuru sana Wabunge wote waliochangia na wale ambao hawakuchangia. Wale waliochangia kwetu sisi ni changamoto kubwa kwa Wizara yetu. Tumeona kwamba michango yao inatujenga zaidi na tutaienzi kama ilivyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia katika hoja hii ni wengi. Kwa mara ya kwanza wamefikia zaidi ya 50 kwa kauli na kwa maandishi. *(Makofi)*

Ningependa niwatambue wale waliochangia kwa kauli kama ifuatavyo, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Joyce Massunga, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Maria Hewa, MheshimIwa Charles Keenja, nampongeza sana kwa kutuunga mkono kwa kuwa yeye ndiyo peke yake Bungeni mwanamume ambaye alichangia. Amezingatia vizuri jinsia pamoja na Mheshimwa Bujiku Sakila, kwa hiyo, Wabunge wawili na Mheshimwa Faida Mohamed Bakar. *(Makofi)*

Aidha napenda kuwashukuru Wabunge waliochangia kwa maandishi ambao wanafikia idadi yao kuwa 41. Naomba niwatambue kama ifuatavyo, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Zainab Vulu, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dorah Mushi na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia masuala yanayohusu Maendeleo ya Jamii wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Mkiwa

Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Janet Kahama na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe radhi kwa kweli kwa sababu kwa kweli wapo Waheshimiwa wa jinsia ya wanaume wengi wamechangia kwa maandishi, lakini wale waliochangia kauli walikuwa wawili. Kwa hiyo, naomba niombe radhi na nawashukuru sana kwa michango yenu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyobainishwa hapo juu hoja yangu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi katika maeneo tofauti. Hata hivyo maeneo yafuatayo yamepatiwa michango mingi zaidi. Moja ya maeneo ambayo yamechangiwa sana ni ufinyi wa bajeti. Ya pili ni hali mbaya ya vyuo kwa namna ya majengo na miundombinu, vitendea kazi na watumishi. Pia imezungumziwa uhaba wa watumishi wa Maendeleo ya Jamii kuwa ni wachache, waliokuwepo na kutothaminiwa na kuwezeshwa vya kutosha. Pia imezungumziwa uwezeshaji wa wanawake hususan katika mikopo, uanzishwaji wa Benki ya wanawake na jambo lingine ambalo limezungumzwa sana ni kuhusu watoto yatima na watoto wa mitaani na kwa ujumla watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Nitajaribu kuzitolea ufafanuzi hoja hizo na nyinginezo na pia kutokana na ufinyu wa muda zile ambazo hatutoweza kuzijibu tutazitolea ufafanuzi kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kujibu hoja iliyotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii hapa Bungeni. Jambo la kwanza ambalo lilitolewa na Kaimu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Othman Ali. Katika hoja zake nimechagua zile ambazo zinahitaji maelezo lakini nyingi ambazo ametoa ni za kuboresha na tunamshukuru sana kwa kuwa mstari wa mbele wa kutaka kuhakikisha kwamba Wizara hii inapewa kipaumbele ili kutimiza malengo yake kikamilifu. *(Makofi)*

Moja amezungumzia kwamba mfuko wa akinamama Wizara itenge fungu kupitia mfuko wa akinamama ili kuvipa nguvu vyama vya akiba na mikopo kwa *agenda* maalum ya kuwakopesha wanawake. Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kuwa wapo wanawake wasiofikiwa na wadau wa nje, waelimishwa na Idara. Swali lake la kwanza ilikuwa Wizara ijenge mpango maalum kupitia Halmashauri ili wanawake wasiofikiwa na wadau wa nje waelimishwe na Wizara. Aidha, majumba ya maendeleo yafufuliwe kwa kazi hiyo. Nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuwa wapo wanawake wasiofikiwa na wadau wa nje. Wizara inaendelea na jukumu la kuwaelimisha wanawake wanaokopa kwa Halmashauri kwa jinsi hiyo Wizara itashirikiana kwa karibu zaidi na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa wanawake wasiofikiwa sasa wanafikiwa. *(Makofi)*

Pia alizungumzia kuwa litengwe fungu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuvipa nguvu vyama vya akiba na mikopo kwa *agenda* maalum ya kuwakopesha wanawake. Sisi tunakubaliana na ushauri wa Kamati kuwa suala la vyama vya akiba na mikopo iwe ni *agenda* maalum ya kuwakomboa wanawake. Tathmini ya

*WDF* imependekeza kuwa tuwakopeshe wanawake fedha za Mfuko wa Wanawake yaani *WDF* kupitia vyama vya kuweka na kukopa, hivyo Wizara italifanyia kazi kwa kuzingatia ushauri huo. Tunaamini kwamba katika vile vyama itakuwa rahisi kuwafuatilia na kwa kuwapa mikopo hii tutatoa nguvu zaidi katika zile *SACCOS* ambazo wamezianzisha. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo wamelizungumzia ni kuhusu suala linalosema kwamba Serikali ifute sheria ya kuwafukuza watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni. Nakubaliana na ushauri wa Kamati kuhusu kufutwa kwa sheria hiyo kama ilivyofanywa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilikwishaanza mchakato wa kushughulikia suala hilo. Suala hili ni suala ambalo bado lina uzito wake na kwamba katika Mikataba ya Kimataifa ambayo sisi Tanzania tuliridhia mmoja ni wa haki ya mtoto. Mkataba ule unamtaka kila mtoto apate haki ya kusoma. Kwa hiyo, hata mtoto ambaye amepata mimba ana haki ya kurudishwa shule na kusoma.

Kwa hiyo, sisi tukishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tuko katika majadiliano ya kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza hawa watoto wakarudishwa shuleni kama vile wenzetu Zanzibar walivyoweza kutunga sheria ambayo sasa watoto waliopata mimba wanaweza kwenda shuleni. *(Makofi)*

Kamati pia ilisema Serikali itenge fedha za maendeleo zaidi katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi. Ni kweli suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na kwamba Wizara itaufanyia kazi ushauri wa Kamati kwa kutenga fedha za maendeleo zenye fungu la kutosha kwa mwaka ujao kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa mwaka huu kulikuwa na ufinyu wa bajeti kwa hiyo, haikuwezekana lakini tutajitahidi kwa mwaka ujao kuufuata ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachuo wa Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi wanaojifunza masomo ya ufundi wapewe kipaumbele kwa kazi za ukarabati. Ushauri huu umekuwa ukitolewa kwenye Bodi za Zabuni ngazi za Wilaya zenye vyuo na tayari baadhi ya Wilaya zimeanza kutekeleza mfano wa Wilaya hizo ni kama Nkansi, Kilwa, Kisarawe na kadhalika. Kwa vile vijana wanaofundishwa katika vyuo hivi pia wanapata mafunzo ya ufundi ni vyema Wilaya zetu, Halmashauri zetu zingeweza kuwapa kazi ndogo ndogo za ufundi ili kuinua hali ya maisha ya hawa vijana ambao wanapata mafunzo katika vyuo hivi badala ya kutafuta watu wa kujenga ambao wanatoza fedha nyingi na pia inaigharimu vyuo fedha nyingi katika ukarabati. *(Makofi)*

Kamati pia inazungumzia kuhusu viongozi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi wawe wabunifu. Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati na kuanzia mwaka 2002 Wakuu wa Vyuo wamekuwa wakihimizwa kuanzisha miradi ya uzalishaji mali iliyo endelevu pamoja na kuanzisha mafunzo yanayoongezea uzalishaji mali kwenye vyuo. Baadhi ya vyuo vimefanikiwa kutokana na ubunifu kiasi cha kujiendesha na kujitegemea kiasi kikubwa. Vyuo hivyo ni kama Monduli, Ilula, Same, Mbinga, Singida, Gera, Ifakara, Njombe na Kisarawe vimeweza kujiendesha kwa asilimia 50 na wengine kujifanyia ukarabati wa baadhi ya majengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa hapa niwakumbushe Wabunge kwamba vyuo hivi vya wananchi ni vyuo vya wananchi hasa kwa hiyo, Halmashauri nazo ziwe makini kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinapatiwa kazi ambazo zitavifanya zijitegemee zenyewe. Kwa hiyo, ni vyema Wakurugenzi wa Halmashauri wangeweza kuwaongeza nguvu vyuo hivi ili viwe chemchem ya kuleta maisha bora kwa wananchi wanaowazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni kwamba Wizara iweke mkakati wa kuboresha maisha ya walimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kama nyumba nzuri na kuwapatia malipo ya mazingira magumu ya kazi. Wizara inakubaliana na ushauri wa kuweka mkakati wa kuboresha maisha ya walimu. Kwa wakati huu Wizara inaboresha mazingira ya vyuo kwa kutenga fedha nyingi zaidi za ukarabati wa majengo zikiwemo nyumba za kuishi walimu. Aidha, Wizara itawasiliana na Ofisi ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusiana na ulipaji wa posho ya mazingira magumu kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliendelea kuzungumzia kuhusu elimu itolewe kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu umuhimu wa kutumia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na sisi kama Wizara kwa kweli tunashirikiana na TAMISEMI ili tuweze kuandaa mafunzo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ili waweze kuelewa na kuwatumia vizuri Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuwapatia usafiri Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Ushauri huu pia umezingatiwa na Wizara imepanga kununua pikipiki 15 kwa mwaka huu kwa ajili ya matumizi ya Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Aidha, utaratibu huu utaendelezwa hadi Halmashauri zote zipate pikipiki. Kamati pia ilizungumzia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wawe na mawasiliano ya moja kwa moja na Wizara. TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii washirikiane kwa karibu sana ili kuboresha utendaji kazi wa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI itaweka mfumo wa mawasiliano utakaowezesha Wizara kupata taarifa za utekelezaji wa kazi za Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa urahisi zaidi na kutoa mrejesho *(feedback)*. Suala hilo hata Mheshimiwa Rais amelizungumzia na ametuagiza Wizara zote tufuatilie Maafisa wetu huko katika Wilaya. Kwa hiyo, na sisi kama Wizara nyingine tupo katika mchakato wa kuanza kuhakikisha kwamba tunakuwa karibu sana na Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika la *SELF* linalotoa misaada ya jamii ya Watanzania ambalo liko chini ya Ofisi ya Rais liwe chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa vile wasimamizi wakuu wa *SELF* wako chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Ushauri huu umepokelewa na Wizara itawasiliana na Ofisi ya Rais ili kuona uwezekano wa Shirika hili kuwa chini ya Wizara yangu. Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inashauri Wizara kuweka mikakati itakayowezeshwa kukusanya maduhuli kama inavyokadiriwa.

Ninawashukuru kwa ushauri wa Kamati, Wizara ina jukumu la kuhakikisha kwamba inakusanya maduhuli kama ilivyokadiriwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2006 Wizara yangu imekusanya maduhuli ya shilingi 18,155,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Ni mategemeo yangu kuwa tutaweza kukusanya maduhuli ya shilingi 25,000,000 kama ilivyokadiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye hoja ya Kamati ya Upinzani. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, alikuwa na mengi sana ya ushauri na tunamshukuru sana kwa hotuba yake kwani ametupa changamoto na tutayachukua mengi ambayo yatatusaidia katika utendaji wetu wa kazi. Yeye anasema upo umuhimu wa kuwa na chombo huru cha wanawake na kwamba Serikali haitaki kuanzisha chombo hicho. Hapana! Lakini nakubaliana naye na msemaji kwamba upo umuhimu wa kuwa na chombo cha wanawake. Hata hivyo Serikali haina hofu ya kuanzisha chama hicho, ndiyo maana kuanzia mwaka 2002 mpaka 2004 Serikali iliwezesha mchakato wa uanzishwaji wa chombo hicho ambacho ilionekana kuwa kuna umuhimu wa kusubiri kwanza maamuzi ya Shauri la Baraza la Wanawake Tanzania (BAWATA) lililoko Mahakamani hadi leo. Hivyo kwa sasa ilionekana kuwa kuna umuhimu wa kuimarisha Wizara ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa hiyo, hicho chombo kesi itakapomalizika basi tutaanza kukifuatilia tena kwa vile ni Serikali yetu ndiyo iliyotaka chombo hiki kiwepo tokea mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa maendeleo hayalingani na fedha zinazotolewa. Hata hivyo fedha sio kipimo pekee cha maendeleo. Wizara imekuwa ikitoa mafunzo kwa wanawake wajasiriamali ili kubadili fikra na kuongeza ujuzi. Hizo zote zikiwa ni jitihada za kumkwamua mwanamke kiuchumi. Hii ni kutokana na swali lake analouliza kwamba tangu Serikali ianze kutoa fedha kwa ajili ya wanawake, je, maendeleo yanalingana na fedha zilizotolewa?

Pia Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, alisema kwamba Sheria ya Mirathi ya Kimila ya mwaka 1963 na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni kero kubwa na zimepitwa na wakati. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa zipo sheria zilizopitwa na wakati na zimekuwa kero kwa jamii na kwa sababu hiyo Serikali ikishaanza mchakato kufanyia marekebisho sheria hizo zikiwemo Sheria za Mirathi na Urithi, Sheria ya Ndoa na Sheria zinazohusu masuala ya watoto. Sheria hizi ziko Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuandaa Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa akiwasilisha hotuba yake hapa alizungumzia sheria hizi na alisema zipo katika hatua nzuri na kwamba tutegemee kwamba sheria hizi zitakuwa zimefanyiwa marekebisho au kutungwa upya kwa muda mfupi sana. Vile vile Mheshimiwa Rais alisisitiza hilo wakati alipokutana na wananchi Dar es Salaam alisisitiza kwamba sheria hizi sasa zimepitwa na wakati na anataka kuona mabadiliko katika sheria hizi.

Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, alizungumzia pia kuwa fungu litolewe kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanaokeketa na wanaokeketwa. Napenda kuchukua nafasi hii

kumuondolea wasiwasi Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu fungu lililotengwa kwa ajili ya kutoa elimu na wanaokeketa na wanaokeketwa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inalo jukumu la kuhamasisha jamii wakiwemo wakeketaji na wanaokeketwa kubadilisha fikra zao ili kuacha mila zote zenye kuleta madhara ukiwemo ukeketaji, kazi hiyo hutekelezwa na Maafisa wetu wa Ugani wa Maendeleo ya Jamii waliopo katika ngazi mbalimbali hapa nchini. Aidha, katika mikutano ya mwaka inayoendeshwa na Wizara kuhusu ukeketaji baadhi ya wakeketaji waliotangaza kuacha ukeketaji hualikwa pamoja na wasichana waliokeketwa ili kutoa ushuhuda na hivyo kuwatia moyo wasichana wengine wakatae chachu ya kushawishi wale wanaoendelea kukeketa. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuelimisha jamii wakiwemo wanaokeketa na wanaokeketwa ni shillingi milioni 15,266 ambazo ziko katika vifungu mbalimbali vya *sub-vote* 3002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee sasa kwa kujibu hoja kwa Wabunge kwa mafungu kama nilivyosema mwanzo. Kwa sababu hoja ni nyingi kwa hiyo nitazijibu kufuatana kwa mafungu. Nitaanza na hoja inayohusu Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mheshimiwa Devota Likokola alitaka kujua taarifa na tafiti za *NGO* kuwa hazijadiliwi na Halmashauri na hata haziingizwi kwenye Pato la Taifa ili wananchi wajue na kuona zinafanya nini. Pia alitaka kujua kanuni na taratibu za kuanzisha *NGO* hazifahamiki vizuri kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Devota Likokola, ni kweli taarifa ya tafiti za *NGO* hazijaanza kujadiliwa na Halmashauri na tathmini zake kuingizwa kwenye Pato la Taifa. Napenda kumjibu Mheshimiwa Devota Likokola, kuwa Sheria ya *NGO* namba 24 ya mwaka 2002 imeanza kufanyiwa kazi rasmi mwaka 2005 baada ya kanuni zake kupitishwa mwaka 2004. Hivyo kufikia Juni, Julai mwaka 2006 tumeanza kupokea Taarifa za mwaka za kwanza kwa Mashirika yanayoendelea kujisajili chini ya Sheria hii. Lengo likiwa ni kutathmini mchango wa *NGO's* hizi katika Pato na Maendeleo ya Taifa kwa ujumla ili wananchi waweze kufahamu *NGO's* hizi zinafanya nini. Kadhalika Wizara yangu imeandaa orodha ya *NGO's* zote zinazojisajili chini ya Sheria ya *NGO's* na kuzitenga katika ngazi zake husika kama vile Wilaya, Mkoa, Taifa na kuainisha sekta mbalimbali ambayo *NGO* imejikita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeshatoa mafunzo ya awali kwa wasajili wasaidizi ambao ni Maofisa Mipango Mkoa na Makatibu Tawala wa Wilaya katika Mikoa na Wilaya zote ili waweze kueneza elimu hii kwa wananchi katika ngazi zao. Maofisa wangu wanaendelea kutembelea na kuhakiki utendaji kazi wa *NGO's* hizi mkoa kwa mkoa na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Devota Likokola kuwa Mkoa Ruvuma utapewa kipaumbele na wanawake watahamasishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma Mikidadi, naye alizungumzia kuhusu *NGO* nyingi ziko Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Arusha, Moshi, Iringa, Mwanza. Amesema tunataka *NGO's* zilizosajiliwa zielekee mikoa ya Kusini. Aidha, Wizara ichukue fursa ya makusudi kuwapa mafunzo mikoa ya pembezoni kuanzisha *NGO's* zao mikoani badala ya kungojea *NGO's* za Dar es Salaam, tunakubaliana na Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Ni kweli *NGO's* nyingi ziko mijini. Wizara yangu imeanza Utekelezaji wa Mpango wa

kuzipenyeza *NGO's* hizi Wilayani na Vijijini kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishwaji wa *NGO's* hizi. Wizara yangu inaendelea kutoa mafunzo na ushauri kuhusu umuhimu wa kuanzisha *NGO's.* Mpaka sasa Makatibu Tawala wa Wilaya zote na Maafisa Mipango wa Mikoa yote wameshapatiwa mafunzo kuhusu uanzishaji, uenezi na sheria za *NGO's.*

Mheshimiwa Esther Nyawazwa naye pia amezungumzia *NGO's,* yeye anasema kuna *NGO's* zinazosaidia kutoa misaada kwa wanawake, zinazosimamiwa na wanawake wenyewe kwa kutoa elimu, kusaidia sheria zinazodhalilisha wanawake na watoto. *NGO* hizi sasa zihame mijini na zielekeze elimu vijijini. Nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Esther Nyawazwa zipo *NGO's* nyingi zinazotoa misaada kwa wanawake na kusimamia wanawake wenyewe mfano *MEWATA, TAWLA, TAMWA, TGNP* na nyingi nyinginezo ambazo kwa kweli ni sasa tu zinajaribu kwenda kwenye miji mingi. Hapo mwanzo zote zilikuwa Dar es Salaam lakini kama *NGO* ya Wanasheria Wanawake sasa hivi wana matawi yao sehemu nyingi za nchi hii ikiwemo pamoja na Dodoma. Wizara yangu ipo katika jitihada za wazi kuhakikisha *NGO's* hizi zinatoa huduma zake vijijini kwa mfano *MEWATA* imeendelea kutoa huduma katika Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, naye pia amezungumzia kuhusu Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Yeye anasema *NGO's* zinazosaidia wanawake zinashindwa kutoa taarifa je, kuna *NGO* ngapi zimetoa taarifa. Tunakubaliana na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo kuhusu utoaji wa taarifa wa *NGO's* kwa mujibu wa takwimu usajili wa *NGO's* chini ya Sheria ya *NGO* namba 24 ya mwaka 2002 ambao ulianza rasmi mwaka 2005 ni *NGO's* 83 ambazo zimewasilisha taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye kipengele cha jinsia. Wapo Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumzia kuhusu masuala ya jinsia. Mheshimiwa Juma Said Omar, wa Jimbo la Mtambwe anazungumzia kwamba Wizara itoe taaluma kwa wanawake juu ya kuweka na kukopa ili iweze kutumia mikopo hiyo kwa kufanya biashara zitakazowaletea tija. Ninapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kuwapatia wanawake mafunzo ya ujasiriamali. Kwa kuzingatia hilo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake kabla ya kupatiwa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Devota Likokola nao pia wamezungumzia mfuko wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* kwa vile viwango vinavyotolewa ni vidogo. Ni kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba fedha za mkopo ni kidogo na viwango vinavyotolewa pia ni vidogo. Wizara imeliona hilo ndiyo maana imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wanawake kuanzisha vyama vya ushirika vya kuweka na kukopo na inaendelea katika mchakato wa uwanzishwaji wa Benki ya Wanawake kama ilivyoelezwa vizuri sana hapa na Mheshimiwa Naibu wangu. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa ni muhimu wanawake wawezeshwe na kupatiwa mafunzo mitaji na waelimishwe kuhusu sera ya maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha kiuchumi Wizara imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, jinsia na uongozi kwa kushirikiana na wadau wengine kuimarisha mifuko na mikopo. Aidha, Wizara imeanza kuwapatia mafunzo dawati la jinsia ngazi ya Halmshauri na Mkoa ambayo yatawasaidia kuwaelimisha kuhusu Sera ya Maendeleo ya Wanawake na jinsia na masuala mengine yanayohusu masuala ya jinsia. *(Makofi)*

Suala la unyanyasaji wa wanawake, wajane kutolewa kwenye nyumba, wakati waume zao wakifariki limezungumzwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, pamoja na Mheshimiwa Martha Mlata. Masuala ya unyanyasaji wa wanawake wajane yote haya yanaangukia katika sheria zetu za mirathi na sheria hiyo kama tulivyozungumza inafanyiwa marekebisho lakini pia ningependa kuiasa jamii kuona umuhimu kwamba wanawake wamechangia katika kipato chochote ambacho kimepatikana wakati wa ndoa.

Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa wanawake hawa wanabakia katika nyumba ambazo wamejenga na waume zao na wanakuwa na mali zile ambazo wameacha waume zao. Lakini tunaamini katika sheria ambayo inatungwa mambo yote hayo yatazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimwia Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum alizungumzia sheria zilizopitwa na wakati zinazomdhalilisha mwanamke na mtoto zirekebishwe. Kama nilivyosema Serikali inafanya marekebisho, katika kurekebisha sheria ya ubakaji. Wizara yangu inaendeleana na kuwasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu kuzifanyia marekebisho sheria zote zinazokiuka haki za binadamu hasa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, wanataka kujua kuwa tutafikaje asilimia ya 50 ya wanawake wawakilishi katika ngazi ya maamuzi. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa inahitajika mikakati maalum ya kuhakikisha kwa asilimia 50 ya wanawake katika ngazi za uongozi inafikiwa. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika siasa kutoa elimu ya uongozi, jinsia na kuhamasisha jamii ili kutambua uwezo wa wanawake katika kutoa maamuzi kutoka ngazi ya familia hadi Taifa. Kwa kutumia mikakati hii pamoja na mingine nina imani kuwa tutafikia asilimia 50 tukiwa pamoja na wenzetu akina baba na nadhani watakubali kwamba wanawake sasa tufike asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Mfaki, anazungumzia kuanzisha *SACCOS* ambazo zinaweza zikawa chanzo kikubwa kuanzishwa Benki. Nakubaliana na Mheshimiwa Mariam Mfaki kwamba *SACCOS* zinaweza kuwa chanzo kikubwa cha kuanzisha Benki ya Wanawake. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba *SACCOS* hizi zitaimarishwa ili hapo baadaye ziweze kukopa fedha kutoka Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, alizungumzia kwamba ni lini na kwa utaratibu gani wajasiriamali wa Ludewa watafikiwa kabla ya kupewa mikopo. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi kuwa wanawake huwa

wanapatiwa mafunzo kabla ya kupewa mikopo. Mafunzo haya huwa yanatolewa na Maafisa Maenedeleo ya Jamii ngazi ya Halmshauri ikiwa ni pamoja na Halmashauri ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi ni mjumbe katika Halamshauri hii hivyo atahamasisha mafunzo haya na mikopo hii ifike katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Elizabeth Batenga anauliza Benki ya Wanawake itaanzishwa Dar es Salaam? Je, wanawake watafaidika? Mahali benki itakapoanzishwa itategemea sana na hadidu za rejea ambazo huwekwa na kamati ya usimamizi. Benki ya Wanawake itawanufaisha maskini kwani kutakuwa na uhamasishaji katika ngazi zote.

Mheshimiwa Ania Chaurembo, anazungumzia mzigo wa kazi kwa wanawake, elimu itolewe ili kuwapunguzia kazi wanawake. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wanawake wana mzigo mkubwa. Aidha, sera ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia inaelekeza namna ya kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake. Aidha, Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia ambao unasisitiza usawa wa jinsia katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sera ziko na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Wilaya na ngazi za Kata wanazielewa. Mheshimiwa Mbunge, Sera hii unaweza ukaipata ili uweze kuzidi kuwaelimisha wanawake katika eneo lako. Mheshimiwa Joyce Machimu alizungumzia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wanawake kama vile mfuko wa fursa sawa kwa wote upelekwe hadi ngazi za chini ili kuwanufaisha wanawake.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wanawake wote wanufaike na mifuko ya uwezeshaji. Napenda kueleza kuwa mifuko kama hiyo ni ya Vyama Visivyo vya Kiserikali ambavyo hufanya kazi kulingana na uwezo wao wa kifedha. Aidha, Serikali inachukua hatua ya kuwafikia wanawake wote kupitia maafisa wa maendeleo ya jamii. Narudia tena tuwatumie Maafisa Maendeleo ya Jamii ili watuelekeze jinsi ya kufikiwa na mifuko hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, alizungumzia mikopo katika Mkoa wa Kigoma. Akinamama wengi wanakipato kidogo au hawana kipato chochote je, Serikali inawasaidiaje? Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya wanawake wa Mkoa wa Kigoma wanapatiwa Mkopo ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kupitia Halmashauri ya Kibondo, Kasulu, Kigoma, Ujiji na Kigoma Vijijini. Kila Halmashauri ilipatiwa fedha za Mfuko huu shilingi milioni 800 kwa kipindi cha mwaka 2001/2002 na 2002/2003. Aidha, mafunzo yametolewa kwa Maafisa Maendeleo ngazi za Halmashauri ya kuhamasisha wanawake kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa. Kama wakirudisha mikopo hii ni dhahiri wataongezewa, watapata mikopo mingine kutoka *WDF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie suala lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge nalo ni kilio cha Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Joyce Masunga, alizungumza kwa uchungu sana kuhusu upungufu wa watumishi katika chuo cha wananchi Buhangija. Ni kweli kuwa Wizara inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti na kama ilivyobainishwa na Mwenyekiti wa Kamati wa Maendeleo ya Jamiii wakati ikiwasilisha maoni ya ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa maendeleo ya jamii.

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mkakati wa Wizara wa kupunguza tatizo la uhaba wa watumishi umeanza kuzaa matunda kwa kupata kibali cha kujaza nafasi 35 zilizoachwa wazi baada ya kuacha kazi, kustaafu na kufariki. Aidha, mwaka 2006/2007 Wizara imeidhinisha ikama ya ajira 72. Matumaini yetu kuwa kwa mwenendo huu Wizara itaweza kupunguza upungufu mkubwa wa watumishi vyuoni ikiwemo chuo cha maendeleo ya wananchi Buhangija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Joyce Masunga alizungumzia kwamba vyuo vya maendeleo ya wananchi vya Mkoa wa Shinyanga vina hali mbaya. Ni kweli Wizara inakubaliana na Mheshimiwa Joyce Masunga kuwa vyuo vya wananchi nchini kote ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Shinyanga vina uchakavu mkubwa wa majengo pamoja na uhaba wa vitendea kazi.

Aidha, Wizara inatambua uhaba mkubwa wa watumishi na ukosefu wa vyombo vya usafiri kwenye vyuo vyote kikiwemo chuo cha Buhangija. Hata hivyo Wizara umejiwekea mkakati wa kukarabati vyuo kikanda ambapo katika mwaka wa fedha 2006/2007, chuo cha Malampaka cha Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa vilivyopangwa kufanyiwa ukarabati. *(Makofi)*

Kuhusu upungufu wa watumishi Wizara inaendelea kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kupata kibali cha kuajiri. Ushauri wa Wizara kutumia fedha za maendeleo ya mwaka wa fedha 2006/2007 kujenga vyuo viwili tu. Hayo yote yamezungumzwa na Mheshimiwa Joyce Masunga. Hata hivyo Wizara inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Joyce Masunga, kujenga vyuo viwili tu. Hata hivyo mkakati wa Wizara ni kuimarisha vyuo vilivyopo kwa njia ya kuvikarabati kikanda badala ya kujenga vyuo vipya. Kwa hiyo, hivyo vyuo pengine kama kutatokea utaratibu mwingine wa kujenga vyuo itawezekana lakini kwa taratibu za Wizara yetu sisi tumepanga tukarabati vyuo vilivyopo tunaamini gharama yake itakuwa ndogo. Vile vile fedha hizi shilingi milioni 253,571ambazo zimepangwa kwa ajili ya vyuo vyote ni kidogo sana kuwezesha ujenzi wa vyuo viwili vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Wizara kutafuta mfadhili wa kukarabati chuo cha Buhangija ili kukifanya kiwe cha Kimataifa. Wizara inakubaliana sana na ushauri wa Mheshimiwa Joyce Masunga kuhusu kutafuta mfadhili kwa ajili ya chuo cha Buhangija wakati huu ambapo Wizara inaendelea kukarabati vyuo vyake kikanda.

Vyuo vingi vina wafadhili na kwa njia hiyo vyuo vingi ambavyo vina hali nzuri ni vile ambavyo vimepata ufadhili wa wenzetu vyuo rafiki kutoka nchi nyingine. Kwa hiyo,

sidhani kama jambo hili litakuwa gumu kwa vile litakuwa linafanana na yale mengine. Ushauri mwingine ambao ameutoa, amenialika kutembelea Shinyanga kuona vyuo vyake, niko tayari kwenda kuangalia vyuo vya Shinyanga pamoja na kwenda kufuatilia mauaji ya vikongwe ambayo yanaendelea huko Shinyanga. Kwa hiyo, nitaweza kupiga ndege wawili kwa jiwe moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, alitoa maoni yake tu ni kuhusu vitendea kazi hususan vyombo vya usafiri na mawasiliano na kutothaminiwa kwa wataalam wa maendeleo ya jamii. Suala hilo limezungumzwa na watu wengi, ukosefu wa vitendea kazi husasan vyombo vya usafiri na kutothaminiwa wataalam wa maendeleo ya jamii. Waliozungumzia suala hilo ni Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba na Mheshimiwa Charles Keenja pamoja na Mheshimiwa Dorah Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kuwa wataalam wa maendeleo ya jamii hawana vitendea kazi muhimu vya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Hata hivyo jukumu la kuwawezesha watumishi wote wa Halmashauri kinyezo, usafiri, kompyuta, *OC* na kadhalika ni la Halmashauri, kwa sababu hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge wazihimize Halmashauri kuhusu umuhimu wa kazi za watumishi hawa na hivyo kuwatengea rasilimali zinazohitajika. Aidha, Wizara yangu inalo jukumu la kuwaendeleza watumishi hao kitaalam na ndiyo maana tunatenga asilimia 60 kila mwaka za nafasi za wanaojiunga na chuo cha Tengeru kwa watumishi wa Halmashauri. *(Makofi)*

Vile vile Wizara inapopata uwezo wa kifedha itaendelea kusaidia kutoa vyombo vya usafiri kama pikipiki. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya rejea kwa watumishi wa vikosi vya ujenzi na mafunzo ya ufundi vijijini na pale inapowezekana kuwapatia vitendea kazi, ni imani yangu kwamba watumishi hawa wakiwezeshwa watatekeleza majukumu yao ipasavyo bila kusukumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo nadhani wote tunakubaliana kwamba Halmashauri wanajukumu kubwa la kuhakikisha kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii. Wanapatiwa ruzuku ya kufanyika kazi pamoja na vitendea kazi ili waweze kufanya kazi zao vizuri kama wanavyofanya maafisa wengine wa kada nyingine wa Halmashauri hizo. Mheshimiwa Zaynab Vulu, alizungumzia kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuwajengea makazi mazuri wazee wetu ambao watatunzwa vyema na Serikali hadi maisha yanapoisha hapa duniani, Serikali yetu inawajali vipi wazee?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahili kwamba wazee wetu ni hazina yetu kuu kwa maisha yetu wazee wana hekima, busara na vipaji ambavyo bado tunahitaji kuvitumia. Katika kujali maendeleo ya wazee, Wizara yangu imeweka wazi katika sera ya maendeleo ya familia inayowasilishwa katika Kamati ya Baraza la Mawaziri. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine itahamasisha jamii na hasa familia kuwapenda kuwajali na kuwatunza wazee ndani ya familia. Nadhani hili halina ubishi, wazee wengi tumelelewa, tuwajali wazee wetu na sisi nadhani tutaendelea na hilo. Serikali itashughulikia wazee wachache, ambao kwa kweli

wana matatizo maalum. Lakini kwa ujumla wazee kama tunavyosema wanabusara na tunahitaji busara na hekima zao basi tuendelee kuwalea ndani ya familia. Wale watakaobainika kuwa hawana watu wa kuwatunza tutahamasisha Serikali za vijiji, jamii kuandaa kutekeleza mipango ya kuwatunza wazee ndani ya vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla alizungumzia kipengele cha 62, kuhusu dhamira ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii ya kukamilisha mitaala katika kukiweka chuo cha Tengeru kutoa mafunzo ya Shahada katika mwaka wa masomo 2006/2007. Utoaji wa Elimu ya Shahada ni sehemu ya Elimu ya Juu na chombo pekee husika katika taratibu ni Tume ya Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Aidha, suala hili tutalizungumza na Mheshimiwa Waziri ili tufuate utaratibu na kwa vyovyote Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kisingeweza kundelea kuwa Chuo Kikuu mpaka kipitie mikondo yote ya sheria ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Devota Likokola, Mhesimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Joyce Masunga wote walizungumzia uchache wa watumishi wa maendeleo ya jamii na mafunzo ya rejea kwa wataalam wa maendeleo ya jamii. Mafunzo yatolewe kwa Mikoa mingine.

Nakubaliana na maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii kwamba kuna uchache wa watumishi wa maendeleo ya jamii. Kwa mfano Sera ya Maendeleo ya Jamii inaelekeza kuwepo kwa watumishi walau mmoja katika kila kata lakini ni asilimia 40 tu ya kata zote Tanzania Bara zenye watumishi hao.

Aidha, sekretarieti tisa za Mkoa hazina washauri wa maendeleo ya jamii. Kwa kuzingatia upungufu huo Wizara yangu imeendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo katika vyuo vya maendeleo ya jamii kama ilivyoonyeshwa katika *paragraph* ya 12 na 61 mpaka ya 65 ya hotuba yangu. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtazihamasisha Halmashauri ili ziwaajiri wataalam hao pindi wanapohitimu mafunzo vyuoni. Nakubalina na Kambi ya Upinzani kuwapa mafunzo rejea watumishi wa vikosi vya ujenzi kwa Mikoa yote. Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo hayo kila mwaka hadi tutakapokamilisha Mkoa yote.

Katika suala la maendeleo ya jamii Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, naye pia amezungumzia Wizara kusaidia chuo cha Gera kupatiwa umeme. Wizara inakubalina na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala kuhusu umuhimu wa vyuo vya maendeleo ya wananchi kuwa na umeme na uhakika. Kwa wakati huu Wizara imeanza kuvijengea mitambo ya umeme unaotokona na nguvu za jua *(Solar Power)* vyuo vyote vinavyotumia *generator* na vile ambavyo viko mbali na njia ya umeme wa *TANESCO*. Hatua itakayofuata ni kuunganisha vyuo hivyo na *TANESCO* hapo njia zitakapofika katika maeneo yao kikiwemo Chuo cha Gera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi alizungumzia kuhusu mmomonyoko wa maadili miongoni mwa watoto, kuongezeka kwa kasi mwenendo na tabia mbaya, ukosefu wa adabu baina ya watoto, vijana na watu wazima. Vitendo vya uhalifu rushwa, ubakaji, ngono na UKIMWI. Nakubalina na mtoa hoja Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna mmomonyoko wa maadili miongoni mwa watoto, vijana na hata watu wazima. Inabidi tujiulize chanzo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu. Mimi naamini kwamba mmomonyoko huu ni matokeo ya malezi na matunzo mabaya ya watoto wetu ndani ya familia zetu. Baadhi ya wazazi na walezi hawaonyeshi mfano mzuri kwa familia zao. Baadhi ya wazazi na walezi wanatabia mbaya ya ulevi, uvivu, uzururaji, lugha na matendo machafu hivyo watoto wanaziona na kuiga tabia hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema kwamba mtoto umleavyo ndiyo akuavyo. Katika kutafuta tiba ya mmomonyoko wa maadili Wizara yangu imeandaa sera ya maendeleo ya familia itakayohamasisha maendeleo ya familia na jamii na hasa familia kutekeleza malezi bora, upendo, uadilifu, adabu na heshima wao kwa wao na wengine katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikiwataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuna Waheshimiwa ambao nilisahau kuwataja ambao ni Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaingia hatua inayofuata ambayo Katibu atatuambia baada ya kuomba muongozo wake. Ninaomba sasa niwahoji kwanza kwa hatua hii na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzingatie muongozo nilioutoa leo saa nne asubuhi na saa saba mchana, tafadhali sana naomba tujielekeze katika vifungu kulingana na hoja tulizonazo. Tusitumie mshahara wa Waziri kama ndiyo ngao ya mambo yetu yote hatutafika kwenye *Development Book* na hiyo itatufanya tusiende kwa utaratibu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 53 - Wizaya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... ... ... 2,938,178,000/=*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 53, programme 10, sub vote 1001, item 250100,* Mshahara wa Waziri.

Kwanza nataka anisaidie jina sahihi la Wizara yake kutokana na Kitabu hiki cha pili, (viii) imeandikwa *Ministry of Community Development, Women Affair and Children.* Lakini ukija ukurasa 186 imeandikwa *Ministry of Community Development, Gender and Children*, kwa hiyo anipe usahihi ni lipi kati ha hayo.

Swali la pili hivi sasa kuna malalamiko mengi sana, misaada inayotolewa kwa watoto yatima haifiki na *statistics* za watoto yatima, *population* yao kiasi gani haijulikani. Je, Waziri ana utaratibu gani wa kutumia maafisa watendaji wa vijiji na mitaa ili wafanye sensa ya nyumba kwa nyumba tujue watoto hawa ili haya mashirika yanayotoa misaada hasa hizi *NGO's* tuweze kuzifuatilia kuona kweli zinafika kwa watoto au hazifiki?

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Waziri u-*concetrate* na hilo la pili. Kwa sababu hilo la kwanza Mheshimiwa Mbunge nafikiri ni *typing error* kwa sababu inajionyesha, fungu lenyewe hasa tunapofungua ukurasa ule wa 185 imeandikwa iko sawasawa na kwa sababu tunataka kupitisha fungu hilo hatuangalii huko kwingine. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ujibu hilo la pili.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake kuhusu watoto yatima kwamba misaada haifiki. Misaada ya watoto yatima mingi inakuja chini ya *NGO's*. Sisi Wizara katika vijiji ambavyo vina maafisa maendeleo ya jamii tu wataweza kujua upatikanaji na jinsi misaada hii inavyokuja na ndiyo maana tunasisitiza kwamba kila kijiji kila kata kiwe na afisa maendelo ya jamii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge namshauri akirudi Jimboni kwake aihamasishe Halmashauri yake ihakikishe kwamba wanakuwa na maafisa wa maendeleo ya jamii na hawa maafisa maendeleo ya jamii kwa sasa wanatusaidia kwa vile idara ya *NGO's* iko chini ya Wizata yangu na hawa maafisa maendeleo ya jamii wanaratibu shughuliza za *NGO's* katika maeneo yao ambayo wanashughulikia. Kwa hiyo, ni kweli hili ni tatizo ambalo wote tunatakiwa tusaidiane jamii isaidie pia watu wasitumie majina ya watoto yatima kwa kujinufaisha. Hata hivyo Idara yangu inakusanya *data* ili kujua ukubwa wa matatizo haya ili kutafuta dawa ya kutatua matatizo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzingatie tu, kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshalijibu hilo lilitakiwa liulizwe kwenye kifungu kinachohusu maendeleo ya watoto na tuna fungu linalohusu hizo *NGO's*. Naomba tuwe waangalifu. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kupata ufafanuzi kuhusu maswali ambayo nilikuwa nimemuulizia. Niko katika Fungu la 53, *Programme 10, Subvote 1001, 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu niliuliza Wizara hii kwamba itachukua hatua gani katika kuweza kuhakikisha kwamba matatizo ambayo watoto yatima wamekuwa wakiyapata katika ngazi mbali mbali, yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, nina swali lingine la pili, katika hotuba ya Rais wakati akifungua Bunge letu Jipya alisema yafuatayo, nanukuu: "Serikali itachukua hatua za kuhakikisha kuwa watoto yatima wote nchini wanapata fursa za kupata elimu pamoja na huduma za afya. Nitataka Wizara nitakayaoiunda kusimamia masuala ya watoto iwasilishe Serikalini katika muda mfupi ujao mpango endelevu wa kushughulikia mahitaji ya kundi hili linaloongezeka katika jamii yetu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua utekelezaji wa agizo hili, kwa sababu alisema kwamba Wizara hii iwasilishe ndani ya muda mfupi. Napenda kupata maelezo kwamba muda mfupi katika Wizara hii unamaanisha muda gani?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumesema suala la *Children Development* haliko katika fungu hili, liko pale mbele. Kuna fungu 3002, ndiyo *Child Development*. Sasa naomba tuendelee kwanza na fungu linalofuata. Waheshimiwa Wabunge, naomba tujali ule utaratibu ili tuendelee kujipa mazoezi zaidi.

**MHE: ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na maelezo yako mazuri, naomba nisubiri kifungu kinachohusika ndiyo nitasimama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zaynab Vulu, kwa kuzingatia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003-*Community Development College,Tengeru 300,160,700/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Gender Development ... ... ... ... ... ... ... ... ... 735,254,300/=*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu naona ametupeleka mbele kidogo. Tulikuwa tupo Ukurasa wa 186. Sasa sasa hivi amekwenda kwenye Kifungu 3000 ambacho kipo ukurasa wa mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungeomba tufuate ile tulivyotoka kwa sababu tulikuwa kwenye *Vote 53, Programme 10, Subvote 1001.* Sasa huko tuliko kwenda ni kwingine, mbali sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Killimbah, nashukuru. Katibu alizingatia suala la *Child Development*. Naomba Katibu turudi tufuate utaratibu wa *votes* kama zilivyojipanga.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts ... ... ... ... ... ... ... ... 252,732,100/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning ... ... ... ... ... ... ... ... .... 188,260,600/=*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo kwenye *Vote 53*, ukurasa wa 187, *Vote 53, Subvote 1003,* Kifungu 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi. Katika maelezo yangu ya asubuhi, niliomba kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukumbuke kwamba katika mishahara ya watendaji, Bunge halina majukumu ya kudhibiti mishahara ya watendaji. Mshahara wenye mamlaka ni ule wa Mheshimiwa Waziri tu. Mheshimiwa Mbunge, nafikiri huu ndio utaratibu ambao Kanuni inatuongoza, hatudhibiti mshahara wa mtendaji katika *vote* hizi. Sasa fungu hilo ni fungu la mtendaji, tena sijui ni mtendaji wa nini, maskini pale. Kwa hiyo, ninaomba tuendelee na kifungu kinachofuata.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nangoja kifungu kinachofuata. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Training and Folk Dev.Colleges ... ... ... 2,313,982,100/=*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 53,* programu ya 20, *subvote* 2001, *Item* 310500, magari na mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa nne mwaka huu, Mheshimiwa Naibu Waziri alipata nafasi ya kutembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu**.** Tunamshukuru sana kwa kutembelea Chuo hicho. Alipofika pale alisomewa risala na tatizo mojawapo ilikuwa ni usafiri, gari lilikuwa juu ya mawe na waliomba shilingi milioni nne ili waweze kukarabati gari hilo liweze kufanya kazi. Pamoja na kwamba tumepatiwa pikipiki moja, tunashukuru, lakini katika bajeti ya mwaka 2006/2007 zimetengwa shilingi milioni 30. Sasa nataka nifahamu, je, shilingi milioni 30 ni pamoja na hizo shilingi milioni nne ambazo Meneja wa Chisalu aliomba kutengeneza gari ili liweze kufanya kazi? Naomba nithibitishiwe kama shilingi milioni nne zilizoombwa na Chuo cha Maendeleo Chisalu, zipo hapa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Lubeleje, naomba kukupongeza sana. Hapo umekwenda kwa utaratibu ambao unatakiwa kabisa. Nakupongeza. Mheshimiwa Waziri, naomba majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matengenezo ya gari katika Chuo chao, Naibu Waziri alilifikisha Wizarani. Kwa manufaa yake na wapiga kura wake na wanafunzi wa pale, ningependa kumfahamisha kwamba tutalifikiria katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na jibu. Watafikiria au watatenga hizo shilingi milioni nne katika kipindi hiki kwa ajili ya kutengeneza gari hilo? Kwa sababu suala la kufikiria ina maana kwamba hilo suala halijazingatiwa bado. Sasa, je, hizo shilingi milioni nne zitatengwa kwa ajili ya kutengeneza gari hilo? Naomba jibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni kufikiria ama ni kutenda?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zitapatikana! *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 53, Programme 20, Subvote 2001,* Kifungu kidogo 260800 *Training Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni fungu ambalo tunalitegemea sana katika Vyuo vyetu vilivyoko huko kwa wananchi vya kutoa elimu ya kutosha. Mwaka 2005/2006, waliidhinishiwa shilingi milioni 45, leo mwaka huu zimepungua sana na ndio elimu tunaitaka ya wananchi wetu wapate kutoka kwenye vyuo vyetu hivi, wameomba shilingi milioni 15. Naomba Waziri anipe ufafanuzi, wameweka vigezo gani vya kupunguza kiasi kikubwa kama hiki? Kupunguza ili elimu isiwafikie walengwa huko vijijini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha zilizotengwa ni ndogo lakini hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti ambayo imetubidi angalau tuwe tumewatengea kiasi hicho.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Community Development ... ... ... ... ... ... .. 1,491,396,200/=*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, fungu gani?

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 53, Programme* ya 20, Kifungu cha 2002 na kidogo kabisa 260500. Nilipokuwa nimechangia

kwa maandishi, nilizungumzia unyonge wa watumishi wa Idara ya Maendeleo kwamba hawapewi misaada ya kutosha ili kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunatekeleza Mkakati wa Kuondoa Umaskini au Kupunguza Umaskini, ziliteuliwa Idara chache ambazo ziliitwa Idara nyeti, kwa hiyo, zikawa zinapewa fungu la *Other Charges,* lakini, Idara ya Maendeleo ya Jamii haikuwemo pamoja na Idara nyingine ambazo hazikuonekana kwamba ni nyeti. Sasa wakati tunatekeleza MKUKUTA, je, hali itaendelea kuwa hivyo au pengine ndio hawa watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii sasa wanapewa fungu la *Other Charges* kwa ajili ya kuwasaidia katika safari za hapa na pale wanapofanya shughuli zao? Naomba msaada.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili analolizungumzia Mheshimiwa Elizabeth Batenga, linahusu *Travel and Subsistance* ya wafanyakazi wa Wizara. Wafanyakazi wa Maendeleo ya Jamii ambao wako chini ya Halmashauri, wanapata *OC* kutoka Halmashauri ambayo inapangiwa bajeti yake na Halmashauri ambayo na yeye Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe katika Halmashauri hizo kama mjumbe wa Kamati ya Fedha. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, wajitahidi kuwatengea Maafisa wa Maendeleo ya Jamii *OC* za kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anlivyosema, mimi ni mjumbe na ni Diwani, lakini katika Halmashauri hizo hizo anazosema au Halmashauri ile ambayo na mimi ni Diwani, Idara ya Afya inapata fungu, inapata ruzuku kutoka Serikali Kuu, Idara ya Elimu wanapata, Kilimo wanapata na Ujenzi wanapata. Sasa na hii vile vile kama tulivyozungumza ni Idara nyeti. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iweze kufikiria au itueleze ni kwa nini hii Idara isipate na yenyewe fungu kutoka Serikali Kuu hilo fungu la *Other Charges?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazingatia maelezo yake na kwamba tutashirikiana na TAMISEMI katika kuangalia tunamalizaje tatizo hili. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Community Development College, Tengeru... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...300,160,700/=*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu hilo la 53, Programu 20, Kifungu 2003, Kifungu kidogo 260800. Kwanza naomba niipongeze Wizara kwamba itachukua wanafunzi 810 kwenda Chuo cha Tengeru. Lakini fedha za kuwahudumia ziko wapi, maana katika kifungu hiki kidogo nilichotaja, fedha zilizopo ni shilingi milioni saba. Hawa vijana wanahitaji kuwa *sponsored* ili waweze kuhudhuria mafunzo kwenye Chuo hiki. Fedha za kuwa-*sponsor* ziko wapi?

Kwa hiyo, naomba ufafanuzi maana tunaweza tukapewa takwimu ya 810, lakini fedha zikatosha 10 tu. Naomba msaada.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili halikuwekewa chochote kwa sababu kutokana na wanafunzi wa Tengeru wanalipa ada. Kutokana na ada ndio zile shilingi milioni 25 ambazo tunategema kuzipata. Lakini pia sisi Wizara tunatoa fedha katika vifungu vingine kama *educational materials* na *supplies* na katika kipengele cha *other goods and services*, tunakuwa tunasaidia. Lakini tunategemea sana zile ada ambazo wanazitoa ili iweze nayo kuchangia katika kuendesha hicho chuo.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaelewa. Sijui kama Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba shilingi milioni 25 zinatosha kulisha na kulaza wanafunzi 810! Kama hivyo ndivyo, watamaliza mwaka wakiwa na utapiamlo. Naomba atufafanulie vizuri fedha zake zilivyokaa ili kumwezesha kuhudumia hii idadi kubwa ya wanafunzi ambayo anachukua kwenye chuo hiki. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Charles Keenja, kwamba, wanafunzi wa Tengeru wanapata *Sponsorship* wale wa *Private* na *Government* kutoka Wizara ya Elimu ya Juu. Kwa hiyo kutokana na hizo pesa wanazolipwa za *sponsorship*, ndio wanaweza wakalipia *school fees*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 – *Gender Development ... ... ... ... ... ... ... ... ...735,254,300/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Children Development ... ... ... ... ... ... ... ...501,313,000/=*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 53, Subvote 3002,* Kifungu kidogo 270300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto ni suala letu sote. Sasa kuna mkanganyiko ninauona, naomba nipatiwe maelezo. Watoto wa Mkoa wa Dar es salaam na Mkoa ninakotoka mimi Mkoa wa Pwani na Mikoa mingine wanapata manyanyaso makubwa sana katika usafiri wa kwenda shuleni na kurudi wa daladala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inashughulikia mitaala, lakini naona imejikita katika suala la kuzungumzia usafiri wa watoto hawa. Wakati sisi tunazungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania, tunamaana maisha hayo yaanzie kwa watoto wadogo.

Sasa je, Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nafasi yake ni ipi katika kuangalia usafiri wa watoto hawa na kuweza kuwapatia usalama na ulinzi wa kutosha kama ilivyoelezwa katika hotuba yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ingawa fungu hilo linahusu usafiri na usafiri kwa ajili ya wafanyakazi. Lakini kwa kuwa linahusiana na tatizo kubwa la usafiri na sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii kama sekta Mtambuka, hebu Mheshimiwa Waziri angalau tuambie mnaweza kushirikiana namna gani na Wizara mtambuka kutatua tatizo hilo!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuuru Mheshimiwa Zaynab Vulu, mdogo wangu kwa kuniuliza swali hili. Nashukuru kwa jinsi alivyo mstari wa mbele katika masuala ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafiri kwa watoto Dar es Salaam ni mtambuka na ni Wizara nyingi zinahusika. Lakini kwa upande wangu nikiwa kama Waziri wa Maendeleo ya Jamii, ningependa nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kila Kata, ina shule zaidi ya mbili za *Primary School*. Kwa hiyo, watoto wa *Primary School* wa Mkoa wa Dar es Salaam, ili kupunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi katika daldala, watoto wanaosoma *Primary School* Dar es Salaam, wanatakiwa wasome katika Kata wanazotoka, hivyo hakutakuwa na sababu ya watoto hawa kupanda mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mzazi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ni wazazi. Siku moja ukipanda daladala uone vile vitoto vya miaka, tano, sita, saba, nane, vinavyobanana kwenye daladala wakienda shule. Mle ndani wananyanyaswa, ni kweli nakubaliana naye. Lakini tatizo hili ni sisi wazazi wa Mkoa wa Dar es Salaam tunatakiwa tuisaidie Serikali, ili Serikali iangalie jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa Sekondari ambao kweli shule ziko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa hapa niwaase wazazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba wajitahidi, waache kutoa mtoto Mbagala kuja kusoama *Kisutu Primary School,* atoke Kimara aje asome Upanga au Muhimbili, wakati kule zipo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wamenisikia na nadhani Mheshimiwa Mbunge ataridhika na hayo kwamba watoto tuwapende, katika kuwapenda basi tusipende watoto watoke asubuhi saa 11.00 alfajiri, anarudi saa 3.00 usiku kutoka shule mtoto wa *Primary School,*si vyema. Kwa hiyo, tupunguze tatizo hili kwa kuwatafutia shule zilizo karibuni. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kabla ya Lucy Mayenga, Mheshimiwa Waziri lakini nafikiri bado tuombe tu mtusaidie kwa sababu yako matatizo ambatanishi kama viwanja kujaa, shule kujaa na nini… Lakini tulichukue kama *agenda* nyingine pia ya kuendelea kujadili.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimesimama tena katika *Vote 53,* kifungu hiki cha maendeleo ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maendeleo ya watoto ni suala ambalo mtoto anatakiwa aangaliwe kuanzia katika ngazi ya chini kabisa ikiwepo kuanzia masuala ya afya, elimu pamoja na vitu vyote vinavyomhusu mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga jamii iliyobora, hatuna budi na Serikali haina budi kwa kupitia Wizara hii, kuweza kuhakikisha kwamba watoto wanaangaliwa kuanzia ngazi ya shule za chekechekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi au kuweza kujua kuhusu suala lifuatalo:-

Mheshimiwa Rais wakati akifungua Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema yafuatayo: "Serikali itachukua hatua za kuhakikisha kuwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, labda kwa kuwa ulishasoma, hebu tuambie tu ufafanuzi, nenda moja kwa moja kwenye ule ufafanuzi ambao unataka Mheshimiwa Waziri akupe. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wangu ni kwamba Serikali inatakiwa iangalie kuanzia ngazi ya chini kabisa kuhusu maendeleo ya watoto katika ngazi zote, lakini Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, je, imejiandaa vipi kuweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba inamlea mtoto huyu wa Kitanzania kuanzia ngazi ya chini ikiwepo kuhakikisha kwamba hizi shule za chekechea zinaangaliwa upya na kuweza kujua kwamba ziko katika utaratibu unaofaa kwa sababu hivi sasa shule hizi zimeachiwa jukumu la sekta binafsi, watu binafsi ndio ambao wamekuwa wakiendesha shule hizi. Kwa maana hiyo jamii ambayo tumekuwa tukiilea imekuwa ni jamii ambayo inakuwa ni jamii isiyokuwa katika utaratibu mmoja unaofahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, kutokana na agizo hili la Rais, Wizara hii imefikia wapi kuweza kuhakikisha kwamba mambo haya yanafanywa sambamba na suala la kuhakikisha kwamba watoto yatima wanaweza kuhudumiwa kwa sababu wamepewa muda kwamba waweze kutekeleza suala hili na mkakati huu waweze kuupeleka kwa Rais katika kipindi cha muda mfupi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, watoto mtawaleaje toka wakiwa wadogo mpaka wanakuwa wakubwa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Kwanza niseme tu kwamba suala la ulezi wa watoto ni suala la familia. Kila mmoja wetu anayetaka kuleta mtoto hapa duniani, awe na uhakika wa kuweza kumhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kufuatana na agizo tulilopewa na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, sisi Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto tukishirikiana na wadau wengine wakiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii,

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tumeanza kuandaa mkakati wa kuhudumia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imepanga kufanya yafuatayo kwa kutumia fedha za MKUKUTA na fedha za ziada kutoka wahisani:-

(i) Kushughulikia watoto wanaoombaomba *(Street Children);*

(ii) Kuanzisha Mfuko Maalum wa Kitaifa wa kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika ngazi ya Kitaifa na Halmashauri;

(iii) Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto na Sera ya Maendeleo ya Familia; na

(iv) Kuratibu juhudi mbalimbali zinazofanywa, zinazohusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili kuwa na mkakati wa pamoja wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuhakikisha kuwa watoto hawa wanapatiwa haki zao za msingi na kuwa na maisha bora kama watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni juhudi za kuzibia pengo kwa wale ambao kwa kweli wanahitaji mahitaji ya Serikali lakini sisi tunatakiwa tuhamasishe jamii ili tushiriki sote katika kuhakikisha hata watoto yatima wanapata malezi bora.

Ningependa kusema tu watoto yatima kuwapeleka kwenye vituo au kulelewa na mtu mwingine iwe ni jambo la mwisho kabisa. Ni vyema watoto yatima wakilelewa na jamii kwa sababu watoto yatima wakikaa kwenye *Institution,* baada ya miaka 18 wakiondoka pale hawajui waende wapi. Kwa hiyo, ni vyema watoto yatima wangeishi katika jamii ili wawe sehemu ya jamii. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 – *NGOs Coordination …………………..… ... 124,938,600/=*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 53, Programme 40, Subvote 4001,* Kifungu kidogo cha 260800, *Training Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mahitaji makubwa ya *NGOs* ziliozopo nchini Tanzania na tunaona kifungu hiki kinashughulikia *Coordination* na *Training* za *NGOs*. Sasa pesa zilizotengwa ni shilingi 2,800,000/=. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, pesa hizi zinaweza zikatosha katika ku-*train* na kusaidia hizi *NGO's* kielimu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba ni kweli fedha hizi

ambazo zimetengwa katika Idara nyingi za Wizara yangu, hazitoshi. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti imebidi iwe hivi. Tutajitahidi kutekeleza yale ambayo yanawezekana na yale ya muhimu zaidi. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko hapo hapo kwenye programu ya 40, *Subvote 4001,* Kifungu kidogo sijui, kwa sababu ninachotaka kuongea naomba mnitafutie ni kifungu gani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nilishawahi kuongelea *NGOs* kwamba kuna *NGOs* nyingi zinakuja na zinafanya kazi hapa, nyingine ni za halali lakini nyingine zinakuja zinapiga picha kama watoto wetu, akinamama wajawazito, wanaobeba maji vijijini, wanaobeba kuni. Zile picha zinachukuliwa, wanapata pesa huko Ulaya, lakini zile pesa hazitumiki huku kwa walengwa ipasavyo. Sijui ni kifungu gani kinachohusika ili nipate kuweza kutatua hizo *NGOs?* Ni nani anayehusika kudhibiti hizi *NGOs?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hebu tusaidie. Unaweza kumpa maelekezo Mheshimiwa Sameer Lotto, katika kifungu hiki kwa sababu *NGOs* zimejigawa katika Wizara mbili tofauti, hebu tuambie katika Wizara yako.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema kwamba ziko *NGOs* nyingine pengine zinapita tu hazirudi na ni kweli tatizo hilo limetokea na ndiyo maana Serikali imeweka Sera ya *NGOs* na pia kwa sasa tumetunga sheria ambayo inashughulikia *NGOs,* sheria namba nne ya mwaka 2002. Kwa sasa bado tunatengeneza Baraza la *NGOs* limeundwa na linatengeneza kanuni na taratibu ambazo zitatakiwa kufuatwa. Pia ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba *NGOs* zinapokuja katika maeneo yenu ni vyema muwashauri waende kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, wao pale ndiyo waratibu wa masuala yote ya jamii na hivi ni vyombo vya jamii. *(Makofi)*

Vile vile ningependa kumfahamisha kwamba *NGOs* hizi zinakuwa *registered* kwenye sheria nyingi. Wizara yangu inasimamia sheria ya *NGO* hii mpya ya mwaka 2002. Lakini pia kuna Sheria ya Vyama vya Hiari *Cap 337* ambayo pia inasajili *NGOs.* Pia Sheria ya Makampuni *Cap 212* pamoja na marekebisho yake na pia Sheria ya Wadhamini *(Trustees Incorporation Act) Cap 375.* Kwa hiyo, zipo sheria mbalimbali ambazo zinasajili hizi *NGOs.* Lililopo ni kwamba wanapofika maeneo yetu tuwaulize wanafanya nini na nadhani Afisa Maendeleo ya Jamii atakuwa katika nafasi nzuri ya kukufahamisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sameer Lotto, bado?

**MHE. SAMEER I. LOTTO** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kujua ni kwamba kama wanapata pesa au hawapati pesa. Maana wanaweza hata huyo Afisa wetu wa Maendeleo ya Jamii wakaja wakazungumza naye, wakazungumzia nia yao na

madhumuni yao. Lakini kama wanapata pesa huko nje, ni vipi tunaweza tukajua kama kweli pesa zimepatikana au la? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri Mheshimiwa Waziri ametuambia, sisi kama Wabunge katika maeneo yetu tujitahidi kujua wale wanapokuja kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii tujue, tuwe karibu nao na ukizingatia kwamba *NGOs* za Wizara hii ziko katika ile sheria iliyounda *NGO* ya mwaka 2002, lakini ziko nyingine ambazo haziko chini ya sheria hiyo na Wizara hiyo. Kwa hiyo, cha msingi tubanane nao pale na wale Maafisa Maendeleo ya Jamii halafu tunaweza kujua hizo taarifa vizuri zaidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza *Volume II* na sasa tunaingia *Development Book.*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... ... ... ... ...737,952,000/=*
Kifungu 1003 - *Policy and Planning ... ... ... ... ... ... ... ... ... 140,292,000/=*
Kifungu 2001 - *Training and Folk Dev. College. ... ... ... ... 253,571,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Community Development ... ... ... ... ... ... ...464,966,000/=*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Fungu 53, *sub-vote 2002,* kifungu kidogo cha 6229, *public buildings.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Waziri kwa taarifa yake nzuri ambayo nimeisoma katika kitabu hiki hasa inayohusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Buhare. Ameonyesha kwamba chuo hicho ambacho kilikuwa kinatoa *Certificate,* mwaka kesho 2007/2008 kitaanza kutoa *Diploma*. Kwa bahati mbaya sana hiki chuo hakina hata *fence* wala hakina gari. Lakini bahati nzuri hapa, Mheshimiwa Waziri amesema na naomba kunukuu: “Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Wizara yangu itafanya ukarabati mkubwa katika Chuo cha Buhare.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba nimejaribu kufunua vitabu vyote hivi kila mahali kuona hizi fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa, lakini sijaona hata sehemu moja, tofauti na vyuo vingine kama Tengeru, fedha zinaonekana. Kwa hiyo, nilitaka tu ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kwamba hizo fedha ambazo zometengwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Chuo cha Buhare ziko katika kifungu gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Fedha za ukarabati ziko chini ya *sub-vote 2002, Public Buildings,* ndiyo *Community Development* ni kiasi cha shilingi 464,966,000/=. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ziko humo, bado kuna swali la nyongeza?

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wasiwasi wangu ni mdogo sana kwamba ukiangalia hapa imeandikwa tu *Public Buildings* ndiyo imewekewa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia kwenye vyuo vingine kama Tengeru fedha zimetengwa kabisa. Sasa hapa kwenye Chuo cha Buhare ambapo inaonekana kwamba kinahitaji matengenezo makubwa ndiyo nilitaka kujua hivi ni shilingi ngapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *sub-vote 2002, Community Development.* Hizi pesa nilizosema shilingi 464,966,000/= ni kwa sababu ya matengenezo ya vyuo vitatu vya Misungwi, Buhare na Lungemba, isipokuwa chuo ambacho kimetengewa pesa zake peke yake ni cha Tengeru ambacho kinafuata huku mbele kwenye *sub-vote 2003.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Community Development College,Tengeru... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..524,220,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu wake na timu yake nzima kwamba sasa bajeti yenu imepitishwa rasmi na Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru na nafikiri sasa ni mwisho wa shughuli zetu za leo. Lakini naomba niseme kwamba nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mlionipa na hasa katika siku yangu ya kwanza ya kupitisha mafungu ya Wizara kwa leo. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema maneno haya, naomba sasa niahirishe shughuli zetu hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 2 Agosti, 2006 saa tatu asubuhi)*